# Nipashe

Jumanne Septemba 27, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581081

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




**ISHA MASHAUZI ATAFUTA MUME**

UKURASA 27


SUPA JACKPOT
TZS. 1,034,905,195
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




**Mbaroni** kwa tuhuma uzushi wa kifo cha Mwakyembe

UKURASA 3

# Padri kizimbani mahakama mbili

• **Kesi** tatu zafunguliwa dhidi yake, ni anayetuhumiwa kunajisi watoto... *Endelea ukurasa 2*



Paroko wa Parokia Teule ya Mtakatifu Dionis Aropagita ya Jimbo Katoliki la Moshi, Padri Sosthenes Bahati, alipofikishwa katika mahakama mbili tofauti za Mkoa wa Kilimanjaro jana, akikabiliwa na mashtaka ya kunajisi watoto. **PICHA: MARY MOSHA**



## Masharti wasio na uwezo Bima ya Afya kwa Wote yaja

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**BABA JELA MAISHA KUMNAJISI MWANAWE**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza imemhukumu kifungo cha maisha jela Alphonce Ngassa...

UKURASA WA 5

**UPELELEZI KESI YA OLE SABAYA NGOMA MBICHI**

UPANDE wa utetezi katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai ole Sabaya...

UKURASA WA 5

**WAZIRI ATAJA SIRI ONGEZEKO WATALII**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, amesema idadi ya watalii imeongezeka kutoka...


## Ziara ya Rais Samia Msumbiji yaleta neema

UKURASA 3


MICHEZO **TOYOTA IST KUTOLEWA SUPA JACKPOT J'MOSI** UK.31

**KABWELA** UK.7

# Padri kizimbani mahakama mbili mashtaka ya kunajisi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

PAROKO wa Parokia Teule ya Mtakatifu Dionis Aropagita ya Kanisa Katoliki Jimbo la la Moshi, Padri Sosthenes Bahati (41), amefikishwa katika mahakama mbili tofauti kwa kesi za madai ya kunajisi watoto watatu wenye umri chini ya miaka 12.

Padri Bahati alifikishwa jana katika Mahakama ya Wilaya ya Moshi akikabiliwa na shtaka moja na katika Mahakama ya Mkazi Moshi kwa mashtaka mawili.

Katika kesi ya kwanza, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi Salome Mshasha, Wakili wa Serikali Kassim Nasri, alidai kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Agosti 12, mwaka huu, akiwa ofisini kwake.

Wakili Nasri alidai mahakamani hapo kwamba mshtakiwa alitenda makosa hayo huku akijua ni kinyume cha Kifungu cha 130 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu.

Wakili Nasri pia alidai kuwa katika kesi hiyo namba 45 ya mwaka 2022 mshtakiwa kwa makusudi, alimbaka mtoto huyo (jina linahifadhiwa).

Baada ya kusomewa shtaka hilo, Padri Bahati alikana na Hakimu Mshasha akaahirisha shauri hilo hadi Oktoba 10, mwaka huu, kesi hiyo itakapotajwa kwa ajili ya kumsomea maelezo ya awali.

Hata hiyo, mshtakiwa Padri Bahati, alikosa dhamana baada ya kudaiwa barua za utambulisho za watu wawili waliopaswa kutia saini dhamana ya Sh. milioni 10 kila mmoja.

Katika kesi ya pili, namba 44 ya mwaka 2022 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi mbele ya Hakimu Mkazi Jennifer Edward, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Kambarage Samson, akisaidiana na Verdiana Mlenza, alidai mshtakiwa alimbaka mtoto wa miaka 12.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Agosti, mwaka huu, kinyume cha kifungu cha 130 na 131 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu.

Baada ya kusomewa shtaka hilo, Padri Bahati alikana shtaka dhidi yake na Hakimu Jennifer alisema dhamana iko wazi kwa mujibu wa sheria.

Kesi hiyo itatajwa tena Oktoba 18, kwa ajili ya kusomewa maelezo ya awali.

Katika shtaka la tatu lililosomwa katika Mahakama ya Wilaya ya Moshi mbele ya Hakimu Mfawidhi Erasto Philly, ilidaiwa kuwa Padri Bahati alimbaka mtoto (jina linahifadhiwa).

Akisoma hati ya mashtaka, Mwendesha Mashtaka Verediana Mlenza, alidai mshtakiwa alitenda kosa hilo Agosti, mwaka huu.

Hata hivyo, mshtakiwa alikana shtaka dhidi yake na kesi kuahirishwa hadi Oktoba 12, mwaka huu.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kushoto) na Waziri wa Nchi wa Mambo ya Fedha wa Nchi za Falme za Kiarabu, Mohamed Bin Hadi Al Hussaini, wakionesha mkataba wa makubaliano ya kuondoa utozaji kodi mara mbili na kuzuia ukwepaji wa kodi ya mapato kati ya nchi hizo mbili, mjini Dubai, Falme ya nchi za Kiarabu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ummy: Saratani bado ni janga

**Pilly Kigome na Saumu Hassan, DSJ**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema saratani bado ni janga nchini kutokana na Watanzania wengi kupoteza maisha kwa sababu ya ugonjwa huo.

Mwaka juzi, zaidi ya Watanzania 25,000 walifariki dunia kutokana na saratani kulinganisha na UVIKO-19 ambao hawakuzidi watu 1,000 waliofariki dunia.

Ummy alisema hayo jana Dar es Salaam, katika uzinduzi wa taarifa ya Hali ya Ugonjwa wa Saratani katika nchi zilizo kusini mwa jangwa la Sahara kwa upande wa Afrika Mashariki.

Utafiti huo uliotolewa na Lancet ulisema saratani katika nchi za Afrika Mashariki ni mbaya na idadi inaongezeka na kufafanua kuwa watu milioni 10 duniani walifariki dunia kwa ugonjwa huo.

Alisema taasisi hiyo imetoa mapendekezo mbalimbali kuishauri Wizara ya Afya ambayo yatasaidia kukabiliana na ugonjwa huo nchini. Ummy alisema moja ya mapendekezo hayo ni kupanga mipango mizuri ya kudhibiti ugonjwa huo.

Ushauri mwingine ni kuboresha upatikanaji wa takwimu za hali ya saratani nchini, kutoa ushauri wa upatikanaji wa huduma bora za matibabu bila tatizo la fedha kwa wagonjwa wa saratani.

Pia wizara imeshauriwa kuboresha huduma za matibabu na huduma za tiba shufaa, kutengeneza wataalamu wazuri wa huduma bora za saratani. Jambo lingine ni kuwekeza katika utafiti na ubunifu ili kukabiliana na ugonjwa huo.

Utafiti huo jumuishi uliohusisha nchi 46 umesema inatakiwa juhudi na mikakati madhubuti kufanyika kwa haraka kwa kuwa ifikapo mwaka 2030 wagonjwa milioni moja wanaweza kupoteza maisha kutokana na ugonjwa huo.

Waziri Ummy alisema serikali imepokea mapendekezo hayo na juhudi za haraka zitafanyika kudhibiti pia homa ya ini ambayo inakuja kwa kasi nchini.

Alisema kuelekea Siku ya Ukimwi Duniani, Desemba Mosi, Wizara ya Afya itazindua Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi, Homa ya Ini na Magonjwa ya Ngono.

Alisema homa ya ini inaenea kwa kasi kwa kuwa inaweza kuaambukizwa kwa jasho na hata kushikana mikono pia.

# Masharti wasio na uwezo Bima ya Afya kwa Wote

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MUSWADA wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote umependekeza watu wasio na uwezo, kutengenezewa vyanzo mahususi kwa ajili ya kugharamia bima ya afya.

Kwa mujibu wa muswada huo unaolenga kutunga Sheria Namba 8 ya Mwaka 2022, baada ya kanuni kutungwa, Waziri mwenye dhamana (Waziri wa Afya) kwa kushirikiana na mamlaka zinazohusika, na kwa kupitia kanuni, atatangaza utaratibu na namna ya kuanza kwa utambuzi wa watu wasio na uwezo.

Kifungu cha 22(2) cha muswada huo kinafafanua kuwa watu watakaotambuliwa kama watu wasio na uwezo, watakuwa na haki ya kujumuishwa chini ya skimu ya bima ya afya kwa namna itakavyoainishwa kwenye kanuni.

Vilevile, muswada huo unaeleza kuwa waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha, kwa kushauriana na Waziri wa Afya, ataainisha vyanzo mahususi kwa ajili ya ugharamiaji wa huduma za bima ya afya kwa watu wasio na uwezo.

Muswada huo ulisomwa kwa mara ya kwanza bungeni jijini Dodoma Septemba 23, mwaka huu na Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi.

Tayari muswada huo umepelekwa katika kamati husika kwa ajili ya kuchambuliwa na kujadiliwa na baada ya hapo Spika wa Bunge atapatiwa taarifa kuhusu kazi hiyo.

**MATIBABU POPOTE**

Kuhusu wigo wa upatikanaji wa huduma za afya ambazo zamani mnufaika alikuwa na ukomo wa hospitali anazoweza kupata huduma, sasa serikali inapendekeza mwanachama au mnufaika kupata huduma za afya mahala popote katika kituo cha kutolea huduma za afya kilichoingia mkataba na skimu ya bima ya afya kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya.

Kulingana na madhumuni ya sheria hiyo uanachama na uchangiaji katika skimu ya bima ya afya sasa utawajumuisha watu wote ambao kabla ya kuanza kutumika kwa sheria, walikuwa wanachama wa skimu ya bima ya afya kama ilivyoainishwa katika sheria zinazosimamia skimu husika.

Wengine watakaojumuishwa ni watu wote ambao katika tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hiyo watakuwa wametimiza umri wa miaka 21 na watu wote ambao kwa tarehe ya kuanza kutumika kwake watakuwa chini ya umri wa miaka 21, lakini wana sifa za kusajiliwa kuwa wanachama.

Wamo pia watu wote walioajiriwa katika sekta binafsi au ya umma, watu wote waliojiajiri, watu wasio na uwezo na makundi mengine ya watu kadri itakavyoainishwa na waziri katika kanuni.

Pia wamo watu kutoka sekta rasmi binafsi au sekta isiyo rasmi watakaojiunga na skimu ya bima ya afya yoyote.

Katika muswada huo inapendekezwa kuwa mwajiri wa sekta ya umma na binafsi rasmi, atapaswa kumsajili mwajiriwa katika skimu ya bima ya afya ndani ya siku 30 tangu kuanza kwa mkataba wa ajira.

Iwapo mwanachama anachangia kwa utaratibu wa michango kwa mwaka atafariki dunia, wategemezi wake wataendelea kunufaika na huduma kwa kipindi kilichosalia cha mkataba wa uanachama.

Muswada huo ulisomwa kwa mara ya kwanza bungeni jijini Dodoma Septemba 23, mwaka huu na Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi.

Tayari muswada huo umepelekwa katika kamati husika kwa ajili ya kuchambuliwa na kujadiliwa na baada ya hapo Spika wa Bunge atapatiwa taarifa kuhusu kazi hiyo.

## HABARI KITAIFA

# Ziara ya Samia Msumbiji yaleta neema

**Na Elizabeth Zaya**

BALOZI wa Msumbuji nchini, Ricard Mtumbuida, amesema Tanzania itanufaika kiuchumi, kisiasa na kijamii kutokana na ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan (pichani) nchini humo.

Kwa mujibu wa taarifa yake kwa umma, alisema uhusiano wa nchi hizo ni wa kihistoria na kwamba kwa sasa kuna tatizo la ugaidi linalohitaji kushughulikiwa kwa haraka.

Alisema faida zilizopatikana baada ya Rais Samia kufanya ziara nchini Msumbiji hivi karibuni zitakuwa na manufaa kwa pande zote.

"Watu wanafahamu kuwa kihistoria, Tanzania na Msumbiji ni ndugu wa damu, si ndugu wa kusema hususani mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma na kwingineko ambako tumejaa. Msumbiji pia maeneo mengi wanapatikana Watanzania.



"Rais Samia kukutana na ndugu yake Rais Filipe Nyusi kulikuwa na faida nyingi sana. Watu wanakumbuka Mapinduzi ya Zanzibar ambayo Msumbiji walishiriki. Kuungana kwa Tanganyika na Zanzibar, Msumbiji pia walishiriki. Uhusiano wa nchi hizi ulianza kushuka kidogo, hivyo ujio wa Rais wa Tanzania umeinua ari mpya na milango yote inafunguka," alisema.

Alisema changamoto kubwa ya Msumbiji ni ugaidi na kwamba magaidi wanaofanya machafuko wanapitia njia ya Tanzania, hivyo ushirikiano unahitajika na tayari wameamua kupambana pamoja kwa nchi zote mbili ili kuimarisha amani.

Pia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ilisema maeneo mengine ya ushirikiano ni mambo ya nje, ulinzi, usalama, mawasiliano, uhakiki wa mipaka, biashara, viwanda, maliasili, kilimo na madini na kubadilishana wanafunzi.

Kadhalika, kulifanyika mikutano ya ulinzi na usalama kwa ajili ya kudumisha uhusiano baina ya pande hizo mbili na mkakati wa kubadilishana ujuzi na uzoefu wa masuala mbalimbali ikiwamo sekta ya gesi asilia.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mabrouk Mabrouk, viongozi wakuu wa nchi hizo waliagiza kufanyika mkutano wa tume ya kudumu ya pamoja kati ya nchi hizo.

"Hii mikutano ya ushirikiano ni muhimu kukuza na kudumisha uhusiano wa nchi mbili. Bahati mbaya kwa muda mrefu hii tume ilikuwa haijakutana lakini Septemba 22 hadi 24, mwaka huu ulifanyika jijini Dar es Salaam, ulikuwa mkutano wa 15.

"Tanzania na Msumbiji zina uhusiano wa kidugu sana. Pamoja na udugu walio nao, takwimu zinaonyesha kuwa juhudi zinatakiwa kuboresha ili kuleta tija zaidi," alisema.

# Mbaroni tuhuma kuzusha kifo cha Dk. Mwakyembe

**Na Halfani Chusi**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limewakamata watu wawili kwa tuhuma za uhalifu wa kimtandao ikiwamo kuzusha kifo cha mwanasiasa na Waziri wa zamani wa Katiba na Sheria, Dk. Harrison Mwakyembe (pichani).

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, jeshi hilo pia lilibainisha kuwa tuhuma zingine za uhalifu wa kimatandao ni za kujinasabisha kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas.

Jeshi hilo lilisema linamewakamata watuhumiwa hao wawili kwa tuhuma hizo za makosa ya kimtandao kufuatia msako linaloendelea kuufanya kwa kushirikiana na kikosi kazi maalum cha kupambana na makosa ya kimtandao.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo iliyotolewa na Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, mtuhumiwa wa kwanza ni Innocent Chengula (23), mkazi wa Kigogo Luanga, aliyekamatwa kwa tuhuma za kujinasabisha kuwa yeye ni Dk. Abbas, Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kupitia mtandao na kutumia laini za simu zenye usajili usio na majina yake.



"Mtuhumiwa huyu amekuwa akiweka picha na majina ya Dk. Hassan Abbas katika maelezo ya ukurasa wake mitandaoni ya kijamii na kutuma ujumbe kwa watu akiwaomba wamtumie fedha kwenye namba tofauti za simu.

"Mfano, amekuwa akituma ujumbe unaosomeka "Kaka naomba niazime milioni 3, Alhamis nitakurudishia" na mwingine unaosomeka "kaka nina mtoto wangu naomba umpatie kazi apo kwako yeye amesomea Bachelor of Commerce in Accounting"," Kamanda Muliro alidai.

Jeshi la Polisi pia limemkamata Tazarn Mwambengo (27), mkazi wa Ukonga, anayetuhumiwa kusambaza taarifa za uongo kuhusu kifo cha Dk. Mwakyembe kupitia chaneli ya televisheni ya mtandaoni.

Kamanda Muliro alisema kuwa katika chaneli hiyo ya mtandaoni, mtuhumiwa huyo anadaiwa kuandika "BREAKING NEWS: HUZUNI YATANDA MAZISHI YA MWAKYEMBE".

Kamanda Muliro alisema taarifa hizo ziliibua taharuki kubwa kwa wananchi hasa kwa Dk. Mwakyembe mwenyewe na familia yake.

Alisema watuhumiwa hao wamekutwa wakiwa na vifaa mbalimbali wanavyodaiwa kuvitumia kufanya uhalifu huo, ikiwamo kompyuta mpakato (laptop), simu tatu, kipaza sauti kwa ajili ya matangazo ya redio au televisheni (mike), modemu moja na kadi za simu za mitandao mbalimbali tisa zenye usajili wa majina tofauti.

Alisema Jeshi la Polisi linatoa rai kwa Watanzania kuwa makini na matumizi ya mitandao ya kijamii pamoja na kuzingatia maadili ya taaluma ya habari na sheria zinazohusika kuepuka kuchapisha taarifa zitakazozua taharuki kwa umma.

Kamanda Muliro pia aliwataka Watanzania kuchukua tahadhari wakati wa kutuma fedha au kufanya miamala kwa njia ya simu ili kuepuka kutapeliwa, akisisitiza Jeshi la Polisi halitasita kuchukua hatua dhidi ya watu wote watakaovunja sheria, kanuni na miongozo inayoelekeza matumizi sahihi ya mitandao.



# Baba jela maisha kumnajisi mwanawe gesti

**Na Richard Makore,** MWANZA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza imemhukumu kifungo cha maisha jela Alphonce Ngassa, maarufu kama Dutwa (51) kwa kumnajisi mtoto wake wa kike mwenye miaka tisa (jina limehifadhiwa).

Mshtakiwa huyo alihukumiwa kifungo hicho baada ya kutiwa hatiani kwa kumweka binti yake katika nyumba ya kulala wageni na kumfanyia vitendo hivyo mwezi mzima huku akimziba mdomo asipige kelele.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mwandamizi Juma Mpuya, alisema mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo mwishoni mwa mwaka jana.

Hakimu Mpuya alisema mashahidi sita, akiwamo mtoto aliyefanyiwa kitendo hicho, walitoa ushahidi katika mahakama hiyo.

Kutokana na ushahidi uliotolewa mahakamani hapo, alisema mahakama imejiridhisha pasipo kuacha shaka kwamba mshtakiwa alitenda kosa hilo, hivyo kumtia hatiani.

Mahakama hiyo ilielezwa kuwa, mshtakiwa huyo alimchukua binti yake huyo kutoka Kahama mkoani Shinyanga alikokuwa anaishi na mama yake mzazi ambaye walitengana na kwenda naye Jijini Mwanza kwa ahadi ya kwenda kumnunulia viatu vya kanisani.

Aidha, ilidaiwa kuwa ahadi hiyo haikutekelezwa na mshtakiwa badala yake alimpeleka kwenye nyumba hiyo ya kulala wageni na kuanza kumfanyia vitendo hivyo.

Taarifa za mtoto huyo kufanyiwa unyama huo zilitolewa na mtu aliyejulikana kwa jina la Minja, ambaye alibaini mwenendo wa mtoto huyo haukuwa sawa na kuanza kumdadisi ndipo akamwambia kuwa baba yake mzazi alikuwa akimfanyia vitendo hivyo.

Minja alidai katika mahojiano, mtoto huyo alikiri kufanyiwa vitendo hivyo, huku akidai baba yake alikuwa akimziba mdomo wakati akimnajisi ili asipige kelele.

Kutokana na hali hiyo, Minja alimpeleka mtoto huyo kituo cha polisi na kufungua kesi namba 162 ya mwaka 2021 ya ubakaji na kupewa fomu namba 3 ya polisi kisha akampeleka hospitalini.

Majibu ya daktari aliyemfanyia vipimo yalionyesha kuwa binti huyo aliingiliwa mara nyingi na sehemu zake za siri zilikuwa katika hali mbaya.

Daktari aliyempima alitoa ushahidi wake mahakamani hapo ikiwamo kuwasilisha fomu hiyo namba tatu ya polisi kama kielelezo.

Baada ya mahakama kujiridhisha na ushahidi wote uliotolewa na mashahidi sita akiwamo mtoto mwenyewe, ilitoa nafasi kwa mshtakiwa kujitetea kutokana na shtaka linalomkabili, lakini alikataa kujitetea.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Ghati Mathayo, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa kutokana na kufanya kitendo kibaya dhidi ya mtoto wake wa kumzaa ambaye ni mdogo na kumharibu sehemu zake za siri, na kumharibu kisaikolojia kwa kumnajisi mwezi mzima.

Kutokana na ushahidi pamoja na maelezo ya mwendesha mashtaka, mahakama ilimhukumu kifungo cha maisha jela.



Mwenyekiti wa Bodi ya Ewura, Prof. Mark Mwandosya (katikati), Makamu Mwenyekiti wa Bodi, Ahmad Kilima (kushoto) na Mjumbe, Richard Kayombo (kulia) wakiwa pamoja na watumishi wa Ewura Kaya ya Mashariki (Dar es Salaam) baada ya kikao jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Sakata aliyekufa kwa madai kugongwa gari la Magereza lachukua sura mpya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SAKATA la ndugu wa Richard Bukombe mkazi wa Miyuji jijini Dodoma, aliyefariki dunia kwa madai ya kugongwa na gari la Jeshi la Magereza limechukua sura mpya baada ya wanafamilia kumtaka mkuu wa jeshi hilo kutowakingia kifua wahusika.

Pia wameiomba Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kuingilia kati sakata hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapo kwa niaba ya familia, mdogo wa marehemu, Bukombe Bulole, alisema pamoja na kuzika mwili wa ndugu yao, hawatakata tamaa ya kupata haki ya ndugu yao.

Baada ya kuuzika mwili wa ndugu yao, alisema walifuatilia katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma na kubainika kuwa mwili wa ndugu yao ulipelekwa na kutelekezwa katika chumba cha kuhifadhia maiti na askari Magereza.

"Kamishna (Jenerali) anapaswa kulifanyia kazi hili kwani liko mikononi mwake. Asiwape kazi viongozi wake wa juu kwa ajili ya kuwalinda wahusika. Tunamwomba sana atusaidie, hakuna haja sisi kumfuata Waziri Mkuu au Rais Samia Suluhu Hassan afanye kitu ambacho ni jukumu la mteule wake," alisema Bukombe.

Alisema kuendelea kukaa kimya kwa Jeshi la Magereza kunazidi kuwapa hofu kuwa ndugu yao alipogongwa na gari hakuwa amekufa bali wao ndio waliommalizia ili kuondoa ushahidi.

"Ndugu wanahabari, Sheria ya Usalama Barabarani kifungu cha 57 (ii) (b) kinamtaka mtu yeyote atakayesababisha ajali aripoti kituo cha polisi ndani ya saa 12 ila sheria itamsamehe akichelewa endapo kutokana na ajali hiyo atakuwa hawezi kutimiza takwa la sheria hiyo.

"Lakini kifungu cha 40 sura ya 168 kilichofanyiwa marekebisho mwaka 2002 inasema mtu yeyote atakayesababisha majeruhi au kifo kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani atakuwa ametenda kosa la jinai," alisema.

Bukombe alisema kwa kuwa Magereza ni miongoni mwa vyombo vinavyohakikisha sheria za nchi hazivunjwi na kwa kutoripoti ajali ile kituo cha polisi, wamevunja sheria.

"Hivyo askari Magereza ambao ni wasimamizi wa sheria za nchi wametenda kosa la jinai na tunawaomba viongozi wao wawafikishe mahakamani mara moja bila kusumbua vyombo vingine vya usalama kuchunguza jambo hilo," alisisitiza.

Pia alisema familia inamwomba Mkuu wa Magereza aige mfano wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, aliyoruhusu sheria ifuate mkondo wake kwa mtoto wake ambaye alivunja sheria za nchi.

Bukombe alisema tangu ajali ilipotokea Septemba 13, mwaka huu, hadi sasa zaidi ya siku 14 zimepita bila kuona chochote kilichofanywa na jeshi hilo zaidi ya danadana za kivuta muda ili wasahau na kuacha kufuatilia jambo hilo.

Richard Bukombe, maarufu kwa jina la Baba Paroko, anadaiwa kugongwa na gari la Jeshi la Magereza (Landcruiser pickup) Septemba 13, mwaka huu, jirani na eneo la Hoteli ya Twiga, Msalato jijini hapo.

Kwa mujibu wa ndugu zake, aligongwa na gari hilo majira ya saa 12:30 jioni na baadhi ya askari wa jeshi hilo walimchukua na kuondoka naye kisha baadaye mwili wake kukutwa umetelekezwa mochwari.

Mkuu wa Magereza Mkoa wa Dodoma, Kenneth Mwambije, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alikiri kuwa analifahamu kama ambavyo watu wengine wanavyolisikia lakini akasisitiza kuwa watu wa kulitolea ufafanuzi ni makao makuu ya jeshi hilo.

Wiki iliyopita, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alisema anaomba kwanza kukutana na wanafamilia ili kusikiliza malalamiko yao.

# Asimulia mwili ulivyofungwa kamba, plasta

**Na Grace Gurisha**

DAKTARI Bingwa wa Magonjwa ya Binadamu na Vifo vya Mashaka, Innocent Mosha, amedai kuwa Farihani Maluni kabla ya kuuawa na kufukiwa, alifungwa kamba ya katani mikononi na plasta kichwani.

Amedai kuwa haikuwa rahisi kujua chanzo cha kifo cha Maluni lakini kutokana na uwapo wa plasta eneo la fuvu, alihisi aliuawa kwa kuzibwa mdomo na kusababisha akose pumzi.

Dk. Mosha alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Joyce Minde wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakati akitoa ushahidi katika kesi ya mauaji inayomkabili Hemed Ally.

Alidai kuwa Februari 9, 2015 akiwa katika eneo lake la kazi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, alipelekewa taarifa na Ofisa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa (RCO) wa Ilala, ikimtaka kwenda Sharif Shamba ndani ya Wilaya ya Ilala kuchunguza mwili wa binadamu unaohisiwa kufunikwa ndani ya ua wa nyumba.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Salome Asey, Dk. Mosha alidai alichukua vifaa vyote vya kazi na kuongozana na askari polisi hadi eneo la tukio.

Walipofika eneo hilo majira ya saa sita kasoro mchana, Dk. Mosha alidai kuwa alikuta vijana wakiwa wameishaanza kufukua eneo hilo na ndani ya shimo walikuta matofali mapya, mabaki ya mwili yaliyokuwa yamezungushiwa ndani ya godoro, huku mikono ikionekana kufungwa kwa katani na fuvu likiwa na plasta.

Shahidi huyo alidai baada ya mabaki ya mwili huo kuonekana, wananchi waliokuwapo katika eneo hilo walikumbwa na taharuki wakitaka kumpiga mtuhumiwa aliyekuwapo pale na kumfanya ashindwe kufanya uchunguzi, ikabidi wachukue mabaki na nguo hadi Muhimbili.

Alidai Februari 10, 2015 alifanya uchunguzi akiwa na askari pamoja na ndugu wa marehemu waliotambua mavazi ya marehemu ikiwamo fulana ya pinki.

## HABARI KITAIFA

# Waziri Chana aeleza siri ongezeko watalii

**Na Elizabeth John,**

NJOMBE

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, amesema idadi ya watalii imeongezeka kutoka 450,000 mwaka 2020/21 hadi 700,000 kwa kipindi cha Januari hadi Julai, mwaka huu.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa mkakati wa kutangaza utalii kusini mwa Tanzania uliofanyika mkoani hapo, alisema mafanikio ya The Royal Tour yamesaidia watalii kumiminika nchini.

Waziri huyo alisema licha ya sekta ya utalii kuchangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa nchi, mchango huo hauakisi utajiri wa rasilimali za utalii zilizoko.

Alisema kikwazo cha ukuaji wa utalii kusini mwa Tanzania ni watalii wengi kupenda zaidi kutembelea vivutio vilivyoko kaskazini vikiwamo Hifadhi za Taifa Mlima Kilimanjaro, Serengeti, Ziwa Manyara na Mamlaka ya Hifadhi Eneo la Ngorongoro (NCAA).

Chana alisema hali hiyo inasababisha siku za watalii ambao wanakuja nchini kukaa kuendelea kuwa chache na watalii kutojirudia.

Alisema katika kufungua utalii kwenye vivutio vya nchi mwaka 2017, serikali ilianzisha mradi wa kuboresha usimamizi wa maliasili na kukuza utalii kusini mwa Tanzania kwa lengo la kupanua wigo wa mazao ya utalii kijiografia.

"Mradi huo unatekelezwa kupitia fedha za mkopo wa masharti nafuu wa dola za Marekani milioni 150 kutoka Benki ya Dunia," alisema.

Kwa mujibu wa waziri, katika kufanikisha azma ya kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko mikoa ya kusini, wizara kupitia Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), imeendaa mikakati mahususi ya kutangaza vivutio vya utalii.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mtendaji TTB, Felix John, alisema utalii ni moja ya sekta za vipaumbele nchini na Rais Samia Suluhu Hassan amejitoa kupitia programu maalum ya Tanzania Royal Tour, ili kuitangaza na kuifungua nchi katika sekta ya utalii.

Alisema bodi hiyo imejipanga kufungua utalii Nyanda za Juu Kusini kwa kuleta watalii kwenye vivutio vilivyoko katika mikoa hiyo.

"Kama mnavyofahamu viko vivutio vingi katika ukanda huu wa kusini tunayo Kitulo, Mpanga Kipengele na eneo la kihistoria la Nyumbanitu," alisema John.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema Tanzania ina hifadhi nyingi na zinafanana lakini upekee ulioko kwa mkoa wa Njombe ni Hifadhi ya Taifa Kitulo ambayo ni maalum kwa uhifadhi wa maua.

"Kwa maana kama shughuli inafanyika Dar es Salaam haya maua inabidi waagize kutoka sehemu nyingine lakini kama ni Njombe yanapatikana hapa hapa," alisema Mtaka.

Alisema watu wengi hawafahamu kuwa hata biashara ya maua inayofanyika mkoa wa Kilimanjaro Wilaya ya Moshi na Arusha ilianzia mkoani Njombe.

Mtaka alisema biashara hiyo haikufanyika mkoani Njombe kutokana na kukosekana kwa miundombinu ya uwanja wa ndege.




Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili Baraza la Habari Tanzania (MCT), Jaji Robert Makaraba, akifungua mkutano jijini Dar es Salaam jana kuhusu matokeo ya ufuatiliaji wa kesi zilizomalizika za vyombo vya habari, uhuru wa vyombo vya habari na kujieleza, ulioandaliwa na MCT. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Upelelezi kesi ya Ole Sabaya ngoma mbichi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

UPANDE wa utetezi katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai ole Sabaya, umeiomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi kuielekeza Jamuhuri kubadili hati ya mashtaka dhidi ya mteja wao.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi Salome Mshasha, Wakili wa Utetezi, Hellen Mahuna, aliomba busara ya mahakama kuikumbusha Jamhuri kuhusu ahadi ya kubadili hati hiyo.

"Ni rai yetu kwamba mahakama yako iukumbushe upande wa Jamhuri kubadili hati ya mashtaka kama wakivyoahidi wakati uliopita, lakini upelelezi nao ukamilike," alidai.

Awali Wakili wa Jamhuri, Susan Kimaro, akiambatana na Wakili Sabitina Mcharo, aliiomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa kesi hiyo kwa kuwa upelelezi bado haujakamilika.

"Niiombe mahakama yako ipange tarehe nyingine ya kutajwa kwa kesi hii kwani bado upelelezi haujakamilika. Lakini bado hatujapata kibali cha mahakama hii kusikiliza shauri hili," alisema.

Akijibu maombi ya upande wa utetezi, Wakili Mshasha aliomba upande wa Jamhuri kupewa muda zaidi ili kukamilisha upelelezi na kubadili hati ya mashtaka dhidi ya Sabaya.

Baada ya hoja hizo, Hakimu Mshasha aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 10, mwaka huu, na Sabaya ataendelea kuwa chini ya uangalizi wa Magereza kutokana na kesi yake kutokuwa na dhamana.

Sabaya alipanda kizimbani kwa mara ya pili akiwa peke yake baada ya washtakiwa wenzake wanne kukiri kosa na kutiwa hatiani Septemba 6, mwaka huu.

Washtakiwa hao walilipa faini ya Sh. 50,000 kila mmoja pamoja na fidia ya Sh. milioni moja kila mmoja kwa mfanyabiashara Godbless Swai.


MEDIA COUNCIL OF TANZANIA

## EXCITING EMPLOYMENT OPPORTUNITY

**Background**
The Media Council of Tanzania (MCT) is an independent, voluntary, self-regulatory body with the objective of promoting freedom of the media and ensuring the highest professional standards and media accountability in the United Republic of Tanzania.

MCT implements its programmes with the aim of expanding the perimeters of freedom of expression and of the media as well as promoting professionalism and accountability in order to ensure that the Tanzanian media contributes effectively to the country's development and democratic processes.

MCT's incumbent head of secretariat, the Executive Secretary, will be retiring soon and the Council would like to recruit a competent Tanzanian to fill that position.

**Overall Responsibility:**
As chief executive officer of the organisation, reporting to the President of MCT and Chairman of the Board, the Executive Secretary shall be answerable and accountable to the Governing Board of MCT in terms of the Constitution of the MCT, any regulations made thereunder and directives issued by the said Board through its President. He/she is responsible for financial sustainability, resource mobilization, financial accountability, programing and administration of MCT as well as being accountable for ensuring quality assurance and control of the overall Council outputs and results.

**Duties and responsibilities of the employee:**

a) To run all the affairs of the Council with utmost efficiency, honesty and integrity and in the best interest of the organization and the media profession;
b) To ensure that the reputation, name and public image of the Council are not compromised by his/her word or conduct or that of his/her subordinates;
c) To ensure maintenance of up to date records of the Council, the Governing Board and its various committees and ensure that the financial accounts of the Council are maintained to the standard required and audited annually;
d) To oversee efficient and effective implementation of decisions and directives of the National General Convention (NGC), Governing Board and its committees and the Board of Trustees;
e) To oversee the development, implementation and review of the MCT plans for effective utilization of resources and report to the Governing Board for notification or approval as the case may be;
f) To raise funds for the Council operations without compromising its basic principles and independence;
g) To mobilize resources for the smooth running of the Secretariat;
h) To prepare budgets and policy proposals for the deliberation and/ or approval of relevant statutory bodies;
i) To develop and maintain good relations with members of MCT, other professional organizations and the media industry generally;
j) To develop and maintain effective networks with national, regional and international partners;
k) To promote establishment of independent media councils in Africa;
l) To organize, service and attend National General Conventions, Governing Board, Committee and Board of Trustees meetings;
m) To develop, promote and uphold professional ethical standards in media;
n) To oversee review, investigation and resolution of complaints brought before the Council;
o) To organise and or assist in the organization of such other activities as may promote the objectives of the Council;
p) To oversee the production, and provide leadership, assistance and guidance to the editors and other functionaries of the regular publications of the Council;
q) To assume such other duties as may be assigned from time to time by the Governing Board and its Committees within the mandate of the Council; and
r) To do all other things consequential upon, and incidental to the carrying out of his main duties.

***Key Qualifications and Experience:***

**Education:**
- Master's degree in Journalism, Mass Communication, Social Sciences or MBA or its equivalent.

**Experience:**
- 5 years or more in managing related activities or NGO/CSO.

**Competencies:**
- Resource mobilization and fundraising
- Interpersonal skills / public relations and communication
- Coordination, supervision, management with bias towards participatory styles of management and collective decision-making
- Team building
- Computer literacy in relevant packages
- Knowledge of Tanzanian media landscape
- Gender awareness and capacity to mobilize media towards the same.

**MODE OF APPLICATION**
To apply, submit a detailed Curriculum Vitae (CV) with email address, telephone number, copies of relevant certified certificates/testimonials, and names of three professional referees. Applicants are also required to submit application letter explaining why they should be considered for the job through the address below:

**Executive Secretary,**
**Media Council of Tanzania,**
**PO Box 10160,**
**Dar es Salaam.**

Please send your application through post or **recruitment@mct.or.tz**

**Closing date is November 15, 2022.**

MCT is an equal opportunity employer. People with disabilities, women, youth and any other groups are encouraged to apply. Only shortlisted candidates will be contacted.

217062901

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# NEMC inapaswa kubadilika katika utendaji kazi wake

**BARAZA** la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limepewa dhamana kubwa katika kuhakikisha suala la mazingira nchini linasimamiwa ipasavyo ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua dhidi ya watu, vikundi na taasisi zinazokiuka sheria zinazohusu mazingira.

Miongoni mwa shughuli muhimu za baraza hilo ni kutoa adhabu pamoja na kuwafikisha katika vyombo vya sheria watu wote na taasisi zinazovunja sheria, kanuni na taratibu kuhusu mazingira.

Kutokana na kupewa nguvu hizo kisheria, katika miaka ya karibuni jamii ilishuhudia viongozi wa NEMC, pamoja na mawaziri wenye dhamana ya masuala ya mazingira wakichukua hatua dhidi ya wakiukaji wa sheria ikiwamo kufunga baadhi ya viwanda vinavyochafua mazingira. Pia baraza hilo limekuwa likitoa matamko na maonyo mbalimbali dhidi ya wakiukaji wa sheria za mazingira.

Pamoja na kutekeleza majukumu hayo, hivi karibuni kumekuwa na malalamiko dhidi ya NEMC kuwa haitekelezi makujumu yake ipasavyo kubwa zaidi ikiwa ni ucheleweshaji wa vibali kuhusu tathmini na athari za mazingira. Vibali hivyo ndivyo vinavyotoa mwanga kwa wawekezaji na taasisi za serikali na za binafsi kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa barabara, viwanda na masoko.

Mbali na ucheleweshaji wa vibali, NEMC pia imekuwa ikilalamikiwa kwa kutokuchukua hatua dhidi ya kampuni zinazojenga vituo vya mafuta karibu na makazi ya watu, jambo ambalo linadhaniwa kuwa kuna ukakasi katika kuruhusu utekelezaji wa kazi hizo.

Kadhalika, NEMC imekuwa ikilalamikiwa kushindwa kuwachukulia hatua wamiliki wa nyumba za starehe na ibada kutokana na kelele zinazotokana na muziki, hivyo kusababisha usumbufu kwa watu wanaoishi karibu na maeneo hayo.

Mifano halisi juu ya malalamiko hayo, kwanza ni kutoka mkoani Manyara ambako NEMC imelalamikiwa kwa urasimu wa upatikanaji vibali kwa wawekezaji wenye nia ya kuweka vitegauchumi mkoani humo. Mfano wa pili ni katika Manispaa ya Songea ambako baraza hilo lililalamikiwa kuchelewesha vibali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kutokana na urasimu huo, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, amesema unakwamisha mkoa kupata wawekezaji hasa wa viwanda. Jambo la kushangaza zaidi ni kwamba kwa mujibu wa Nyerere, kutokana na ucheleweshaji huo, mtu anaweza kukaa hata miaka miwili bila kupata kibali tangu alipowasilisha maombi katika ofisi za baraza hilo.


Athari za ucheleweshaji huo ni kubwa kwa kuwa miradi yoyote ile inatoa fursa za upatikanaji wa ajira hasa kwa vijana ambalo ni tatizo kubwa hivi sasa. Sambamba na kukosekana kwa ajira, urasimu huo pia, unasababisha kudumaa kwa pato la taifa na uchumi wa wananchi.

Mwakilishi huyo wa Rais katika mkoa alishangazwa na hatua hiyo hata kuhoji labda NEMC ina kazi nyingi kiasi cha kushindwa kutoa vibali kwa wakati licha ya kuwa waombaji wanakuwa tayari wameshalipa ada mbalimbali kwa ajili ya upatikanaji wa hati hizo ambazo zinatoa mwanya kwa wawekezaji kuanza kutekeleza miradi yao.

Wahenga wanasema ngoma ikivuma sana mwishowe hupasuka. Kwa mantiki hiyo, NEMC inapaswa kuanzia sasa kujitafakari juu ya malalamiko na lawama inazotupiwa na kuchukua hatua ili kubadilika kiutendaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com





Na Golden Kisapile, TUDARCo

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mitandao itumiwe kujenga si kwa uovu

**MITANDAO** ya kijamii ikitumika vizuri inaweza ikawa fursa na maendeleo badala ya kugeuzwa kuwa chaka la uovu kama ilivyoanza kuonekana.

Ikumbukwe kwamba Septemba 12, mwaka huu, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alitoa onyo kali kwa wanaosambaza maudhui yanayohamasisha kutoka nje ya mstari. Ni masuala kama mapenzi ya jinsia moja kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari, akiwataka kuacha mambo hayo yasiyo na tija kwa taifa.

Anasema, "Tutawazoa watu kwa kutafuta mnyororo wote waliohusika katika usambazaji pamoja na 'maadmin' wa makundi hayo itakuwa mfano na kujua serikali ipo."

Mitandao ya kijamii kama vile WhatsApp, Facebook, Twitter na Instagramu inaweza kutumiwa kwa namna nyingi ili kuongeza tija au manufaa mbalimbali kwa vijana na wazee hata Mtanzania mwenye rika lolote ili aondokane na umaskini au kupanda ngazi zaidi kimaisha.

Ni jukwaa la kutangaza biashara mbali mbali kama vile bidhaa za kipekee, mfanyabiashara anazozalisha kama lishe ya asili inayoweza kutibu magonjwa kama sukari.

Lakini kutangaza vifaa, bidhaa na kazi za kibunifu mfano kwenye umeme, mavazi, urembo na mapambo mbalimbali. Na kupitia mitandao hiyo vijana na wajasiriamali wanaweza kuongeza thamani ya biashara na kupata wateja wengi zaidi.

Mitandao ni chanzo cha ajira, kwa watu wengi mfano watengeneza maudhui wameajiriwa na wengine wamejiajiri kwenye mitandao mbalimbali ya kijamii wakaitangaza na kuuza maudhui mbalimbali.

Hii inakuza kipato cha mtu na hata kundi kubwa, ili kupata mahitaji ya msingi kupitia mitandao na kazi hizo, pia vijana wengi wabunifu wametengeneza TV mtandaoni, wana blog, redio na magazeti na huko ndiko kujiajiri na kuajiri wengine.

Mitandao ni chanzo cha habari na taarifa nyingi ambazo wanazihitaji wanafunzi shuleni, vyuoni na kwenye ujasiriamali na uwekezaji mbalimbali hivyo ni maabara na maktaba inayoishi.

> **Kusoma na kujifunza kutoka kwenye vitabu na nyaraka mbalimbali mfano kama vile vitabu vya kiada na ziada, ambavyo vinapatikana katika programu zilizoko mitandaoni ni njia ya kupata elimu kwa ufanisi.**

Yapo mambo ya kitaifa, kimataifa na anga za juu. Kuna masuala ya ugunduzi, teknolojia na kazi za watu mbalimbali ambazo kama ni mwanafunzi akizisoma anajiweka kwenye kufahamu na kuelewa mambo mengi zaidi.

Kufanya biashara za mitandaoni kupitia programu mbalimbali kama vile forex ndiyo habari ya mjini. Kuna mifumo wezeshi ya kifedha ambayo inasaidia kununua bidhaa mbalimbali na kuuza kutoka sehemu na mataifa mengine duniani. Mitandao ni kama soko la kujua namna ya kuuza na kununua siyo uwanja wa masuala machafu.

Kusoma na kujifunza kutoka kwenye vitabu na nyaraka mbalimbali mfano kama vile vitabu vya kiada na ziada, ambavyo vinapatikana katika programu zilizoko mitandaoni ni njia ya kupata elimu kwa ufanisi.

Hivyo, kufanikisha wanafunzi au wanavyuo kupata ujuzi na maarifa mbalimbali kuhusu masomo ya uchumi, kijamii, kisiasa, uhandisi na teknolojia wanayojifunza.

Kufanya mikutano na midahalo mbalimbali, kupitia programu kama vile Whatsap na zoom ni matumizi chanya ya mitandao yote huwasaidia watu kufanya mazungumzo ya ana kwa ana na kupanga mikakati ya maendeleo.

Mijadala mitandaoni inafanikiwa kwa watu kujiunga na kushiriki kwenye mada tofauti zinazojadiliwa kama vile zinazohusu uchumi, siasa, teknolojia, utafiti bila kujali mipaka hata kama mtu yupo nje ya nchi au mbali ya eneo aliko mwenzake mazungumzo hufanyika mtandaoni.

Burudani ni njia bora inayopatikana kwa kuitumia mitandao ya kijamii, hapa watu hupata burudani kwa njia mbalimbali kama vile kupakua na kusikiliza miziki yaweza kuwa ya Bongo Fleva, Injili, kuangalia filamu za ndani na nje ya nchi, hivyo kupitia burudani hizo kijana au yeyote anapunguza msongo wa mawazo.

## Marekani kukipa nguvu kituo umahiri wa barabara cha NIT

**Na Prosper Makene**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), kipo katika mazungumzo na Mamlaka ya Barabara (FHWA) ya Marekani ili kukiwezesha Kituo cha Kikanda cha Umahiri katika Usalama Barabarani (RCoE) kufanya utafiti wa kina kwa lengo la kupunguza ajali za barabarani.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Zacharia Mganilwa alisema mazungumzo yanaendelea vyema na wanategemea kuingia makubaliano hayo wiki chache zijazo.

"Ushirikiano wetu na Mamlaka ya Barabara (FHWA) ya Marekani utasaidia kwa kiasi kikubwa kituo chetu kuongeza ubora hasa kwenye eneo la utafiti na mafunzo.

"Nchi ya Marekani iko very advanced (imepiga hatua) kwenye eneo la usalama wa barabara duniani, hivyo ushirikiano wetu utakuwa wenye tija kwa kuwa tutafundishwa teknolojia mbalimbali za usalama wa barabara," alisema.

Mkuu wa Chuo alisema, wataalamu kutoka Marekani watakuja kuwafundisha wahadhiri chuoni hapa, ambao watatoa mafunzo hayo kwa wakufunzi mbalimbali katika ukanda wa Afrika Mashariki.

"Baada ya wahadhiri wetu kupewa mafunzo hayo, nchi zote zilizopo katika ukanda huu wa Afrika Mashariki zitanufaika kupitia Kituo chetu cha Kikanda cha Umahiri katika Usalama Barabarani (RCoE)," alisema.

Prof Mganilwa alisisitiza: "Lengo kuu la kituo chetu ni kutoa mafunzo, utafiti na huduma za ushauri zinazohusu usalama barabarani. Kwa hiyo, ushirikiano huo utakiwezesha kituo kuwa mahiri katika maeneo yote ya utafiti na ufundishaji wa madereva nchini na kwenye eneo la ukanda wote wa Afrika Mashariki."

Alisema, ni utafiti tu unaoweza kutoa majawabu ya moja kwa moja na kupunguza ajali za barabarani na siyo njia nyingine yoyote.



Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza (wa pili kulia), akizungumza jana katika kikao kilichoitishwa na Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi Kata ya Makumbusho Dar es Salaam, Mwita Julius (wa tatu kulia), kujadili mbinu za kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia, baada ya mtu mmoja kukamatwa kwa tuhuma za kurubuni wanafunzi kwa rushwa ya ngono. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wawekezaji, wafanyabiashara India waonyesha nia kuwekeza

**Na Romana Mallya**

WAWEKEZAJI na wafanyabiashara wa sekta ya kilimo kutoka India wameonyesha nia ya kuwekeza katika uzalishaji wa zana za kilimo, utunzaji na uhifadhi wa mazao hapa nchini.

Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, Anthony Mavunde, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika hafla iliyokutanisha wafanyabiashara na wadau mbalimbali waliopo katika sekta ya kilimo, Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), ikiwamo wafanyabiashara hao ili kujadili mwonekano wa sekta ya kilimo kati ya Tanzania na India.

Halfa hiyo ambayo iliandaliwa na Ubalozi wa India nchini kwa kushirikiana TPSF, ilitanguliwa na maonyesho ya kimataifa ya biashara ya bidhaa za chakula, vifungashio, uchapaji, bidhaa za plastiki, uhandisi na zana za kilimo yaliyofanyika kwa siku tatu kuanzia Septemba 22, mwaka huu, na kukutanisha kampuni 90 za wawekezaji za India ambao baadhi wameonyesha nia ya kuwekeza Tanzania.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mavunde alisema wafanyabiashara hao wameonyesha nia ya kuwekeza katika uzalishaji wa zana za kilimo na utunzaji wa mazao.

Alisema mkutano huo ni muhimu kwa sababu kwa sasa kilimo ni kati ya vipaumbele vikubwa vya serikali ambapo kwa mwaka huu wa fedha 2022/23, serikali imetenga bajeti kubwa katika sekta ya kilimo hasa kilimo cha umwagiliaji.

"Tumezungumza nao na mwitikio ni mzuri na wameonyesha nia ya kuja kuwekeza katika uzalishaji wa zana za kilimo hasa katika teknolojia bora ya kilimo, utunzaji na uhifadhi wa mazao," alisema.

Kiongozi huyo aliwaeleza wawekezaji hao kuwa serikali ina nia ya dhati katika sekta ya kilimo ambapo mwaka huu wa fedha, Rais Samia Suluhu Hassan, ameongeza bajeti yake kutoka Sh. bilioni 294 hadi Sh. bilioni 954, ambapo fedha nyingi zimeelekezwa katika ujenzi wa miundombinu na skimu za umwagiliaji.

"Kiasi kikubwa cha fedha kimetengwa kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji sambamba na kufanya upembuzi yakinifu ya kina katika mabonde makubwa yaliyopo lengo ni Tanzania inafanya kilimo cha umwagiliaji, katika mwaka huu wa fedha serikali itayapitia mabonde makubwa 22, tunategemea kuwa na miradi mikubwa ya umwagiliaji kuanzia mwaka wa fedha unaokuja," alisema.

Mavunde alisema katika mwaka huu wa fedha, mabwawa makubwa 12 yatajengwa ambayo yatakuwa na uwezo wa mita za ujazo zaidi ya milioni 131.

Pia alisema fedha nyingi zimeelekezwa katika uzalishaji wa mbegu ili nchi ijitosheleze katika eneo hilo, ndiyo maana bajeti imepanda kutoka Sh. bilioni 10 hadi Sh. bilioni 43.

Kadhalika, alisema bajeti hii imelenga kukuza na kuviendeleza vituo vya utafiti, ambapo vilivyopo ni 17 na lengo lake ni kuwajengea uwezo wataalamu ili waje na mbinu mbalimbali za kumfanya mkulima alime kwa tija ikiwamo ugunduzi wa mbegu.

Mkurugenzi wa Sera na Huduma kwa Wanachama TPSF, Zachy Mbenna, alisema mkutano huo umehusisha wadau sekta ya kilimo kutoka Tanzania na India na kwamba ni sehemu ya kilele cha maonyesho na mikutano ya kibiashara iliyofanyika katika ya nchi hizo mbili ikihusisha kampuni zinazojikita katika kilimo hasa uzalishaji wa pembejeo za kilimo, mashine na vitendea kazi.

"Tunazishukuru serikali za nchi hizi mbili Tanzania na India pamoja na Ubalozi wa India ambao umeratibu hili kwa kushirikiana na TPSF. Maeneo ambayo wadau wa sekta ya kilimo tunaweza kunufaika ni mengi, kilimo chetu kinapitia maboresho na mapinduzi ya kilimo ambayo ni sehemu ya mkakati wa nchi kuboresha kilimo ambapo kama alivyosema Mheshimiwa Mavunde tunahitaji kukua kutoa asilimia nne hadi asilimia 10 mwaka 2030.

## KABWELA



WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA
TFS
MISITU NI MALI

## SIKU YA UTALII DUNIANI

WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA
TFS
MISITU NI MALI

# TFS na fikra mpya kuhusu utalii nchini

**Na Mwandishi Wetu**

Kila mwaka kuanzia 1980 dunia imekuwa ikiadhimisha siku ya utalii huku kukiwa na kaulimbiu kwa kila mwaka.

Mwaka huu kauli mbiu ya siku hii muhimu ni "Rethinking tourism" kwa tafsiri isiyo rasmi ni "fikra mpya kuhusu utalii".

Itakumbukwa sekta ya utalii miaka michache iliyopita iliathirika sana na janga la Uviko -19 hivyo kauli mbiu ya mwaka huu inatukumbusha na kutuhamasisha wote kuwa tuwaze tena kuhusu utalii na kusimamisha upya sekta hii muhimu kwa maendeleo ya nchi na dunia kwa ujumla.

Kamishna wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dos Santos amefanya mazungumzo na gazeti hili na haya ni baadhi ya mambo aliyoyabainisha:-

**Ni ipi nafasi ya TFS katika kuchochea ukuaji wa sekta ya utalii?**

TFS inasimamia jumla ya misitu takriban 463, kati yake misitu ya Hifadhi za Mazingira Asilia 20, mashamba ya Miti 8, misitu ya Hifadhi 4, Misitu ya mikoko kwenye mwambao wa Bahari ya Hindi na Hifadhi 6 za Malikale ni baadhi ya maeneo machache ambayo utalii unafanyika.

Misitu hii pamoja na Hifadhi za Malikale ni kichocheo cha zao jipya la utalii katika nchi yetu ambayo ni utalii ikolojia pamoja na utalii wa urithi wa utamaduni.

Aina hii ya utalii ikolojia tofauti na utalii uliozoeleka na wengi, ni aina ya utalii ambayo kwa sehemu kubwa hufanyika kwenye misitu iliyofunga na yenye utulivu mkubwa na nguzo zake kuu ni hasa kutunza mazingira na huduma zitokanazo na mazingira, utalii usio na athari kwa mazingira, na pia utalii wenye kujali na kutunza halimaisha za jamii zilizopakana na maeneo ya utalii.

Aina hii ya utalii ni mojawapo ya mkakati wa kuongeza mchango wa sekta ya misitu kwenye ukuaji wa pato ghafi la nchi (GDP) lakini pia katika kuchangia kukuza idadi ya watalii kufikia milioni 5 kwa mwaka na mapato ya shilingi bilioni 6 kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya chama cha Mapinduzi (CCM), Mpango wa Taifa wa Maendeleo 2025, miongozo na sera za Serikali kwa kubuni na kuongeza mazao mapya ya utalii ikiwemo utalii wa misitu (Utalii Ikolojia).

**Nini ambacho TFS imeshakifanya tofauti katika kukuza utalii wa ikolojia?**

Kwa hapa nchini, dhana ya utalii ikolojia ilianza kusikika katikati ya mwanzoni mwa miaka ya 2010 na ilianza na misitu michache takriban saba huku idadi ya wageni ikiwa takriban 500 kwa mwaka.

Hata hivyo, katika kukuza wigo wa mazao ya utalii ikolojia wakala uliendelea kubuni maeneo mapya ya utalii ikiwa ni pamoja na kupandisha hadhi baadhi ya misitu iliyokuwa na hadhi ya Misitu ya Hifadhi kwenda kwenye hadhi ya Hifadhi za Mazingira Asilia ambayo ni hadhi ya juu zaidi ya uhifadhi kwa mujibu wa shirika la IUCN na hivyo kufikia idadi ya Hifadhi za Mazingira Asilia 20 mwaka 2020.

Haikuishia hapo, bado wakala umeendelea kuyatambua maeneo mengine ya vivutio vya utalii kwenye mashamba ya miti na misitu mingine inayosimamiwa na wakala na hivyo kufanya idadi ya maeneo ya utalii kuwa zaidi ya 30 kwa sasa na bado jitihada zinaendelea kuyatambua maeneo mengine mengi yenye vivutio vya utalii.

Pamoja na jitihada zinazoendelea kutambua maeneo mapya ya vivutio, wakala umeendelea kuboresha miundombinu ya utalii katika maeneo ya vivutio ikiwa ni pamoja na kujenga kwa kiwango cha kupitika kwa barabara zinazoenda kwenye maeneo ya utalii, njia za watembea kwa miguu ndani ya hifadhi, huduma za maliwato, sehemu za kupumzika, huduma za malazi na chakula kwa baadhi ya hifadhi na malango ya kuingia na kutoka ndani ya hifadhi.

Aidha, wakala unaendelea na jitihada za kutangaza utalii ikolojia na kutoa elimu kwa umma kupitia njia mbalimbali za redio, TV, kushiriki maonesho ya ndani na nje, kutumia mitandao ya kijamii na watu mashuhuri na kuandaa safari za kuhamasisha utalii hasa wakati wa maonesho ya ndani mfano 77 na 88.

Pia, TFS imeweka viwango vya chini kabisa vya kiingilio na shughuli zinazofanyika kwenye utalii ili kuchochea na kuhamasisha wageni wengi zaidi wa ndani na hata nje ya nchi kutembelea vivutio vya utalii ikolojia.

**Nini hatma ya ushirikiano wa TFS na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) katika kukuza utalii?**

Serikali imeandaa kanuni za uwekezaji kwenye misitu kupitia Tangazo la Serikali namba 85 la mwaka 2020 ambapo wawekezaji kutoka taasisi binafsi na mtu mmoja mmoja wanaruhusiwa sasa kuwekeza kwenye Hifadhi za Misitu na kuendesha shughuli za malazi na chakula.

Aidha, Serikali kupitia GN 59 imeruhusu uwekezaji kwenye misitu kwa huduma za burudani na michezo na shughuli zote zenye mrengo wa burudani ili kuongeza mazao ya utalii na muda wa wageni kukaa kwenye hifadhi na hatimaye mapato ya Serikali.

TFS inashirikiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ambacho ni lango la wawekezaji na kuainisha maeneo ya uwekezaji kwenye misitu kwa ajili ya huduma za utalii ikiwemo ujenzi wa hoteli za kitalii na huduma za malazi na chakula ili TIC iweze kuwapatia wawekezaji wanaotafuta fursa za uwekezaji kwenye sekta ya utalii.

**Vivutio gani ambavyo mtalii anaweza kukutana nayo katika utalii wa ikolojia?**

Kila hifadhi au msitu una aina tofauti za vivutio vyake kuanzia maporomoko ya maji, mabwawa ya kuogelea, mimea, wanyama, milima, ndege, vyura, panzi, vinyonga, mandhari na vivutio vya urithi wa utamaduni.

Baadhi ya vivutio vya utalii kwa kutaja vichache ni pamoja na Maporomoko ya Kalambo ambayo ni ya pili kwa urefu Afrika yakiwa na urefu wa mita 235, Ziwa Ngosi ambalo lina muonekano wa ramani ya bara la Afrika nalo likiwa la pili kwa ukubwa Afrika kwa maziwa yatokanayo na volcano, Msitu wa Pugu ambao unasimama kama mapafu ya jiji la Dar es Salaam, Misitu ya Milima ya Tao la Masharíki mfano Amani, Magamba, Uluguru, Nilo, Chome na Mkingu ambayo inatambulika duniani kama maeneo ndwele kwa misitu ya bioanuai za wanyama na mimea na pia maeneo mahsusi kwa ajili ya utalii wa ndege.

Pia mlima Rungwe wenye mita 2,981 ambao ni kilele kirefu katika nyanda za juu kusini mwa Tanzania, na Mlima Hanang ambao ni wa nne kwa urefu nchini ukiwa na urefu wa mita 3,423 kutoka usawa wa bahari. Milima hii hutumika kama sehemu ya mazoezi na kujiandaa kupanda Milima mirefu zaidi nchini.

Vilevile, maeneo ya urithi wa utamaduni ikiwemo eneo la Mjimkongwe Bagamoyo, Magofu ya Kaole na michoro ya miambani katika eneo la Kondoa Irangi ni mojawapo ya maeneo ya utalii yenye vivutio na historia ya kale na urithi wa utamaduni.

Kama yalivyo maeneo mengine, taratibu ni za kawaida ambapo mgeni akitembelea eneo husika analipa kiingilio na malipo mengine kadri ya huduma atakazohitaji katika eneo husika.

Viwango vya malipo vimeainishwa katika Gazeti la Serikali na vinatofautiana kulingana na umri wa mgeni, uraia na shughuli anazofanya atakapokuwepo ndani ya hifadhi.

**Utalii wa ikolojia unakabiliana na changamoto gani?**

Maeneo ya utalii wa misitu baadhi yapo kwenye milima na maeneo ambayo yana changamoto ya kufikika kwa urahisi, hivyo yanahitaji maboresho ya mara kwa mara ya barabara na huduma zingine za muhimu mfano maji na umeme.

Rasilimali misitu kwa ajili ya utalii ikolojia ni tete (delicate) hivyo inahitaji umakini katika kusimamia uendelezaji wa utalii na miundombinu ili kutokuathiri uasili wa mazingira.


Hili ni zao jipya na aina ya soko lake kimataifa linatofautiana na utalii uliozoeleka, hivyo jitihada za ziada zinatakiwa ili kuwa na mikakati ya kulifikia soko hilo.

**Fursa zilizopo katika utalii wa ikolojia ni zipi?**

Zipo fursa nyingi hasa kwa upande wa wadau wanaofanya biashara ya utalii kwani wanaweza kuwaongezea wageni wao kwenye package yao aina hii ya utalii.

Vilevile, wananchi waishio jirani na Hifadhi hizi wanaweza kupata fursa za kuongoza watalii, kuuza utamaduni wao na vyakula na kuwahudumia wageni kwa ukarimu ili kuongeza mnyororo wa thamani kwenye utalii.

Pia, sekta hii kwa sasa inakua kwa kasi na hivyo mahitaji ya wageni nayo yanaongezeka ikiwa ni pamoja na kuhitaji huduma za chakula na malazi, hivyo hii inatoa fursa kwa wawekezaji na ili kuona jinsi ya kuchangamkia fursa za kuwekeza katika hoteli za kitalii kwani maeneo ya kuwekeza tayari yamekwisha ainishwa kwa kila hifadhi.



*Watalii wakipiga Makasia kwenye Bwawa, huu ni moja wapo ya utalii wa Ikolojia*



*Mahema madogo ya watalii ndani ya Msitu*

## Vitongoji viwili Bagamoyo kupatiwa majisafi Desemba

**Na Joseph Mwendapole**

WAKAZI wa vitongoji vya Nyakahamba na Kitonga, Kata ya Kerege wilayani Bagamoyo mkoani Pwani wamehakikishiwa huduma ya maji ifikapo Desemba mwaka huu.

Wananchi hao watapata maji kupitia mradi mkubwa wa uboreshaji huduma ya maji kutoka Bagamoyo hadi Makongo ulio ukingoni kukamilika.

Ahadi hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki Meneja wa Mkoa wa Huduma wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA) Mapinga, Abraham Mwanyamaki.

Akizungumza katika kikao na wananchi wa vitongoji hivyo viwili, Mwanyamaki aliwaondoa hofu wananchi hao na kuwahakikishia kuwa huduma inaenda kuboreshwa na wananchi watarajie huduma ya maji ya uhakika.

"Niwape pole wananchi wa maeneo haya mawili kwamba mamlaka inaelewa changamoto ya kukosa huduma ya maji ya uhakika, tunaahidi ndani ya miezi miwili ijayo kuanzia sasa huduma itakuwa bora," alisema.

Alibainisha kuwa mradi huo mkubwa utamaliza shida iliyopo katika upatikanaji wa majisafi kwa kuwa uko mbioni kukamilika na ndiyo utaleta ufumbuzi wa kudumu katika vitongoji hivi viwili.

Mwanyamaki alisema Kata ya Kerege huduma ya majisafi ni nzuri isipokuwa katika vitongoji hivyo na katika maeneo mengine ndani ya kata uboreshaji wa miundombinu unaendelea.

"Kwa kipindi hiki tunaposubiri kukamilika kwa mradi, mamlaka inaendelea kufanya juhudi nyingine ikiwamo kuboresha miundombinu chakavu ya maji ili wananchi waendelee kupata huduma ya majisafi," alisema Mwanyamaki.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Bagamoyo, Mohamedi Usinga, aliwaomba DAWASA kusimamia mradi kwa karibu zaidi ili ukamilike haraka na kuwapunguzia wananchi kero ya maji.

Diwani wa Kerege, Ngatiruka Said Abdalah, aliwataka wananchi wa vitongoji hivyo viwili kuwa na subira na kuamini serikali kwamba itawaondolea changamoto ya maji.

Mradi wa uboreshaji huduma ya maji kutoka Makongo hadi Bagamoyo unalenga kuboresha upatikanaji wa huduma kwa wakazi takribani 450,000 ambao umehusisha ujenzi wa matangi matatu yaliyopo Vikawe, Mbweni na Tegeta A yenye ujazo wa lita milioni tano kila moja na yatahudumia wakazi wa maeneo ya Mapinga, Mabwepande, Bunju, Mbweni, Wazo, Tegeta A, Madale, Goba na Makongo.

# Wachimbaji wadogo wataka maji, umeme

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

WACHIMBAJI wadogo wanaoshiriki maonyesho ya teknolojia ya madini mkoani Geita, wamelalamikia ukosefu wa huduma za umeme, maji na miundombinu ya barabara katika maeneo mbalimbali ya mchimbo ya dhahabu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wachimbaji hao wamedai kuwa kutokana na kukosekana kwa huduma hizo katika maeneo ya uchimbaji kumesababisha kutumia gharama kubwa kuendesha shughuli hizo.

Mkurugenzi wa kampuni ya utafiti na uchimbaji wa madini ya Geita Resources Limited, John Luhende, alisema kukosekana kwa huduma hizo kunawafanya watumie gharama kubwa kununua mafuta kwa ajili ya kuendesha mitambo ya kusaga mawe (makarasha) na kuvuta maji.

Alisema kwa siku hutumia zaidi ya lita 500 za mafuta ya dizeli kuendeshea mitambo hiyo na hivyo kuiomba serikali kusaidia kuwasogezea huduma za nishati ya umeme na maji katika maeneo ya machimbo.

"Kwa mfano, Mgodi wa Nyakamatagata tunalipa kodi kubwa kwa serikali, lakini hakuna huduma ya maji, umeme na barabara.

"Kuna mtu amejenga daraja linalounganisha Nyakabale na Nyamatagata, kila siku tunalipa Sh. 5,000 wenye magari na hili daraja siyo imara kwa magari ya mizigo.

"Inapotokea maeneo kama hayo tunaomba serikali iwe inaona kama jambo la dharura kwa sababu maeneo hayo yanatoa kodi nyingi kwa serikali," aliwasilisha kero zao.

Akizungumzia maonyesho hayo ya tano, Luhende alisema yamekuwa mwanga kwao kwa kuwa huwasaidia kuwakutanisha na wafanyabiashara wakubwa wakiwamo wauzaji wa mitambo na taasisi za kifedha.

Meneja wa Geita Resource Limited, Masanja Michael, alisema maonyesho hayo yamewasaidia kuondokana na matumizi ya zana duni na imani za kishirikina katika utafutaji wa madini.

Aliongeza kuwa kwa sasa wanatumia vipimo vya kisasa katika uchimbaji na uchakataji wa madini hayo.

Mmoja wa wachimbaji katika Mgodi wa Nyamatagata, Anael Thomas alisema maonyesho hayo ambayo hufanyika kila mwaka yamesaidia kuuweka Mkoa wa Geita kwenye ramani nzuri katika sekta ya madini.

"Kupitia maenyesho haya, Geita inaonekana kwenye sura ya dunia na hivyo kusaidia kupata wawekezaji wa ndani na nje ambao wanahitaji kuja kuwekeza kwenye sekta ya madini, hivyo tunaipongeza serikali kwa hatua hii," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Wadogo wa Madini mkoani Geita (GEREMA), Christopher Kadeo, alisema kabla ya maonyesho hayo ya kila mwaka yaliyoanza mwaka 2018, wachimbaji walikuwa na imani potofu, wakienda kwa waganga wa jadi kupewa walichoamini mbinu za kubaini madini yaliko.

Aliongeza kuwa baada ya kupata elimu kupitia maonyesho hayo, wengi wameachana na imani hizo potofu na badala yake wanatumia teknolojia ya kisasa kwa kupeleka sampuli maabara za kisasa badala ya kuchinja kuku kwa waganga wa jadi.

"Kwa sasa kuku wamesalimika, badala ya kwenda kuchinja kwenye 'maduara' sasa kuku wanaliwa, tumeamini kuwa uchimbaji wa madini siyo kuchinja kuku ni sayansi ambayo inahitaji teknolojia ikiwamo mitambo ya kisasa," alisema Kadeo.

Katibu Tawala Mkoa wa Geita, Prof. Godius Kahyarara, alibainisha kuwa wachimbaji wadogo wa dhahabu mkoani humo huzalisha wastani wa tani 5.8 za dhahabu kwa mwaka.

Alisema matarajio ya mkoa huo ni kuzalisha wastani wa tani 20 kwa mwaka kutokana na elimu ya matumizi ya vifaa vya kisasa kwa wachimbaji inayotolewa kwenye maonyesho hayo.



Shekhe Mkuu wa Jumuiya ya Shia Ithna'ashariyyah Tanzania Maulana, Hemed Jalala (wa tatu kulia aliyeshika kitabu), akiongoza mamia ya waumini wa dini ya Kiislamu dhehebu la Shia Ithna'ashariyyah nchini, katika matembezi ya amani ya kumbukizi ya kifo cha Mtume Muhammad yaliyoanzia Ilala Boma hadi Viwanja vya Pipo, Kigogo jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# NRA yachagua viongozi wapya

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAJUMBE wa mkutano mkuu maalum wa Chama cha National Reconstruction Alliance (NRA) wamemchagua Khamis Faki Mgau kuwa mwenyekiti mpya wa chama hicho katika mkutano ulifanyika mwishoni mwa wiki mkoani Morogoro.

Mkutano huo ulikuwa na ajenda mbili ya kupitisha katiba mpya ya chama hicho pamoja na kufanya uchaguzi mkuu wa viongozi ngazi ya Taifa.

Katika uchaguzi huyo aliyekuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama hicho, Simai Abdallah Abubakar, hakuwania tena nafasi hiyo badala yake aligombea kwenye kinyang'anyiro cha nafasi ya mwenyekiti wa bodi ya chama iliyokuwa na wagombea wanne na kuambulia kura moja, nafasi hiyo ikinyakuliwa na Mohamed Ismail Abood aliyepata kura 96.

Mwenyekiti mpya aliyechanguliwa, kabla ya uchaguzi huo alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama Zanzibar.

Akitangaza matokeo hayo Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya NRA Taifa, Leopold Mahona alisema nafasi ya Mwenyekiti wa Taifa ilikuwa na wagombea wawili ambao ni Mahusin Aboud Ahmed na Mgau.

Katika matokeo ya nafasi hiyo wajumbe wa mkutano mkuu walimchangua Mgau kwa kura 106, wakati Ahmed akiambulia kura moja huku moja ikiharibika.

Kwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Chama cha NRA Zanzibar waligombea wawili; Suleiman Mohamed Abdallah aliyepata kura mbili na Bimkubwa Abdallah Said aliyepigiwa kura 107 na kura moja iliharibika.

Kwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Chama Taifa kwa Tanzania Bara, wagombea walikuwa wawili; Ulotu Mariam Abubakar ambaye hakupata kura hata moja huku Mohamed Majaliwa Mohamed akipata kura 109 na kura moja iliharibika.

Nafasi ya Katibu Mkuu wa Chama hicho mgombea Hassan Kisabya Almas alifanikiwa kutetea nafasi yake kwa kupata kura 104 na kuwashinda wenzake wawili, Nadra Abubakar Muyotu aliyepata kura mbili na Balama Methord Geogre kura tatu.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Taifa la Chama hicho alisema wagombea walikuwa wawili ambao ni Suleiman Juma Hamad aliyepata kura moja na Hamis Fadhili Kiswaga aliyepata kura 109.

Mahona alitaja nafasi nyingine ni Katibu wa Baraza la Wazee Taifa ambapo wagombea walikuwa wawili - Feruz Juma Feruz aliyepata kura nne wakati Sarah Abdallah Mlula alipata kura 106 na hakuna kura iliyoharibika.

Kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu chini ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya NRA kwa kushirikiana na wajumbe wa kamati hiyo, Rashid Nyumba pamoja Shauri Hamis Shauri waliridhia hoja za wajumbe wa mkutano kufanya mabadiliko ya madogo ya katiba.

Mabadiliko hayo yalilenga kukidhi matakwa ya Sheria mpya ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 2019 inayotaka wajumbe wa mkutano mkuu vya vyama kuwa siyo chini ya wajumbe watano na wanawake siyo chini ya wawili.

# Wakulima 3,000 Muheza wasajiliwa kupata mbolea

**Na Steven William,** MUHEZA

WAKULIMA 3,342 wilayani Muheza mkoani Tanga wameingizwa kwenye mfumo wa namba za usajili kwa ajili ya kupata huduma ya mbolea.

Ofisa Kilimo wilayani hapo, Hoyange Mbwambo alibainisha hayo wakati wa mkutano wa wadau wa kilimo kujadili maboresho ya kilimo juzi.

Alisema katika mpango huo wa usambazaji wa mbolea kwa wakulima, mpaka sasa wakala aliyesajiliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA) ni Batoge Agribusiness and General Supplies.

Mbwambo alisema katika Halmashauri ya Muheza usajili wa wakulima ulianza rasmi Septemba Mosi mwaka huu baada ya Sensa ya Watu na Makazi kukamilika ambapo wilaya hiyo imepokea jumla ya vitabu 320 na vitabu 133 vimegawanywa kwenye kata 37 kupitia maofisa watendaji kata na vijiji na vitabu 187 havijatumika.

Mkuu wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Halima Bulembo, alisema TFRA inatekeleza mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbolea msimu wa mwaka 2022/23 kwa lengo la kuongeza uzalishaji, tija, kipato cha mkulima na kuimarisha usalama wa chakula nchini.

Alisema utekelezaji wa mpango huo unahusisha usajili wa wakulima, wazalishaji na waingizaji wa mbolea pamoja na mawakala watakaoteuliwa na kampuni kusambaza mbolea kwa wakulima kwa kutumia mfumo maalum wa kielektroniki.

Bulembo alisema kila ofisa ugani anatakiwa kusajili wakulima kwenye eneo lake kwa kutumia daftari maalum lililowasilishwa kwenye kila halmashauri za wilaya na taarifa za wakulima zitathibitishwa na viongozi wa eneo husika.




Ofisa Huduma kwa Wateja wa Benki ya NCBA, Maria Mabella (kulia), akimkabidhi pikipiki Richard Mkoba mkazi wa Pwani, ambaye ni mmoja wa washindi wa awamu ya pili wa kampeni ya Mpawa ya Chuzi Limekubali kwa kushirikiana na Vodacom. Kushoto ni Fulgence Otaru mshindi wa kampeni hiyo kutoka Dar es Salaam. Makabidhiano hayo yalifanyika katika viwanja vya Zakhem Mbagala mwishoni mwa wiki.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtendaji Mahakama aionya menejimenti kujivunia vyeo

**Na Mwandishi Wetu**

MTENDAJI Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, ameitaka Menejimenti ya Mahakama kuacha kusumbuliwa na vyeo bali ijivunie kutatua matatizo makubwa yanayowakabili wananchi.

Prof. Gabriel alitoa angalizo hilo jana alipofungua mafunzo ya siku tatu kuhusu uongozi bora kwa wajumbe wa Menejimenti ya Mahakama Tanzania.

Alisema lengo kuu la mafunzo hayo ni wote kuzungumza lugha moja kwa kuwa hakuna mafanikio bila kuhakikisha watendaji wote wanaelekea kwenye uelekeo unaofanana.

"Tunapozungumzia uongozi bora ni kuhakikisha mambo yanayofanyika sahihi na yanafanyika kwa usahihi.

"Ninyi siyo bomba tu la kupeleka mambo kwa viongozi, mnatakiwa kuchakata mambo na kupeleka kwa kiongozi wenu," aliagiza.

Prof. Ole Gabriel alisema uamuzi unaofanywa na watendaji unatakiwa umsaidie mwananchi anayetafuta haki yake, ipatikane kwa wakati na yenye tija.

"Katika uongozi bora haijalishi una nafasi gani, unatakiwa ujiulize una thamani gani ndani ya mahakama?" Aliagiza na kuwataka watendaji kutumia muda vizuri kwa kuwa Tanzania kuna shida ya 'kuchelewa kufanya mambo'.

Aliwakumbusha watendaji wakiwamo wasajili na wakurugenzi wa mahakama kuwa mahakama inatarajia kuhamia rasmi Dodoma Desemba 29, mwaka huu.

## NCBA, Vodacom wakabidhi pikipiki

**Na Frank Monyo**

BENKI ya NCBA kwa kushirikiana na Kampuni ya Mawasiliano ya Simu ya Vodacom Tanzania imetoa zawadi ya pikipiki (bodaboda) kwa washindi watatu wa Kampeni ya M-Pawa iliyopewa jina la 'Chuzi Limekubali'.

Zawadi hizo zilikabidhiwa jana kwenye Viwanja vya Zakhem Mbagala mkoani Dar es Salaam ikiwa ni mara ya pili kutolewa.

Kampeni hiyo ya NCBA na Vodacom ni mahususi kwa ajili ya kuwahimiza wateja kuweka akiba, kukopa na kurejesha mikopo ili kujishindia zawadi kila siku na kila wiki.

Mmoja wa mshindi wa bodaboda hizo, Fulgence Otaru, ambaye ni mfanyabiashara kutoka Dar es Salaam, alisema: "Ilikuwa vigumu kwangu kuamini mwanzoni, lakini baada ya simu kadhaa kutoka katika kitengo chao cha huduma kwa wateja, shaka yangu iliondoka.

"Nataka kuhimiza kila mtu aanze kuweka akiba na M-Pawa kwa sababu mikopo ni ya haraka na rahisi," alisema.

Richard Mkoba, mkulima kutoka Pwani aliyejinyakuliwa bodaboda, alipongeza kampeni hiyo, akikiri kuwa zawadi hiyo itainua shughuli zake za kilimo.

"Ninyi (NCBA) mmekuwa benki ya watu - pikipiki hii ina maana kubwa kwa safari zangu za kwenda na kurudi shambani. Siamini nilishinda pikipiki baada ya siku tatu tu za ushiriki. Asanteni sana," alipongeza.

Ofisa wa Huduma kwa Wateja wa NCBA, Maria Mabella, alibainisha kuwa M-Pawa imekuwa 'kipengele' muhimu kwa wateja kwa kuwa inainua matarajio ya Watanzania kupata mikopo ya haraka na yenye riba nafuu.

Mabella alisema; "Kwa upande mkubwa, kampeni hii inalenga kuwahamasisha wateja wetu nchi nzima na Watanzania kwa ujumla kuanza na kuendeleza tabia ya kuweka akiba ya fedha zao kupitia M-Pawa. "Fursa hii inawapa manufaa mengi zaidi ikiwa ni pamoja na kupata mikopo ya haraka na kwa riba nafuu kuliko sehemu au huduma nyingine yoyote," alisema.

Ofisa Huduma huyo alisema Tanzania ni mojawapo ya soko la kimataifa la ushindani na linalokua kwa kasi katika huduma za fedha kwa njia ya simu.

Kwa kulitambua hilo, Mabella alisema kampeni hiyo inatoa motisha kwa wateja kwa kuwa wana nafasi ya kujishindia pikipiki mpya kila wanaporejesha mikopo kwa wakati na kuweka fedha zao M-Pawa.

Mabella aliongeza: "Wateja wana nafasi ya kujishindia hadi Sh. 50,000, fedha taslimu wanaporejesha mikopo yao ndani ya siku sita. Kila wiki tangu wiki iliyopita tumewazawadia wateja zaidi ya 50 walilipa mikopo yao mapema na kuweka akiba."

Alisema kila mwezi wateja wanaoweka akiba katika kipindi hiki cha kampeni watakuwa na nafasi ya kujishindia mara mbili ya akiba yao kuanzia Sh. 10,000 na zawadi kubwa kuliko zote itakuwa kitita cha Sh. milioni tano mwishoni mwa kampeni.

Alibainisha kuwa kwa miaka mingi huduma ya M-Pawa imewanufaisha wateja wasiopungua milioni sita nchini ambao kwa sasa wananufaika na mikopo midogo ya hadi Sh. 500,000.



## Wanavuguvugu wataka sarafu moja Bara Afrika

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WANAVUGUVUGU wa Afrika wamesema watakwenda kuzishauri serikali za bara la Afrika kuwaunga mkono kwa azimio lao walilokubaliana la kuwa na sarafu moja itakayotumiwa na nchi zote za bara hilo.

Wakiwa Arusha katika Kituo cha Mafunzo na Uhusiano wa Kimataifa (MS TCDC) kwenye Kongamano la Muunganiko wa Vuguvugu la Waafrika (African Rising, All African Movements Assembly), walipitisha azimio kwa nchi za Afrika kuwa na sarafu moja.

Akizungumza wakati wa kufunga kongamano hilo, Mratibu Mwenza wa kongamano hilo kutoka Senegal, Coumba Toure, alisema kuwa baada ya kutamatisha kongamano, wamekubaliana kwenda kuzishirikisha na kuzishauri serikali za nchi za Bara la Afrika kuunga mkono azimio lao la kuwa na fedha yao wenyewe itakayotumiwa kwenye nchi zote za Afrika.

Alisema umefika wakati kwa Bara la Afrika kuwa na fedha yake kama zilivyokuwa nchi nyingine za Bara la Ulaya, Amerika na Asia.

"Kama nchi za Afrika zinataka kusonga mbele na kupiga hatua kwa kupata maendeleo, ni lazima tuwe na fedha yetu wenyewe kama ilivyokuwa kwa nchi zingine za mabara mengine," alisema.

Awali akifungua kongamano hilo, Mkurugenzi wa MS TCDC, Makena Mwabobia, aliwataka vijana wa Afrika kuungana kuwa kitu kimoja ili kutatua matatizo yanayowakabili Waafrika.

Alisema vijana hasa wale ambao wamechaguliwa kuwa viongozi, wanapaswa kuungana kuwa kitu kimoja kutafuta njia mbadala za kutatua matatizo yanayowahusu wananchi wa bara hilo.

"Asilimia 90 ya rasilimali zilizoko katika nchi zetu za Afrika zinamilikiwa na wachache ambao ni asilimia tano tu, hivyo viongozi vijana na wanaharakati tunatakiwa kubadilisha mfumo huo kwa kutafuta njia mbadala," alisema Makena.

# Shirika lamaliza tatizo la ukosefu maji kijijini

**Na Allan Isack,** ARUMERU

SHIRIKA lisilo la kiserikali la WAMATA limechimba kisima, kuweka miundombinu rafiki ya kuhifadhi na vituo vya kuchotea maji kwa wakazi wa Kijiji cha Themiyasimba katika Halmashauri ya Arusha.

Hatua hiyo imewawezesha wanawake wa kijiji hicho kuondokana na kero ya upatikanaji wa majisafi na salama iliyokuwa inawakabiri kwa miaka mingi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo, Mkurugenzi wa WAMATA, John Tarimo, alisema wamefanikisha uchimbaji wa visima hivyo kwa ufadhili wa Shirika la World Server la nchini Marekani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Suleman Msumi, aliwashukuru wadau hao kwa kutoa huduma hiyo muhimu kwa wananchi wa eneo hilo, akisema ni utekelezaji wa malengo ya serikali ya kumtua mama ndoo kichwani.

"Serikali inathamini kazi zinazofanywa na wadau kwa kusaidia kufanikisha vipaumbele vyake, tunawapongeza kwa kuwa mmewezesha kumtua mama ndoo kwa kuwa ni sera ya serikali," alisema Msumi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Themiyasimba, Mussa Msengi, alishukuru kwa utekelezaji wa mradi huo, akisema kwamba kabla ya kuchimbwa kwa kisima hicho kulikuwa na tatizo la ukosefu wa maji lililokuwa tishio kwa afya kwa wananchi wengi.

"Wananchi walikuwa na uhitaji wa majisafi na salama, tunaomba kama ikiwezekana kuongezewa tangi lingine ili maji yawafikie wananchi wengi zaidi katika vijiji vya jirani kwa kuwa kisima hiki kina maji mengi na ya kutosha,"alisema.

Baadhi ya wananchi wa kijiji hicho walilishukuru shirika hilo kwa msaada huo, huku wakieleza namna wanawake walivyokuwa wakiteseka kupata maji.

Happy Kaaya, Mkazi wa Nyamagana, alisema ukosefu wa maji katika kitongoji hicho, kuliwapotezea muda wanawake kwa kuwa walitembea umbali wa zaidi ya kilometa tano kwenda kutafuta maji, hivyo kitendo hicho kilidhoofisha hali ya afya na uchumi wa familia zao.

"Tumepata mkombozi kwa kuwa tulikuwa waathirika wakubwa kwa kukosa maji kwa kuwa tulitumia muda mrefu kwenda kutafuta lakini kwa sasa tunafuraha baada ya kupata huduma na imefika hadi kwenye zahanati yetu ya Themiyasimba, hivyo kinamama hatutateseka tena wakati wa kujifungua," alisema Happy.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha ambaye ni Kamishna Msaidizi wa Polisi, ACP Justine Masejo, akionyesha dawa za kulevya aina ya mirungi zilizokamatwa kwa mtuhumiwa mmoja aliyekuwa anazisafirisha jijini humo. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Viongozi wa dini watakiwa kumwombea Rais Samia

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WAZIRI wa Madini, Dk. Doto Biteko, amewaomba viongozi wa dini kuendelea kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan ili aweze kuendelea kutekeleza na kuboresha huduma mbalimbali za kijamii ikiwamo kuweka miundombinu rafiki na wezeshi kwa wananchi.

Aliyasema hayo jana mbele ya viongozi wa dini wakati wa jubilee ya kuadhimisha miaka 75 ya Kanisa la Elim Pentekoste Tanzania, iliyofanyika Mjini Babati.

Katika hafla hiyo Wizari Biteko alimwakilisha Makamu wa Rais, Dk.Philip Mpango aliyetakiwa kuwa mgeni rasmi.

Hafla hiyo ilitanguliwa na uwekaji wa jiwe la msingi kwenye ujenzi wa kanisa jipya la kanisa hilo.

Biteko alisema serikali inathamini mchango wa madhehebu ya dini kwa kuwa yanafanya kazi kubwa ya kuwapa maadili mema wananchi.

Alisema ili Rais Samia aweze kuendelea kufanya vizuri kwenye uimarishaji wa huduma za kijamii ikiwamo ya elimu, afya, maji, ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli na umeme ni vizuri viongozi wa dini waendelee kumwombea.

Biteko aliwasisitiza viongozi wa kanisa hilo kuwa na upendo na kushirikiana kwa ajili ya kujenga kanisa ambalo watu watakimbilia kupata kuponyaji wa matatizo yao yanayowakabili.

Alisema endapo watagawanyika hawataweza kujenga kanisa hilo, kama walivyokusudia badala yake watajikuta wanarudi kanisani kutubu kwa makosa waliyoyafanya.

Biteko alikabidhi Sh.milioni sita ili zisaidie katika ujenzi wa kanisa hilo.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Elim Pentekoste Tanzania, Peter Konki, alisema kanisa hilo, halijawahi kuingia katika mtafaruku na serikali na halitakaa lifanye hivyo bali litakuwa sehemu ya kuishauri serikali.

"Wale wanaomshauri Rais Samia tunaomba wampe ushauri wa kweli ili aweze kufanya vizuri katika kuwatumikia wananchi,"alisema Konki.

Alisema wao kama waumini katika kanisa hilo, hawana nchi nyingine mbali na Tanzania, hivyo baadhi ya watu wanaobeza na kuitukana serikali haisaidii.


Vile vile, aliiomba serikali kuwatumia watafiti kuangalia namna ya kuboresha miti ya asili.

Alisema jamii isipolinda mazingira kwa kushirikiana na serikali watoto wakikua watauliza na hakutakuwapo na majibu ya kuwapa.

Konki alisema maadhimisho ya miaka 75 yamefika kilele kwa kuwa yamefanyika mwaka mzima kwenye maeneo mbalimbali ya makanisa yao.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi, Daniel Sarwat, alisema ujenzi wa msingi umegharimu Sh.milioni 56 na hadi kukamilika kwa jengo hilo la ghorofa mbili itagharimu Sh.milioni 800.

Mwakilishi wa Kanisa hilo Uingereza, Roy Jonson, alisema hatua ya kanisa hilo kufikisha miaka 75 ni kama bado watoto, bali wanaendelea kuwa vijana.





## Waajiriwa sekta binafsi watakiwa kufuata sheria

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAAJIRIWA wa taasisi na mashirika mbalimbali mkoani Kilimanjaro, wametakiwa kufuata sheria za ajira na mahusiano kazini ili kuepuka migogoro katika maeneo yao ya kazi.

Rai hiyo ilitolewa na Wakili Kiongozi wa Kampuni ya Mawakili ya Kilimanjaro Elite Attorneys and Consultants, iliyoko mkoani humo, Emmanuel Anthon, wakati wa semina ya waajiri iliyofanyika Septemba mwaka huu.

Alisema lengo la kutolewa kwa semina hiyo ni kuwakumbusha majukumu yao maofisa rasilimali watu, menejimenti, wamiliki wa taasisi na watu wenye jukumu la kutoa uamuzi kwenye taasisi au mashirika kwa kuwa na uelewa wa sheria za ajira ili kuboresha ufanisi katika utendaji kazi.

Kwa mujibu wa Wakili Anthon, ili mwajiri awe sehemu salama katika ngazi zote, endapo kutatokea tatizo akiwa kazini pande zote zinapaswa kuzingatia sheria kuepuka migogoro isiyokuwa na tija.

Kadhalika, alisema mara nyingi waajiri wanachukua hatua za kinidhamu kwa mfanyakazi, pindi mfanyakazi anapotenda kosa na kuna ushahidi lakini linapokuja suala la kutoa uamuzi kinachowaangusha waajiri wengi ni kutokufuata sheria.

Alisema, waajiri wana nafasi ya kuwa salama endapo watazingatia matakwa na maelekezo ya sheria ili kutatua migogoro kwa kutumia njia salama.

"Kimsingi tumewajengea uwezo wa kutafsiri sheria pia kuwafungua katika maeneo ambayo yanahitaji utaalamu zaidi na tumewakumbusha kufuata sheria inavyoelekeza ili kuwapo kwa urahisi wakati wakitekeleza majukumu na kutoa uamuzi pale mgogoro unapotokea na wafanyakazi," alisema.

Naye Wakili Magdalena Kaaya, kutoka kampuni hiyo, alisema wamekuwa wakitoa mafunzo kwa waajiri kila mwaka mara moja ikiwa ni kuwakumbusha nafasi waliyonayo wakati wa kutoa uamuzi kazini.

Ramadhani Mchomvu, Mwajiriwa kutoka Kampuni ya Furahini Partners for Social Changes, alisema mafunzo hayo yamewajengea uwezo hasa katika suala la mikataba wanayopewa na taasisi na mashirika wanayofanyia kazi.

# Wataka wanaofanya shughuli Mto Mtangarini waadhibiwe

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WANANCHI wa Kata ya Sanya Juu, wilayani Siha, mkoani Kilimanjaro, wameomba serikali kuwachukulia hatua watu wanaofanya shughuli za kibinadamu katika Mto Mrangarini.

Walitoa ombi hilo kwa serikali baada ya kuwapo kwa madai kwamba baadhi ya watu wanafanya shughuli za kibinadamu ndani ya mto huo, ikiwamo kuosha magari.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kwa naiba ya wananchi wa eneo hilo, Somsoni Munuo, alisema wameamua kupaza sauti ili wadau wa mazingira wafanye jitihada za kunusuru vyanzo vya maji wasikie na kuchukua hatua.

Alisema mto huo ni muhimu na tegemezi kwa wananchi kwa kuwa wanautumia kwa shughuli za mbalimbali ikiwamo kunywesha mifugo na kumwagilia mazao yao.

"Ni kweli chanzo hiki ni muhimu kabla ya kuletwa kwa maji ya bomba miaka mingi iliyopita, wananchi walikuwa wakikitumia kwa ajili ya matumizi ya nyumbani ikiwamo kunywa baada ya kuchemsha, kufulia na kuogea.

"Hata sasa tuna maji ya bomba bado mto huu ni msaada kwetu, lakini baada ya watu kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya mto umeanza kukauka, tunaomba viongozi wa wilaya hii kuwa makini na mto huu usije ukakauka,"alisema Munuo.

Alisema chanzo cha mto huo kinamama walikuwa wakikitumia kwa ajili ya shughuli za kilimo ikiwamo kulima kwa muda mrefu, lakini kutokana na kuanza shughuli za kibinadamu kuosha magari na kupigia matofali kimeanza kukauka.

"Watu wanaofanya shughuli za kupiga tofali na kuosha magari ndani ya mto baada ya kuona chanzo hiki kinakauka wameamua kuchimba visima ndani ya chanzo hicho, ninavyofahamu mimi maji ni kwa matumizi ya binadamu suala la kuoshea magari na kupiga tofali ni hatua nyingine wakachimbe visima sehemu nyingine siyo kwenye chanzo,"alisema Munuo.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watumia Maji Mto Sanya (JUWAMMASA), Goodchance Moshi, alisema wanaochimba visima kwenye chanzo hicho wamewapa maagizo ya kuandika barua ya maombi ambayo itapitia kwa Mtendaji wa Kata na kupelekwa Ofisi ya Bonde la Pangani.

Alisema baada ya hapo wataalamu kutoka bonde hilo, watakuja kukagua sambamba na kuangalia kama watapewa vibali vya kuendesha shughuli zao.




Mwongoza watalii wa Kampuni ya Utalii ya ZARA Tanzania Adventures (ZARA Tours) mjini Moshi, Faustine Chombo (mwenye shuka la Kimasai), akiwa pamoja na watalii kutoka mataifa mbalimbali duniani katika kilele cha Mlima Kilimanjaro Uhuru Peak (5,895m ASL) mwishoni mwa wiki. Idadi ya watalii Mlima Kilimanjaro imeongezeka ikilinganishwa na miaka miwili iliyopita kufuatia tishio la UVIKO-19. **PICHA: JAMES LANKA**

# Walimu walia nyaraka zao kupotea wilayani

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WALIMU katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wamelalamikia kitendo cha nyaraka zao muhimu za madai kupotea katika masjala ya wilaya hiyo.

Kutokana na kupotea kwa nyaraka hizo, wamedai kwamba imeleta usumbufu kwa wale wanaokaa kata za pembezoni kwa kuwa wamekuwa wakitumia muda mwingi kufuatilia haki zao.

Hayo yalielezwa jana na Katibu wa Chama cha Walimu (CWT) Wilaya ya Moshi, Carolina Ng'eleshi, alipowasilisha kero zinazowakabili walimu hao kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Abbas Kayanda, wakati akizungumza na wawakilishi wa walimu kutoka shule za halmashauri hiyo.

"Suala la nyaraka za walimu kupotea katika masjala limekuwa tatizo kubwa kwa kuwa wapo wanaotoka mbali na mjini, hivyo wanajikuta wanatumia gharama kubwa kwenda kufuatilia madai yao,"alisema katibu huyo.

Alisema kero ya kupotea kwa nyaraka hizo imekuwa kubwa kwa kuwa inajirudia mara kwa mara na walimu wamelalamika sana, lakini tatizo linaendelea kujitokeza.

"Tunaomba Mkuu wa Wilaya utusaidie kufuatilia jambo hili kwa kuwa walimu wamekuwa wakilalamika sana mara kwa mara kuhusu nyaraka zao kupotea masjala ya wilaya yetu ya Moshi ili waweze kupata haki zao bila usumbufu,"aliongeza Katibu huyo.

Baada ya kupokea malalamiko hayo, alitoa agizo kwa Ofisa Utumishi wa halmashauri hiyo, kuweka utaratibu mzuri kwa walimu kupata haki zao kwa wakati bila ya usumbufu.

"Ofisa utumishi nakuagiza hakikisha unaweka utaratibu mzuri kwa walimu kupata haki zao bila ya kuwapo kwa usumbufu wowote kwa kuwa serikali inatambua mchango mkubwa wa kundi la walimu katika Taifa,"alisema.

Nipashe
TESA
Jumanne Septemba 27, 2022
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



## Ndivyo kasi wanyama kuhatarisha maisha duniani inavyoongezeka

Ukurasa 19



Ukurasa 14

## Mafanikio kielimu yanaanzia na ufuatiliaji kila hatua si kulipa ada

SAYANSI

**NA MWANDISHI WETU**

### KILIMO BONDE MSIMBAZI


# Wakati umefika kuachana na 'kwikwi' kulitangaza iwapo ni eneo hatarishi

KILIMO cha mboga na mazao mengine pembeni ya mito jijini Dar es Salaam ni kama kitendawili kisicho na jibu, kiasi kwamba hata ndani ya tope linaloweza kuwa na taka za sumu zenye madini mazito (tembo) kutoka viwandani na baharini watu wanayatumia kupanda mazao bila mamlaka zozote kuchunguza hali ya ardhi na maji ya eneo hilo ili kuchukua tahadhari.

Ni kilimo kinachoendelea Jangwani kwenye mdomo wa bahari lakini pia sehemu ya maji ya Mto Msimbazi yanapoingia baharini. Pamoja na taka za viwandani, zipo nyingine kutoka kwenye makazi, huku ukulima wa mboga na mazao mengine unaendelea japo ulihitajika kufanyika uchunguzi kwanza.

Kulima kwenye mabonde ya mito kumeenea kwa kasi katika maeneo mbalimbali lakini kinachoshangaza ni kwamba, kilimo cha pembeni au chini ya kingo za mto ni kinyume cha sheria kwa vile shughuli za uzalishaji zinatakiwa kufanyika umbali wa mita 60 kutoka kwenye ukingo wa mto, inakuwaje hilo linasahaulika.

Bila kuzunguka zunguka wakati umefika kutafiti na kutathmini athari za kimazingira na hasara za kilimo kinachofanyika Jangwani kwenye ukingo wa Mto Msimbazi ili kujua hivi ukulima huo ni salama? Udongo wa Jangwani licha ya kuwa mweusi na wenye rutuba, unyevunyevu mwingi na wa muda mrefu huenda kuna taka za sumu zinazotoka kwenye viwanda vingi viwe vilivyoko Barabara za Nyerere, Mandela, maeneo ya Vingunguti unaweza kuwa chanzo cha maradhi mengi lakini mamlaka hazijasema neno na kilimo kinaendelea.



Bamia moja ya mboga zinazostawi kwa wingi kwenye bonde la Msimbazi likizalishwa kwenye bustani zilizoko Kigogo, Jangwani na Buguruni. **PICHA: MTANDAO**

Wakati umefika wa uchanguzi wa 'data na taarifa udongo, ubora na ubovu wake kuangaliwa na wataalamu ikiwamo Hospitali ya Taifa Muhimbili iliyoko mita chache kutoka Jangwani, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na cha Ardhi kwa kutumia wahandisi wa mazingira, SUA, Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira na wadau wengi kwa kuangalia sampuli za maji na udongo hata mimea ya eneo hilo ili kuchukua hatua.

Wakati mwingine ikibidi serikali itangaze eneo hilo kuwa ni hatarishi au 'harzadous area'. Taasisi za serikali zisikae kimya zinapaswa kushirikiana ili kusaidia ili kuwe na kilimo cha mboga chenye afya kwa Watanzania kupunguza athari kiafya na uharibifu wa mazingira kwenye mito na kuwahakikishia wananchi usalama kwenye vyakula wanavyokula ili kupunguza uwezekano wa kupata magonjwa hatari kama saratani, maradhi ya figo, ngozi na mifupa.

Licha ya Jangwani kuwa ni sehemu yenye 'rutuba chafu na sehemu inayonuka' kando ya kingo za mto Msimbazi kwenye mdomo wa bahari, watu wanaweza kuhofu kuwa rutuba hiyo si salama kwa mazao yanayozalishwa kwa sababu inachafuliwa na kemikali za viwandani zenye madini na sumu nyingi.

Aidha ni mdomo wa bahari inawezekana taka nyingine zikatoka baharini, lakini pia rutuba hiyo inaongezwa na mafuriko ya msimu wa masika na mvua zinazoleta taka za vyooni kutoka makaro na vyoo vya wakazi wa bonde la

INAENDELEA UK. 18

ELIMU

NA PANKRAS LUOGA

# Mafanikio kielimu yanaanzia na ufuatiliaji kila hatua si kulipa ada



Wazazi na walezi wasijasahau baada ya kulipa ada, wakumbuke kufuatilia maendeleo ya watoto shuleni. Wawaulize maswali, kukagua madaftari na kuzungumza na walimu. **PICHA: MTANDAO**

UFUATILIAJI wa maendeleo ya elimu ya watoto zama hizi unayumba kwa sababu walezi na wazazi hawafanyi tathmini ya ufuatiliaji wa masomo darasani wakidhani kuwa jukumu lao ni kulipa ada na kuwapa mahitaji muhimu ya kishule.

Hilo linasababisha kujengeka utamaduni kuwa maendeleo ya darasani ni kazi ya walimu na uongozi wa shule na inavyoelekea linashamirishwa na kuenea kwa utandawazi na matumizi ya mitandao na kunakobadilisha mifumo ya maisha ikiwa ni pamoja na wazazi na walezi kujishughulisha na kusaka pesa.

Wengi hukosa muda wa kufanya ufuatiliaji wa

maendeleo ya elimu ya watoto na hata muda wa kuzungumza nao juu ya changamoto zao za kielimu. Ni kwa sababu wanatingwa sana na kutafuta hela hivyo, huondoka mapema alfajiri na kurudi kuanzia saa 3:30 usiku muda ambao watoto wamelala.

Hivyo, hupelekea kukosa muda au kutumia muda mfupi sana kukaa na watoto wao na wategemezi pia kushindwa kufanya tathmini na ufuatiliaji wa karibu wa elimu ili kutambua

maendeleo na changamoto za shuleni kwa watoto wao.

Mwisho wa haya yote ni madhara kwenye elimu ya watoto wao ikiwa ni pamoja na watoto kutofuata ratiba za masomo na kutoonekana darasani.

Wengi kutofanya kazi za darasani na nyumbani kikamilifu. Aidha, wapo wanaotoka nyumbani na kushinda mtaani kwenye michezo ya kompyuta na kutazama video na tamthilia, wengine wakuvutishwa bangi na dawa za kulevya hata kunyanyaswa kingono kwa kubakwa na kulawitiwa na kukatisha masomo.

Si hivyo, wapo wanaomaliza darasa la saba bila kujua kusoma, kuhesabu na kuandika. Wengine wakijihusisha na ulevi na uvutaji wa bangi na madawa ya kulevya, wizi na uhalifu ukiwamo wa panya rodi.

Chanzo kikubwa cha yote haya ni kutokuwapo kwa tathmini na ufuatiliaji wa karibu wa wazazi na walezi kwenye elimu ya watoto wao na mwishowe kutotambua maendeleo na changamoto zao kielimu.

**UFUMBUZI WA HARAKA**

Katika kutimiza jukumu hili la tathmini na ufuatiliaji wa karibu ambao ni muhimu katika kila kitu unachowekeza hasa fedha na nguvu kwenye elimu ya watoto ni vyema kila mmoja abebe jukumu hilo kuwa ni kazi yake kufuatilia maendeleo ya mtoto shuleni.

Afahamu kuwa kazi yake sio kulipa gharama za masomo pekee waanze kuwajibika wakiwa na watoto nyumbani hasa wakati wa jioni baada ya kumaliza shughuli zao za siku nzima. Mfano, wazazi na walezi wanaweza kuuliza nini wamesoma au kujifunza ikiwa ni pamoja na kupitia na kukagua daftari za watoto ili kuona kilichoandikwa pamoja na tarehe ya somo na siku alizokwenda shuleni.

Waangalie pia mazoezi waliyopewa na kujua iwapo wamefanya mangapi wamefaulu na yapi wameshindwa na kwa kiasi gani na mangapi hayajafanyika na kwanini hayakufanywa?

Pia, ni vyema kupitia maeneo ambayo mwalimu au walimu wamesahihisha au kutosahihisha kazi za watoto na kuulizia ili kujua sababu zake.

Zaidi ya hayo yote walezi na walezi wanatakiwa kufanya ufuatiliaji kwa kuhakikisha ratiba ya masomo ya watoto inafuatwa kikamilifu kama inavyotakiwa na kuondoa utoro, kutohudhuria masomo kwa muda Fulani na kuacha baadhi ya vipindi.

Ikibidi wazazi na walezi wanaweza kwenda shuleni na kuongea na walimu kuhusu maendeleo ya kielimu na changamoto za watoto wao ili kuzitafutia ufumbuzi.

Pia katika kutekeleza jukumu hilo ni muhimu wakazingatia misingi ya ufanyaji tathmini na ufuatiliaji wa karibu hasa katika utoaji wa rasilimali zao kuwezesha utekelezaji wa hatua za kubadilisha rasilimali na kuwa bidhaa au huduma na kurekebisha kasoro mapema ili mwishoni kufikia mafanikio ya kielimu kwa watoto wao.

Rasilimali zinazohitajika ni pamoja na mtoto kupelekwa katika shule yenye ubora , anapewa vifaa vya kujifunzia kama, kalamu, daftari na begi, nafasi na muda wa kujisomea na kufanya mazoezi aliyopewa na walimu wake.

Kingine ni chakula bora, upendo, heshima na kupewa hamasa za faida za kuweka juhudi katika elimu pia, thamani ya elimu katika maisha yake ya baadae.

Zaidi ya yote wazazi na walezi wajitahidi kuwa karibu na walimu wa watoto wao, na wafanye ufuatiliaji wa karibu kwa kuona rasilimali zinapatikana kuendana na mahitaji, hatua za kujifunza zinafanyika kwa usahihi ili mwishoni kufikia matokeo mazuri katika elimu ya watoto wao.

**FAIDA ZA KUFUATILIA**

Wazazi na walezi wakifanya tathmini na ufuatiliaji wa karibu kikamilifu juu ya maendeleo ya elimu ya watoto wao wataondoa matatizo ya utoro, kutomaliza darasa la saba au sekondari, kumaliza elimu ya msingi bila kujua kusoma, kuandika wala kuhesabu.

Juhudi hizo zitawawezesha kupata taarifa mapema kuhusu maendeleo ya watoto kielimu na kasoro zote hizo zikibainika mapema zinaweza kudhibitiwa na kukabiliana na mabadiliko ya kielimu kwa watoto kila mara au baada ya kupita muda fulani au ngazi fulani.

Kwa mfano, ufuatiliaji wa karibu unaweza kumsaidia kujua maeneo yapi ya elimu ya mtoto yanahitaji juhudi zaidi na kupewa kipaumbele katika mipango iwe ya muda mrefu au mfupi.

Aidha, ufuatiliaji wa karibu katika masomo hufanikisha kugundua upungufu walio nao watoto katika somo fulani kama hisabati au lugha au kusoma, kuhesabu, kuandika au kusikiliza.

Kutambua hayo husaidia wazazi kuanzia pale nyumbani pamoja na walimu shuleni kuongeza jitihada kumsaidia mtoto katika kurekebisha kasoro hiyo na kumuwezesha kufanya vizuri katika somo au eneo linalomsumbua kulingana na kasoro iliyojitokeza hapo awali.

Mfano wa juhudi hizo ni kama kumtafutia masomo ya ziada au 'tuition'katika eneo ambalo mtoto anapata changamoto. Na kama wasemavyo wahenga kuwa "kujua chanzo cha tatizo ni nusu ya kulitatua tatizo" basi kufanya tathimini na ufuatiliaji wa karibu katika elimu ni tiba ya kufikia malengo ya kuwa na elimu bora kwa watoto wa Tanzania.

Ikumbukwe kuwa, tathimini na ufuatiliaji wa karibu pia huwasaidia wazazi na walezi kujua vitu vilivyosaidia katika kuleta mafanikio au kushindwa kufikia mafanikio au malengo ya kielimu kwa watoto wao.

Wito wangu kwa jamii, wazazi,walezi kuwa wasiishie kuwalipia ada watoto bali pia wafanye tathimini na ufuatiliaji wa karibu katika elimu ili kujua maendeleo na changamoto za kielimu.

***Mwandishi ni Mhadhiri Msaidizi Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili***

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Sheria ya Ndoa 1971, kesi kuishia nyumbani 'petroli' inayochochea moto ndoa za utotoni



Mtoto akifungishwa ndoa ya utotoni. **PICHA:MAKTABA**

LICHA ya Mahakama ya Rufani Julai 8, 2016, kutamka kuwa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ifanyiwe marekebisho ili vipengele vinavyopingana na katiba ya nchi vifutwe, sheria hiyo haijaguswa na inatajwa kuwa ni kikwazo cha kukabiliana na tatizo la ndoa za utotoni.

Mkoa wa Shinyanga kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa kutetea haki za watoto, wanapambana kutokomeza tatizo la ndoa za utotoni, lakini kikwazo kikubwa ambacho wanakumbana nacho ni Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 na umalizaji wa kesi kimya kimya.

Sheria hiyo inaruhusu binti mwenye chini ya miaka 14 kuolewa kwa ridhaa ya wazazi au walezi wake, na miaka 15 mahakama ikiridhia.

Aidha, umalizaji wa kesi kimya kimya baina ya wazazi na walezi wa mtoto na upande wa mtuhumiwa kwa kupeana kitu kidogo, kumeendelea kusababisha kukosekana ushahidi mahakamani na kesi zinafutwa na watuhumiwa kuachiwa huru na vitendo hivyo kuendelea bila hofu.

Umalizaji kesi kinyemela unamwibua Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, anayekemea na kuwataka wazazi waache tabia hizo ambazo zimekuwa zikiumiza watoto na kuharibu dira ya maisha yao.

Takwimu za kitaifa na kimataifa zinautaja mkoa wa Shinyanga kuwa unaongoza kwa ndoa za utotoni kwa asilimia 59, ikifuatiwa na Tabora 58 na mkoa wa tatu ni Mara wenye asilimia 55.

Sophia anasema mzazi anapomaliza kesi hizo kimya na mtuhumiwa kuachiwa huru, ni moja ya sababu kubwa ya kuendelea kwa vitendo vya mimba na ndoa ya utotoni mkoani humo na kuzima ndoto za wanafunzi.

"Nachukizwa na vitendo hivi vya umalizaji wa kesi kimya kimya, hivi mzazi ukichukua hiyo hongo ya Shilingi 300,000 itakusaidia nini huku mtoto wako tayari ameshaharibiwa maisha yake,"anasema katika mahojiano na Nipashe kuhusu kukabili mimba za utotoni.

"Ukishamaliza hiyo kesi, unabaki umeachiwa mjukuu umlee na mama yake, na bahati mbaya mtoto wako kaambukizwa maradhi unaingia tena gharama ya kumtibu, na hako kahela ulikochukua kanaisha na kuanza tena kutumia pesa nyingine, hakuna ulichokifanya zaidi ya kuingia kwenye majukumu ambayo hukutarajia,"anaongeza na kuwataka walezi na wazazi kulinda na kuepusha watoto na uharibifu..

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anapozungumzia suala hilo anawasihi wazazi kuacha tabia ya kuzima ndoto za watoto wao na kuwaozesha utotoni, akisema.

Serikali imeboresha miundombinu ya elimu ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, ili watoto wote wapate elimu bora na kutimiza ndoto zao, na taifa pia lije lipate wataalamu wa kuchangia maendeleo.

> "Kesi inafunguliwa mahakamani wakati ikiendelea kusikilizwa na kupangwa tarehe, siku ya kusikilizwa tena mwanafunzi ana mkana mtuhumiwa na ukiwabana zaidi wanahama mkoa na kwenda kuishi kwingine mwisho inabidi umwachie huru mtuhumiwa na kuifunga kesi,"anasema Mary.

"Ukimsomesha mtoto wa kike utanufaika sababu watoto wa kike wanajali wazazi na kukumbuka kusaidia nyumbani kuliko wa wengine anasema Jasinta.

**MWIBA KISHERIA**

Mratibu wa Polisi Jamii Mkoa wa Shinyanga, Oswald Nyorobi, anazungumza kuhusu kikwazo kingine ambacho kimekuwa kikisababisha kumaliza tatizo la ndoa za utotoni kuwa ni sheria ya ndoa ya mwaka 1971, ambayo inaruhusu mtoto kuolewa kwa ridhaa ya wazazi, walezi na mahakama.

Anatolea mfano wa tukio ambalo limetokea Agosti 16, mwaka huu, katika Kijiji cha Manyada Kata ya Usanda wilayani Shinyanga, ambapo mtoto wa miaka 15 alikuwa akiozeshwa na wazazi wake, lakini walipowafikisha wazazi hao kwenye mikono ya sheria wakakingwa na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

"Kesi ya juzi tu hapa ya kukamata wazazi wakiozesha ndoa ya utotoni mwanafunzi imeishia juu juu tu, baada ya wazazi kusema kuwa waliridhia mtoto wao aolewe, wakakingwa na sheria ya ndoa ya mwaka 1971 ambayo inasema mtoto ana ruhusa ya kuolewa kwa ridhaa ya wazazi au mahakama," anasema Nyorobi.

Mkurugenzi wa Shirika la Agape John Myola, ambalo linatetea haki za watoto na anayeishi na watoto walioathirika na ndoa za utotoni, anasema katika juhudi zao za kupambana na vitendo hivyo hukwamishwa na Sheria ya Ndoa na umalizaji wa kesi kimya kimya.

Anasema endapo Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 itafanyiwa marekebisho, ili kutokinzana na sheria ya elimu na mtoto ambayo ina mlinda na kumtimizia mahitaji yake, ikiwamo kumpatia elimu bora bila ya ubaguzi.

Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 ina mtambua mtoto ni yule mwenye umri chini ya miaka 18, ambayo imelenga kuimarisha ulinzi wa mtoto, kwa kumpatia haki zake zote za msingi ikiwamo matunzo, chakula, malazi, mavazi, matibabu, pamoja na elimu bila ya kubagua jinsi yake.

Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mkoa wa Shinyanga, Mary Mrio, anasema umalizaji wa kesi kimyakimya, umekuwa tatizo la kuwatia hatiani watuhumiwa sababu ya kesi kukosa ushahidi.

"Kesi inafunguliwa mahakamani wakati ikiendelea kusikilizwa na kupangwa tarehe, siku ya kusikilizwa tena mwanafunzi ana mkana mtuhumiwa na ukiwabana zaidi wanahama mkoa na kwenda kuishi kwingine mwisho inabidi umwachie huru mtuhumiwa na kuifunga kesi,"anasema Mary.

Akizungumzia Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, anasema inapaswa ifanyiwe marekebisho ili isiinakinzana na sheria nyingine ambazo zinamlinda mtoto na imekuwa ikiwapatia wakati mgumu katika usikilizaji wa kesi hizo.

John Msabila mkazi wa Shinyanga, anasema wazazi wamekuwa wakimaliza kesi kimya kimya sababu ya kuogopa uhasamasa kwenye familia ya mtuhumiwa vijijini na mitaani.

Mratibu wa mpango mkakati wa kitaifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA) mkoani Shinyanga. Tedson Ngwale, anasema mipango ya serikali mkoani humo ni kuhakikisha hadi kufikia mwaka 2025 kusiwepo na ndoa za utotoni kabisa mkoani humo.

Anasema katika mipango hiyo wameanza mchakato wa kutunga sheria ndogo ambazo zitatumika kuzuia ndoa za utotoni, kwa wazazi kujaza fomu ambazo zitakuwa kwa viongozi watendaji wa vijiji, ili kujiridhisha kama bibi harusi anayeolewa siyo mtoto.

"Utungwaji wa sheria hizi ndogo utatusaidia kudhibiti tatizo la ndoa za utotoni, sababu kabla ya ufungwaji ndoa kutakuwa na fomu ya kujaza ambayo itakuwa kwenye ofisi za watendaji, na kabla ya kufungwa ndoa kutakuwa na tathmini ya kujiridhisha kama ndoa hiyo hafungishwi mtoto," anasema Ngwale akiongeza: Tunataka hadi kufikia mwaka 2025 ndoa za utotoni mkoani Shinyanga zisiwepo na kubaki kuwa historia."

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

WALIMU KAENI CHONJO

# Yadaiwa 'mnachemsha' kila mmoja anawabeza, kisa kulewa, uhalifu, unyanyasaji shuleni mpo



Mwalimu na mavazi ya kisasa 'fulana' akifundisha darasani. **PICHA: MTANDAO**

HESHIMA ya walimu imepotea pengine duniani kote kutokana na mambo mengine huenda hata kipato 'kiduchu' kinachangia lakini utandawazi nao unatajwa kuitikisa taaluma hiyo.

Ualimu unaotoa watu kwenye ujinga na kuwapatia maarifa, huku ukizalisha wataalamu mbalimbali wakiwamo madaktari, wanasayansi nguli, wanasheria na viongozi wakuu duniani haujaachwa na mitikisiko ya kukosa maadili kama ulevi kupindukia, mavazi yasiyo na heshima, uhalifu na hata unyanyasaji watoto kijinsia.

Miaka ya nyuma walimu walikuwa wakiheshimika zaidi ndani ya jamii, ambapo mwalimu akipita watu walikuwa wakisema yule mwalimu fulani anakuja na kumpatia heshima zote na hata kuwekwa kiti cha mbele kwenye mikusanyiko.

Haya yanaibuka wakati wa uzinduzi wa mikakati ya kuboresha elimu unaofanyika mkoani hapa unaofanywa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, na katika maeneo mengine viongozi wakifikisha ujumbe kuhusu walimu.

Karne hii ya 21 ya kizazi kipya na dunia ya utandawazi, heshima ya walimu haipo tena imeshapotea na kuonekana kama watu wa kawaida mno, anasema Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Uzogole iliyoko Manispaa ya Shinyanga Yusuph Mbundi.

Hata kwenye mikutano ya kijiji mwalimu alipozungumza jambo, wananchi walikubaliana na mawazo yake sababu alikuwa akiheshimika na wote, huku akipongezwa kwa kuonyesha njia na mwelekeo, anasema.

Anaeleza baadhi ya sababu za heshima ya walimu kupotea, kuwa wengine hawajitambui na wapo wanaoiga mabadiliko ya kidunia bila kujitambua kuwa wao ni kioo na mwanga unaomulika jamii.

Anasema, utandawazi umepoteza mwelekeo wa walimu wengi, kwa kuiga mitindo ya kisasa tofauti na taaluma inavyotaka, kusimamia nidhamu, hali ambayo imesababisha walimu kudharaulika.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, akishiriki uzinduzi huo, anataja sababu zingine ambazo zimesababisha heshima ya walimu kupotea, kuwa baadhi ya walimu

> "Zamani nakumbuka akipita mwalimu mtaani anahemishika kweli, utasikia yule mwalimu fulani amepita, hata akitoa ushauri una tija na kuzingatiwa, lakini siku hizi heshima hiyo haipo tena, walimu wanalewa kwenye baa na wengine wanavaa nguo za ovyo yote ni vurugu tupu,"anasema Mjema.

ni walevi, wanavaa nguo za nusu utupu, na wanatumia lugha za mitaani na hata kushiriki uhalifu kama unyanyasaji wanafunzi shuleni na vyuoni.

"Mwalimu ni kioo cha jamii lakini siku hizi walimu wamekuwa walevi wapo wanaovaa nguo zisizo na heshima, kujichubua, hata sasa hapo wanaofundisha 'ujinga' badala ya maarifa. Jamii inakuonaje lazima udharaulike," anasema Masumbuko.

Anaongeza: "Unamkuta mwalimu hata katika mazungumzo yake anatumia lugha za mitaani Shilingi 500 anaiita jero, wengine ni wachafu unapaswa uwe nadhifu muda wote uonekane tofauti katika mtindo wa maisha yako ndipo utaheshimika."

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anasema, heshima ya walimu inapotea hata ufundishaji nao unashuka na hatimaye wanafunzi wanapata matokeo mabaya shuleni.

Heshima ya walimu inapaswa kurudi kama zamani, pamoja na wazazi kuwaheshimu na kuacha tabia ya kuwadhalilisha tena mbele ya wanafunzi na hata wengine kufikia hatua ya kuwapiga, anasema.

Katika wilaya yake hataki kusikia mzazi akimdhalilisha mwalimu, atakaye bainika kufanya hivyo atamshughulikia, kwa sababu kazi yao ni kubwa inatoa wataalamu mbalimbali kama vile, wachumi, madaktari bingwa, wahandisi na viongozi wa ngazi zote.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, anawataka walimu kujitambua ili kurudisha heshima yao kama zamani na kuacha tabia ya kukesha kwenye baa wakilewa pombe tena za kienyeji, kuvaa mavazi yasiyo na heshima, kubaka na kukosa uadilifu.

"Zamani nakumbuka akipita mwalimu mtaani anahemishika kweli, utasikia yule mwalimu fulani amepita, hata akitoa ushauri una tija na kuzingatiwa, lakini siku hizi heshima hiyo haipo tena, walimu wanalewa kwenye baa na wengine wanavaa nguo za ovyo yote ni vurugu tupu,"anasema Mjema.

Wanajamii wakitoa maoni yao akiwamo mwananchi Joseph Jilala, anasema zamani mwalimu alikuwa akiogopeka licha ya kumheshimu, sababu ya unadhifu wake kuanzia nywele, mavazi, makazi hadi busara zilibadili jamii, lakini miaka ya sasa hawaheshimiki tena kutokana na kuiga maisha ya utandawazi.

Anaongeza kuwa, zamani kila mzazi alikuwa anatamani mtoto wake akihitimu masomo yake aje kuwa mwalimu, lakini baada ya kada hiyo kushuka kiheshima hakuna ambaye anautamani.

Anakiri baadhi ya walimu zama hizi wamekuwa mfano wa mambo yanayokwenda kinyume na maendeleo pamoja na maadili kama kuishi kwenye makazi duni, kushiriki kwenye uovu mfano, kukopa bila kulipa na wengine kuwa wateja wa pombe za kienyeji.

Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, Dafroza Ndalichako, anasema serikali imeanza mikakati ya kurudisha heshima ya walimu na sasa imezindua vitabu vitatu vya mikakati ya kuboresha elimu nchini.

Anakumbusha kuwa vitabu hivyo vimekuja ili kuelekeza mambo mbalimbali yanayopaswa kuzingatiwa na walimu na hatimaye kuboresha elimu na pia kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Anaeleza kuwa, ujumbe uliopo ni pamoja na mikakati ya kuboresha elimu kama kuimarisha nidhamu ya walimu, mafunzo ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji bora ili kuongeza ufaulu na kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazoikwamisha sekta ya elimu.

ELIMU

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

# Changamoto na yakujifunza kutoka kwa Wahadzabe- 4



Wahadza wanatunza mazingira, kwao hata miti yenye miiba wanailinda ili kuendeleza ikolojia na ustawi wa baioanuai. **PICHA: DK. FELICIAN KILHAMA**

NIANZE kwa kumshukuru Mungu ambaye kwa wingi wa rehema zake kwetu tunaishi na siyo kwamba sisi tuliohai ni haki yetu bali ni kwa neema yake yeye aliye Alpha na Omega.

Makala iliyopita nilifafanua kuhusu vyakula vya Wahadzabe hasa matunda, leo ninakamilisha simulizi ya maisha yao katika eneo la Yaeda-Chini, wilayani Mbulu, Mkoa wa Manyara kama jamii na changamoto zinazowakabili na nini kifanyike kuboresha maisha yao.

Kwa upande wa huduma za jamii, wadau wanapendekeza serikali ya Wilaya ya Mbulu ianzishe huduma za shule na afya. Yaeda-Chini, kuna makazi ya watu mbalimbali karibu na msitu ambako Wahadza wanaishi. Ili kuinua na hali zao kielimu, imeanzishwa shule ya msingi na sekondari ili watoto wa Kihadzabe waelimike.

Lakini Wahadzabe hawakai ilipo shule, ila mara mojamoja hutembelea sehemu hiyo kupata baadhi ya mahitaji kama tumbaku au sigara. Hata hivyo, niliozungumza nao wanasema, pamoja na shule kuwapo 2007, wanafunzi ni wachache sana na walimu ni shida. Wahadzabe hawajawa na mwamko wa kuwapeleka watoto wao shule. Na hao wachache waliojiunga bado ni watoro hawahudhurii masomo ipasavyo.

Siku nilipotembelea shule ya msingi hakukuwapo na mwalimu wala mwanafunzi ni kawaida watoto wanakaa na wazazi wao huko msituni wakijifunza kwa vitendo yale wazazi wanayofanya. Hii ni pamoja na namna ya kuwinda, kutafuta na kurina asali kutokana na nyuki wasiouma na wanaouma na kutafuka matunda.

Baada ya kutembelea baadhi ya sehemu wanazoishi ilionekana kuwa Wahadzabe hawaishi wote sehemu moja; bali wanakaa katika makundi yenye watu 10 hadi 20 na kila kundi likiwa na nguvu sawa na jingine. Ilifahamika pia kuwa makazi yao ni ya muda yanayobadilika kulingana na hali ya hewa na mahitaji muhimu kama chakula na upatikanaji wa maji.

Kijamii hujiita 'kundi' na hawana upekee bali huwepo ushirikiano wa makundi mbalimbali. Wanasema 'kukitokea jambo fulani makundi hujadiliana na kufikia msimamo wa pamoja na kila moja kutekeleza makubaliano ipasavyo. Mathalani, kukitokea kutokuelewana baina yao, hufanya majadiliano kwa amani mpaka waafikiane. Nilifahamishwa kuwa kulea watoto ni kazi ya wote bila kujali nafasi ya mzazi baba au mama, wote hushiriki.

### HUKIMBIA KIFO

Hata hivyo kulingana na hali ya mazingira yao, wanasema vifo kwa watoto chini ya miaka mitano ni vingi kama asilimia 20. Kwa upande mwingine wapo wazee ingawa hawana kumbukumbu za kuzaliwa kwao wana zaidi ya miaka 80 na bado wana nguvu.

Wahadzabe wanakiona kifo kama adui wao mkubwa hivyo kinapotokea wanalazimika kuihama kambi kwenda kwingine na hali ikiwa hivyo 'sehemu inakuwa yenye mikosi na haifai kuendelea kuishi' na wanaweza kugawanyika katika makundi mawili tofauti iwapo kundi limekuwa kubwa. Wanaongeza kuwa sehemu ya kuanzisha kambi inaashiriwa na upatikanaji chakula kwa wingi hasa matunda. Kadhalika, ukame na hali mbaya na mbadiliko ya tabianchi hupelekea kuhamisha kambi kutoka sehemu kwenda nyingine.

### MASUALA KIJAMII

Kuhusu maji wanasema zamani yalikuwa tele msituni lakini kwa miongo miwili sasa upatikanaji wake ni changamoto kubwa hasa nyakati za ukame na kiangazi. Moja ya jadi yao muhimu ni uwindaji hiyo. Wanasema kuwa iwapo mwindaji ataua mnyama mkubwa kama twiga, nyati, simba, nyumbu au nyani kambi huhamia mahali mnyama alipouawa. Ikitokea akawa mnyama mdogo nyama yake huletwa kambini.

Haikujulikana kama Wahadzabe ni wenye umri mkubwa kwa sababu wanasema hawahangaiki na umri; isipokuwa msingi wao ni heshima kwa wote wanawake kwa wanaume na wanapewa uhuru na kuheshimiwa ipasavyo. Kimila mwanamume anaweza kuishi nyumba moja na mama mkwe lakini siyo baba mkwe.

Kijana akitaka kuoa na kuanzisha familia yake lazima awinde na kuua nyani mkubwa na kutolewa kwa mahari kwa wake, inayopokelewa kwa shangwe. Wanaeleza kuwa hawana dini yoyote, isipokuwa kuabudu na kutambika kwa kufanya maombi kwa 'ishoko' au jua na 'haine' kumaanisha mwandamo wa mwezi mume wa 'ishoko'. Kadhalika, utmaduni kama ngoma ya wanaume iitwayo 'epeme' inayochezwa wakati wa giza hakuna mwanga wa mwezi na dansi isiyoshabikiwa kila wakati ya 'maukolo' wakati wa kutahiri na 'kuvunja ungo' mabinti kuashiria kukua kwao.

Kwa maelezo yao nyakati za nyuma masuala haya yalikuwa yanaheshimiwa na kupewa umuhimu mkubwa. Lakini siku hizi yamepungua umuhimu wake baada ya kuwepo na mwingiliano na watu kutoka makabila mbalimbali hata watalii.'Epeme' ni suala la kimila kwa wanaume walio na zaidi ya miaka 20 kuashiria ukomavu. Hapa suala la uwindaji linapewa kipaumbele ili kuwa sehemu ya 'epeme' kijana lazima aue nyati, twiga, nyumbu, nyani au simba.

Sehemu muhimu za nyama wanaziita 'epeme meat' ni pamoja na figo, moyo, mapafu, shingo, maini na ulimi. Hairuhusiwi kijana ambaye hajaua mnyama kushiriki lakini iwapo atafikisha miaka 30 bila kuua mnyama atahurumiwa na kuingizwa kwenye kundi la 'epewe'. Pamoja na huruma hiyo vijana wengi hupenda kuwa sehemu ya wakiwa wameua mnyama.

### CHANGAMOTO

Wahadzabe wanakumbwa na changamoto nyingi ikiwamo kuingiliwa na watu wengine, watalii hasa utalii wa uwindaji na msitu wanamoishi kuwa eneo la uwindaji wa kitalii. Vilevile, mabadiliko ya tabianchi ni tishio kwa maisha yao maana ukame unapozidi ikolojia ya msituni hubadilka, maji kukosekana na chakula kupungua sana. Wanasema siku hizi wanalazimika kula 'ugali' kitu ambacho hawakuzoea.

Changamoto nyingine ni kunywaji pombe na kuvuta tumbaku na sigara kupindukia. Wamejengewa kituo cha afya Haydom, wanakopata matibabu lakini hali hiyo imekuwa ikitumiwa wa baadhi ya watu waishio Haydom au sehemu nyingine, kuwalewesha pombe na hatimaye kubaka wanawake hata kusababisha baadhi kuambukizwa UKIMWI au magonjwa mengine ya ngoo.

Wanapoulizwa nini kifanyike kuboresha maisha yao wanasema, serikali na wadau wahakikishe haki za Wahadzabe zinaheshimiwa na wawezeshwe kisheria kulimiliki eneo wanalolitegemea kwa maisha yao ya kila siku kwa kuzingatia sera na sheria zilizopo hasa Sheria za Ardhi ya Vijiji ya1999, ya Wanyamapori ya 2009 na ile ya Misitu na Nyuki za 2002.

Kwa kuwa serikali na wadau wanataka kuinua hali zao za maisha kupitia elimu na huduma nyingine kama afya, miundombinu na maji; vema suala hili likafanyika kwa weledi ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha taratibu, kuheshimu mila na desturi zao. Kituo kilichojengwa Haydom, ni mwanzo mzuri lakini kitumiwe kwa nia njema ya kuwasaidia Wahadzabe waweze kusogea mbale kimaisha na siyo kinyume chake au kwa maslahi binafsi.

Yapo mambo mazuri ya kujifunza hususani jinsi walivyoweza kuutunza msitu kwa miaka mingi bila kuuharibu kwa kuchoma moto wala kukata miti hovyo. Kinachohitajika ni jinsi ya kuwasaidia wasiathiriwe haraka na maisha ya kisasa kwa kuwalewesha au kuwarubuni kwa sigara inayodhuru afya. Twende nao taratibu mwisho watoto watapenda shule, watasoma na hatimaye watakuwa wa kwanza kuibadili jamii yao na kuingia katika maisha mapya bila kutegemea sana rasilimali misitu kwa maisha yao.

# Wakati umefika kuachana na 'kwikwi' kulitangaza iwapo ni eneo hatarishi

**INATOKA UK. 13**

mto huo wanaelekeza uchafu wa vyoo mtoni, hivyo isingefaa kulima au kunyamaza na kuacha kilimo kiendelee bila kukataza.

Uchafuzi wa mto huo uchunguzwe pengine unahusisha sumu za viwandani, japo inafahamika kuwa kuna taka za vyooni ambazo si suala lenye afya kimazingira kwani licha ya kutofanyiwa utafiti na wanaolima wakakatazwa au kutakiwa kuachana na kilimo hicho bidhaa zinazozalishwa Jangwani haziwezi kuwaacha walaji salama.

Zinaweza kuwa tishio kubwa kwa afya ya binadamu kwa sababu metali nzito na dawa za kuulia wadudu (viuatlifu) kutoka sehemu mbalimbali ziko ndani ya maji na huenda zimeshaanza kuhatarisha maisha ya walaji.

Ni wakati wa kufanya tathmini na kuaangazia athari ya sumu ya metali nzito kama 'cadmium, risasi, shaba, na zinki' pia dawa za kuua wadudu (viuatilifu) viua magugu na kuvu au fangasi, sumu nyingine zinazotupwa mtoni.

Kama yote hayo yamo ndani ya Mto Msimbazi kwanini bonde lake lisiwe sehemu hatarishi na kutangazwa kisheria kuwa ni sehemu ya kukwepa?"

Ni wazi kuwa taka za sumu zimeathri mfumo wa ikolojia, kilimo cha mboga na mimea, wanyama na na udongo na hata afya ya binadamu. Zaidi ya hayo, mrundikano wa metali nzito na mabaki ya viua sumu kwenye udongo wa eneo hilo, huongeza zaidi tahadhari.

Mahojiano yaliyofanywa na baadhi ya wakazi wa Jangwani wanaolima mazao mbalimbali kama mboga, mahindi na ndizi wanasema kulima kwenye Bonde la Jangwani hakujaanza leo na kwamba CCM na serikali ndiyo waanzilishi na wasingelima kwenye bonde ambalo si salama.

Baadhi ya wakulima wanaeleza kuwa miaka ya mwishoni mwa 1980



Mafuriko Jangwani yakitishia hata usafiri, maji yanayoingia kwenye eneo hilo la Mto Msimbazi yenye taka za kila aina hatarishi huongeza rutuba kwenye mabonde na kufanikisha kilimo cha mboga zinazoliwa na mamilioni ya wageni na wakazi wa Dar. **PICHA: MAKTABA**

CCM ilikuwa na Shirika la Uchumi na Kilimo-SUKITA lililokuwa na uwekezaji mkubwa kuanzia kufuga kuku, nguruwe, samaki na kulima kwenye maeneo mbalimbali ya Mto Msimbazi na kwamba wasingefanya hivyo bila kutumia wataalamu wa kuchunguza kwanza athari za mazingira.

Wanaamini kuwa serikali ililiona eneo hilo kuwa linafaa kiuwekezaji ndiyo maana na wakulima wa sasa wa mboga na mazao mengine wanautumia utetezi huo licha ya kwamba si salama na pia wanaamini kuwa kama kungekuwa na athari wangekatazwa kuendeleza kilimo Jangwani.

**SIFA ZA MSIMBAZI**

Kwa mujibu wa taarifa za jiografia ya Dar es Salaam, mto huo ni wa pili kwa urefu jijini Dar Salaam unaoanzia katika Milima ya Pugu na kutiririsha maji kwenye Bahari ya Hindi.

Una urefu wa karibu kilometa 32 na eneo la vyanzo vya maji zaidi ya 200. Mito yake muhimu ni pamoja na mito Sinza au Ng'ombe, Luhanga au Ubungo na Kinyerezi. Kuna Mto Mpiji, Mbezi lakini pia kuna vijito na mabonde yenye makazi kama Kigogo, Mwananyamala na Buguruni ambayo mwanzoni yalikuwa yanatumiwa kwa kilimo kabla ya kugeuzwa kuwa makazi japo duni na yenye mafuriko.

Uchunguzi wa nyaraka za serikali kuhusu ardhi unabaini kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi haijatoa Tangazo la Serikali (GN) lolote kuhusu usalama au 'uhatarishi' kwa maisha kwenye bonde hilo.

Lakini, mwaka 2007, lilitolewa tangazo namba 227 lililochapishwa Agosti 2011 likisema Tangazo la Mipango Miji (Eneo la Mto Msimbazi, Eneo Maalum la Mipango 2011, kuwa sehemu yote ya ardhi kuanzia Daraja la Salenda hadi Vingunguti litaendelezwa kuwa 'paki' sehemu ya burudani kibiashra," lakini hadi sasa hilo halijafanyika tangu 2011 na imetimia miaka 10 sasa.

## WANENAVYO MALENGA

### VIONJO USWAHILINI

VIONJO Uswahilini, Kijiji cha Makumbusho,
Mpango uko mbioni, kuanza leo si kesho,
Kazi za Uswahilini, ziwe kwenye maonyesho,
Upande huu mwema, ungekuja toka jana.

Hapa ni Watanzania, kufanya majumuisho,
Yale wanajifanyia, yafanyiwe maonyesho,
Watu wapate tumia, waingie kama josho,
Ni utalii nyumbani, ungekuja toka jana.

Mavazi ya hapa kwetu, kwa watu yawe fundisho,
Na chakula hiki kwetu, kilete virutubisho,
Hata ngoma ngoma zetu, kina Mpoto Mrisho,
Utalii wa nyumbani, ungekuja toka jana.

Ni Royal Tour nyingine, yakudumu maonyesho,
Watakuja na wengine, kupata viburudisho,
Zitakuja pesa nene, kuikuza Makumbusho,
Utalii wa nyumbani, ungekuja toka jana.

Yote ya Watanzania, Kijiji cha Makumbusho,
Ndivyo tutajiuzia, leo kuendea kesho,
Watu watapafikia, kwa raha na bila jasho,
Utalii wa nyumbani, ungekuja toka jana.

Lugha yetu Kiswahili, kutakuwa mafundisho,
Japo ya hapa mahali, yaenea hadi mwisho,
Wanaongea Wandali, hata watu Kibosho,
Utalii wa nyumbani, ungekuja toka jana.

Dokta Noel Lyoga, ya Taifa Makumbusho,
Mbiu hii anapiga, kama vile uamsho,
Ni kweli siyo kuzuga, Kijiji cha Makumbusho,
Utalii wa nyumbani, ungekuja toka jana.

Vionjo Uswahilini, Kijiji cha Makumbusho,
Zao la utamaduni, lataka utambulisho,
Iwe ni kote nchini, kule kwenye makumbusho,
Utalii wa nyumbani, ungekuja toka jana.

Huu mpango mzuri, Kijiji cha Makumbusho,
Huu wetu utajiri, taleta utajirisho,
Tuutumie vizuri, udumu pasipo mwisho,
Utalii wa nyumbani, ungekuja toka jana.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

SAYANSI

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Ndivyo kasi wanyama kuhatarisha maisha duniani inavyoongezeka

## Wanabeba ebola, ndui ya nyani, corona



Wanyama hawa ni miongoni mwa wanaotishia usalama wa maisha. Lakini zama hizi zinashuhudia ujio wa magonjwa hatari yakiwamo ya virusi ambayo hayana dawa wala kinga kutoka kwa wanyama yakiwashambulia binadamu. **PICHA: MTANDAO**

SEPTEMBA 2013, mlipuko wa kwanza wa virusi hatari vya ebola ulianza katika kijiji kilichoko kusini mwa Guinea, ulijulikana kama ebola ya Zaire.

Kwa mwaka mmoja haukutambuliwa rasmi na mamlaka ya afya hadi Machi 2014, ukiwa umeambukiza watu 18,000 na vifo 6,300, na kusababisha changamoto ambayo haijawahi kushuhudiwa kwa afya ya umma duniani.

Usafiri wa ndege ulisaidia ugonjwa huo kusambaa kutoka Afrika Magharibi hadi mabara mengine ikiwamo Amerika Kaskazini na Ulaya.

Chanzo kinadaiwa kuwa uwindaji au utunzaji wa wanyamapori hasa jamii fulani za popo ndio wanaoshukiwa kuwa chanzo cha asili cha virusi hivyo na wanadhaniwa kuvihifadhi bila dalili za ugonjwa.

Watafiti wanahisi maambukizi ya ebola yanahusika na vifo vya sokwemwitu, sokwe, na swala aina ya 'duiker' na ushahidi kutoka kwa maambukizo ya binadamu unaonyesha kwamba viumbe hao ni makazi (hosti) kwa muda na ndiyo wanaowaambukiza binadamu wakati wa kuwindwa, kuwabeba na kuwala.

**MARBURG**

Virusi vya Marburg, ni mifano mingine ya mwelekeo unaojitokeza wa binadamu kushambuliwa na magonjwa ya wanyama yote hayo yanaashiria kuongezeka kwa mawasiliano ya binadamu na wanyama ambayo kama hayatarekebishwa binadamu hataweza kubaki salama.

Ndui ya nyani/kima, Congo inakuwa tena chanzo cha maradhi ya ndui ya nyani ambayo 2019, iliripotiwa kuwa DRC ilikuwa na wagonjwa 3,794 na vifo 73, katika miezi tisa ya kwanza ya 2020, iliripoti zaidi ya wagonjwa 4,500 wakihusishwa na ndui hiyo ya tumbili au nyani au kima. Iliambatana na vifo 171.

Mafua ya ndege hujulikana kama homa ya mafua ya ndege. Inaambukizwa na virusi vya mafua ya ndege (ndege) aina A. Virusi hivi kwa kawaida huenea kati ya ndege wa porini wa majini na wanaofugwa kwani huambukiza kuku wa kienyeji na aina nyingine za ndege na wanyama.

Hata virusi vya COVID-19 vilidaiwa kusambaa kutoka kwa wanyama kama popo na kuingia kwenye mifumo ya mapafu ya binadamu kutokana na ulaji nyama za wayama hao.



**PANYA**

Kwa Tanzania mamilioni ya nyumba yana wageni wasiokubalika kwa njia yeyote nao ni panya. Uwapo wao unaambukiza maradhi, ni hatari za kiafya za kuwa na idadi kubwa ya panya nyumbani ni hatari, Tauni ni ile iliyoua mamilioni ya watu wakati wa enzi za zamani inaweza inatokana na viroboto wa panya ni hatari kwa maisha ya watu hata sasa.

Panya pia, husababisha ugonjwa wa' 'hantavirus' unaoweza kutishia maisha ambao kwa sasa hauna tiba au chanjo mahususi.

Dalili zake ni homa, uchovu, maumivu ya misuli (kwa ujumla kwenye nyonga, mgongo na mapaja) haya yanaweza

kujumuisha, kuhara maumivu ya tumbo, kichefuchefu na kutapika.

**EBOLA LEO**

Nchini Uganda idadi ya watu waliofariki kwa maradhi hatari ya ebola imeongezeka na kufikia 21 huku kukiweko na taarifa za kuenea kwa kasi kwa maambukizi ya maradhi hayo, inasema taarifa ya UN NEWS jana.

Ikiongeza kuwa, miji mingine kadhaa katika nchi hiyo ya Afrika Mashariki imeripoti kuwapo kwa maambukizo ya ebola na kuzua wasiwasi mkubwa miongoni mwa wananchi.

Serikali hiyo imetoa agizo kwa Wizara ya Afya kuchukua hatua za kuudhibiti ugonjwa huo sambamba na hatua zaidi za tahadhari kama kuwafuatilia watu waliokutana na wagonjwa wa maradhi hayo.

Wakati huohuo, mataifa ya Afrika Mashariki kama Kenya na Tanzania yametangaza umakini na kuchukua tahadhari katika mipaka yake na Uganda, kuhakikisha kuwa virusi hivyo havisambai.

Mlipuko wa ugonjwa ebola mara ya mwisho ulitokea mashariki mwa Jamhuri ya Congo, ambapo ulianza Agosti 2018 na kusababisha vifo vya watu zaidi ya 1,800.

Kumekuwako kwa milipuko minne nchini Uganda na mara ya mwisho Uganda iliripoti mlipuko wa maradhi hayo hatari mwaka 2021.

Ebola ni ugonjwa hatari ambao unaweza kusababisha kifo na huupata binadamu na nyani. Ebola ina aina sita ya virusi, ambavyo vitatu kati yao ni Bundibugyo, Sudan, na Zaire na vimesababisha milipuko.

Mlipuko mkubwa zaidi wa ugonjwa hatari wa ebola ulitokea Disemba 2013 na Aprili 2016 na kuua zaidi ya watu 11,000 katika nchi za Guinea, Liberia na Sierra Leone huko Afrika Magharibi.

***MITANDAO***

## HABARI PICHANI



Mbuzi na kondoo wakipata barabarani bila kuongozwa na mchungaji Kibamba Kwa Mangi, Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam jana. Eneo hilo kwa sasa kuna mnada wa kuuza mifugo hiyo, ambao hufanyika katikati ya wiki.



Mafundi wakiendelea na kazi ya kuweka lami katika barabara ya Stendi ya Magufuli Mbezi Luis Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam juzi, ikiwa ni sehemu ya uboreshaji wa stendi hiyo.



Mafundi wakijenga kituo cha daladala eneo la Njia Nne barabara ya Goba Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Baadhi ya maeneo ya barabara hiyo, hayana vituo ya kupumzikia abiria wakati wakisubiria usafiri. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

## CHEMSHABONGO NA -00 4 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. zuiwa kuongea
5. boflo
6. aina ya kahawa
8. dosari
10. Rais wa sasa Kenya
12. chimbuko
14. hisani
15. kifaa cha kuangalia muda

Chini:
1. boma
2. fuata
3. Safu ya milima Amerika ya kusini
4. nchi ambayo ni bara
7. fanya kavu
9. serikali
10. kiongozi mkuu wa jamhuri
11. miezi ambayo mama hubeba ujauzito
13. kiungo kitoacho nyongo





Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:


| | |
|---|---|
| TAMAA | MKOSI |
| USALAMA | ONA |
| HAMAKI | IGA |
| ASMINI | OKA |
| ADANA | OGA |
| IGIZO | ANA |
| MADA | ZOMEA |
| ZANZIBAR | AGA |
| NADAMA | ANGA |
| BAINIKA | RAI |
| SHANGA | UBORA |
| KAMASI | ADIMU |
| ILIKI | ANASA |
| | AGO |

U B O R A

Majibu toleo lililopita

KINSHASA M
A U A A
MOMBASA ARI
A J E
TRUMP K
W S W A
AMINA N
NIGERIA
ITIKA S
WAASHI
A I A





MAKOSA
A ANA KOMA
KINAI A AU
ANI DUMAZA
ISHI BIA
M A AGANO
B H I M
UPANGA K B
G S NYAKA
ABIRIA O

maoni: 0755429240



## Polisi: Ole wao watakaokutwa na silaha haramu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limewatahadharisha wananchi wanaomiliki silaha kinyume cha sheria kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria endapo watapatikana nazo wakati wa operesheni maalumu ya ukaguzi.

Tahadhari hiyo imetolewa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Kamishna Msaidizi wa Polisi Benjamin Kuzaga, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu operesheni mbalimbali zinazofanyika mkoani humo.

Alisema, jeshi hilo lilishatoa muda maalumu wa wananchi wanaomiliki silaha hizo kuzisalimisha na kwamba baada ya muda huo kuisha operesheni zitafanyika za kusaka wanaomiliki silaha hizo kinyume cha sheria.

Alisema, waliainisha maeneo ambayo silaha hizo zinatakiwa kusalimishwa kuwa ni pamoja na vituo vya polisi na ofisi za serikali za mitaa na kwamba yeyote ambaye anasalimisha kwa hiyari hatachukuliwa hatua yoyote ya kisheria.

"Tutakapoanza kuzisaka wenyewe na tukamkamata yeyote akimiliki silaha hizo, hatua kali sana zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria maana tulishawapa muda maalumu wa kuzisalimisha.

Alisema, mchakato huo ulizinduliwa jijini Dodoma mwanzoni mwa Septemba na kwamba operesheni za kusaka silaha hizo itaanza mwanzoni mwa Oktoba.

Kamanda Kuzaga, aliwataka wananchi wanaotaka kusalimisha silaha hizo kuendelea kufanya hivyo kwenye maeneo yaliyoainishwa na kwamba hawatachukuliwa hatua zozote za kisheria.

**"Tutakapoanza kuzisaka wenyewe na tukamkamata yeyote akimiliki silaha hizo, hatua kali sana zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria maana tulishawapa muda maalumu wa kuzisalimisha.**

# China kuwekeza kilimo cha soya, maparachichi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI ya China imeahidi kupeleka wawekezaji kwenye sekta mbalimbali mkoani Mbeya kwa lengo la kukuza uchumi na kuimarisha uhusiano baina yake na Tanzania.

Pia, imeahidi kupeleka wawekezaji kwenye sekta za kilimo, hasa cha soya na maparachichi ambayo ni miongoni mwa mazao ambayo soko lake ni kubwa katika taifa hilo.

Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, aliyasema hayo juzi alipofanya ziara mkoani Mbeya na kufanya mazungumzo na Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera alisema, serikali ya nchi hiyo imevutiwa na hali ya hewa ya mkoa huo.

Alisema, mbali na mazao hayo pia wanatamani kuwekeza katika sekta ya madini hasa katika Wilaya ya Chunya, kwamba watatumia teknolojia zao kwenye uzalishaji kwenye sekta zote watakazowekeza.

"Tunaamini kwamba mkoa huu ni sehemu sahihi ya kuwekeza, tumevutiwa na mazingira ya mkoa huu na tupo tayari kuwaleta wawekezaji kutoka nchini kwetu tiunachoomba ni ushirikiano wa viongozi wa mkoa," alisema Balozi Mingjian.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema serikali ya mkoa huo iko tayari kuwapokea wawekezaji hao na kuwaandalia maeneo ya kuwekeza kwa ajili ya maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Alisema, yapo maeneo mbalimbali ya uwekezaji ambayo yameandaliwa katika kila wilaya na kwamba huko ndiko watakakowapeleka wawekezaji hao wa China.

Homera, aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya kujiandaa kunufaika na wawekezaji kutoka China kwa kuanza kuzalisha mazao mbalimbali ambayo wawekezaji hao watakuwa wanayahitaji kwa ajili ya kusafirisha kwenda maeneo mbalimbali.

Alisema, mbali na kuwekeza kwenye sekta hizo mbili pia aliomba Serikali ya China kusaidia kuboresha miundombinu ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ili isaidie kwenye usafirishaji wa mizigo kwa maelezo kuwa reli hiyo imekaa muda mrefu.

"Asilimia zaidi ya 60 ya mizigo inayopitia bandari yetu ya Dar es salaam, inaenda Zambia, Kongo, Malawi na baadhi ya mazao ya ukanda huo wa SADC, sasa tumeomba watusaidie kuboresha miundombinu ya reli yetu na balozi amekubali," alisema Homera.

Alisema, wawekezaji hao watasaidia zaidi kwenye kilimo cha maparachichi na soya ambayo ni miongoni mwa mazao ambayo yanastawi vizuri mkoani humo.

Katibu Tawala Msaidizi Viwanda na Biashara wa Mkoa wa Mbeya, Mwajabu Nyamkomola alisema watahakikisha wanawasaidia wawekezaji hao kupata maeneo mazuri kwa ajili ya uwekezaji.

Alisisitiza kwamba, nchi ya China ni miongoni mwa mataifa duniani ambayo yana teknolojia za kiwango cha juu, hivyo akawataka wananchi kujiandaa kunufaika na teknolojia hizo.

Katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Serikali imeandaa mashamba yenye ukubwa wa zaidi ya hekta 1,000 kwa ajili ya kilimo cha soya ambazo zinaelezwa kuwa ina soko kubwa nchini China.



Mkuu wa Wilaya ya Ileje mkoani Songwe, Anna Gidalya (kulia), akisalimiana na Askofu wa Kanisa la Kilutheri la Afrika Mashariki (KKAM) Dayosisi ya Nyanda za Juu Kusini, Dk. Edward Mwaikali, katika ibada ya uzinduzi wa Parishi ya Mlowo wilayani Mbozi juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Viongozi wa dini watakiwa kukemea vitendo vya ukatili

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

VIONGOZI wa dini mkoani Songwe, wametakiwa kuisaidia serikali katika kukemea vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake katika mkoa huo.

Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Anna Gidalya alitoa ombi hilo juzi alipomwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, Waziri Kindamba kwenye uzinduzi wa Parishi ya Mlowo ya Kanisa la Kilutheri la Afrika Mashariki (KKAM) Dayosisi ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema, vitendo vya ukatili vimekuwa vikitokea na kwamba baadhi ya maeneo hata vitendo vya mauaji ambayo yanahusishwa na imani za kishirikina na mapenzi vimekithiri.

Alisema viongozi wa dini wanatakiwa kushirikiana na serikali kukemea vitendo hivyo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha watoto wanapata malezi bora ili waepuke ukatili huo.

Alisema, ili kukomesha vitendo hivyo ni lazima kila mtu kwenye jamii atimize wajibu wake na kwamba viongozi wa dini wana nafasi kubwa zaidi ya kuwajenga watu kiimani.

"Kwenye maeneo mengi ya mkoa wetu imani imeshuka sana, kuna matukio mengi ya ukatili dhidi ya watoto na wanawake pia, kuna mauaji ambayo ni ya ajabu ajabu, tujitahidi sana kukemea mambo haya," alisema Anna.

Askofu Mkuu wa Dayosisi hiyo, Dk. Edward Mwaikali aliahidi kushirikiana na Serikali kukemea maovu kwenye jamii kwa maelezo kuwa kazi hiyo ni miongoni mwa wajibu wa viongozi wa dini.

Alisema katika kanisa hilo huwa wanafanya maombi maalumu kila wiki kwa ajili ya kuwaombea watoto kwa ajili ya kuepuka mambo mbalimbali ambayo yanahatarisha ustawi wao.

Dk. Mwaikali, alisema wakati Serikali ikiendelea kutimiza wajibu wake wa kisheria na wao wataendelea kutekeleza wajibu wao wa kiroho ili baadhi ya mambo hayo yatatuliwe.

"Tukuahidi tu Mkuu wa Wilaya kwamba hilo jambo lipo ndani ya uwezo wetu na tutahakikisha tunashirikiana na serikali, tunaamini tukishirikiana vizuri tutafanikiwa sana," alisema Dk. Mwaikali.

Alisema wamekuwa wakisikia kila siku kupitia vyombo vya habari kwamba watoto wadogo wanabakwa na kunajisiwa kwenye maeneo mbalimbali jambo ambalo alisema huwa linawahuzunisha viongozi hao wa kiroho.

Hivyo, aliiomba serikali kuendelea kuchukua hatua kali za kisheria kwa watu wote ambao wanabainika kutekeleza vitendo hivyo vya kinyama na kwamba na wao wataendelea kuwa mabalozi wa kutoa elimu na kukemea.





## Biashara bodaboda sasa yarasimishwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MRATIBU wa Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), Dk. Seraphia Mgembe amesema wamefanikiwa kurasimisha biashara ya bodaboda mwaka huu.

Amesema, mpango huo umewezesha kundi hilo kutambulika rasmi kama zilivyo tasnia zingine na hatimaye kuondokana na migogoro ya mikataba kati yao na wamiliki wa vyombo hivyo.

Dk. Mgembe, alibainisha hayo jijini hapa juzi alipotoa mada kwenye semina kwa wabunge wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa (USEMI).

Alisema hatua ya kurasimisha biashara ya bodaboda ni mwendelezo wa uwezeshaji wananchi kiuchumi.

"MKURABITA umekuwa ukitekeleleza majukumu yake ya urasimishaji wa ardhi vijijini na kujenga masjala, urasimishaji ardhi mijini, kujenga vituo vya urasimishaji na urasimishaji wa biashara na kwa mwaka huu tumefikia kurasimisha biashara ya bodaboda," alisema.

Aliongeza kuwa katika kurasimisha biashara ya bodaboda, halmashauri sita zimefikiwa ikiwamo Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Halmashauri zingine ni Manispaa ya Moshi, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Halmashauri ya Rungwe na Halmashauri ya Tarime Mji.

Dk. Mgembe alisema kupitia mpango huo wa kurasimisha bodaboda, waendesha bodaboda 6,365 wamepata mafunzo huku vituo vya bodaboda vipatavyo 264 vimesajiliwa.

Alisema, leseni 3,014 zimetolewa huku serikali ikipata mapato ya Sh. milioni 30.14 kutokana na utolewaji wa leseni hizo.

Wadau wa urasimishaji biashara ya bodaboda ni halmashauri, LATRA, Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Mapato (TRA), taasisi za fedha na Umoja wa Waendesha Bodaboda.

Akizungumzia matokeo kwa wananchi yaliyotokana na urasimishaji wa biashara ya bodaboda, alisema waendesha bodaboda wamekopa zaidi ya Sh. milioni 880.

Serikali inatekeleza MKURABITA kwa lengo la kuwezesha wananchi kurasimisha rasilimali na biashara zao, kuwezesha upatikanaji wa mitaji na kuwawezesha watanzania wengi kushiriki katika fursa za kiuchumi.

# TANROADS yaagizwa ukarabati maeneo korofi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, ameagiza mameneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) kuhakikisha wanatoa kipaumbele kwa ajili ya kutengeneza maeneo korofi ya barabara na madaraja ili kuepuka kero za kutopitika msimu wa mvua.

Kasekenya, aliagiza hayo juzi jijini hapo wakati wa kikao kazi cha kujadili utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na wakala huo katika maeneo mbalimbali nchini.

"Miundombinu ya barabara ni kichocheo katika ukuzaji wa sekta nyingine, hivyo hakikisheni mnajenga na kukarabati maeneo yote korofi ili kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji," aliagiza.

Kasekenya pia, aliuagiza uongozi wa TANROADS kutoa elimu kwa wasafirishaji na wadau wote wanaotumia miundombinu ya barabara nchini kutomwaga mafuta, mchanga, mawe na kokoto ambavyo vinasababisha kuharibu miundombinu hiyo.

Mbali na hilo, naibu waziri huyo aliwataka mameneja hao kuendelea kuwa wabunifu, waadilifu na kusimamia kazi zao kwa ubora na kwa wakati ili kuleta matokeo chanya.

"Endeleeni kutumia utaalamu wenu katika ujenzi na usimamizi wa miradi ili kuwa na miundombinu bora itayokidhi mahitaji ya vizazi vya sasa na vijavyo," aliagiza.

Awali akimkaribisha mgeni rasmi, Katibu Mkuu anayesimamia sekta ya ujenzi, Balozi Aisha Amour, alisema lengo la kikao hicho ni kujadili na kushauri namna bora ya kutatua kero za watumiaji wa miundombinu ya barabara na kupeana mbinu mbalimbali za kutatua kero hizo.

Alizitaja baadhi ya kero hizo kuwa ni kuwapo matuta yasiyo na viwango, mashimo kwenye barabara na uwekaji wa alama usio sahihi mahali husika.

"Kikao hiki kinalenga zaidi katika kazi za matengenezo ya barabara, miradi ya maendeleo inayoendelea, usalama barabarani na matukio ya ajali, hivyo tumieni fursa hii kuleta mawazo chanya yatakayoikuza sekta," aliagiza.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Dar es Salaam, Haroun Senkuku alisema ofisi yake inatarajia kuongeza barabara tatu za juu ili kupunguza msongamano wa magari yanayoingia na kutoka katika jiji hilo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu, George Simbachawene, akizungumza na Mzee Michael Mnubi katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kijiji cha Wihenzele Jimbo la Kibwage Halmashauri ya Pwapwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC azipa mbinu taasisi za kifedha kupata wateja

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, ameziomba taasisi za kifedha nchini kuendelea kutoa misaada kwenye jamii inayozizunguka ili kutoa huduma kwa jamii hiyo.

Jabiri Shekimweri, alitoa rai hiyo juzi wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa wafanyabiashara na viongozi wa dini Mkoa wa Dodoma yaliyoandaliwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na Benki ya Kiislamu jijini hapa.

Shekimweri alizitaka taasisi za kifedha kuendelea kutoa misaada kwenye jamaii ili kujitangaza kwenye maeneo husika.

"Dunia ya leo inahitaji kujitangaza, wewe unaanzisha benki unabaki kuomba watu wafungue akaunti lakini hufiki kwenye maeneo yao," alifafanua.

Alibainisha kuwa misaada ya vitu mbalimbali inayotolewa kwenye jamii inasaidia kuwatangaza kwa wananchi wa maeneo mengi.

Alivitaja vitu ambavyo vinasaidia kuzitangaza taasisi hizo kwenye jamaii kuwa ni misaada ya madawati, mashuka, vifaa tiba vya hospitalini, ujenzi wa majengo ya shule na sekta ya afya. Aliongeza kuwa vitu vingine ni misaada wakati wa majanga yanayotokea katika jamii kama njaa, moto na mafuriko pamoja na kusaidia vituo vya watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Alisema, vifaa hivyo vilivyotolewa vinaweza kuandikwa jina la taasisi husika, hivyo inakuwa ni sehemu ya kujitangaza.

Mkuu wa wilaya huyo alisema kutokana na Mkoa wa Dodoma kuwa makao makuu ya nchi, kuna ongezeko la wageni wanaohamia, hivyo taasisi za kifedha zinatakiwa kufungua matawi mengi ili kuwahudumia watu hao.

Kaimu Mkurungenzi wa Huduma Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Badru Massoud alisema wameandaa mafunzo hayo kwa lengo la kutoa elimu ya huduma zinazotolewa na benki hiyo.

Alisema, mafunzo hayo yamewashirikisha watu binafsi, viongozi wa dini na wafanyabiashara pamoja na jumuiya mbalimbali.

Massoud alisema, mafunzo hayo yamekuwa endelevu na yanatolewa kwa awamu kwenye mikoa mbalimbali na mpaka sasa wana matawi 28.

Meneja wa PBZ na Benki ya Kiislamu Tawi la Mkoa wa Dodoma, Mohamed Massoud alisema tawi hilo lilifunguliwa miezi minne iliyopita.

Alisema kuwa tangu kufunguliwa kwa tawi hilo, wamefanikiwa kupata wateja zaidi ya 2,500 na lengo lao ni kuwafikia watu wengi zaidi katika mkoa huo.



**HABARI ZANZIBAR**

# Utupaji, utelekezaji wa watoto wamchefua waziri

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, amelaani vitendo vya kuwatupa watoto wachanga baada ya kuzaliwa na wale wanaotelekezwa na wazazi wao.

Alitoa kauli hiyo jana ofisini kwake Mwanakwerekwe Mjini Zanzibar baada ya kutokea tukio la kutupwa kwa kichanga.

Alisema, juzi majira ya mchana mtoto huyo alitupwa katika Mtaa wa Muungano Mjini Zanzibar, huku mwili wake ukiwa umeshambuliwa na wadudu.

Waziri Riziki alisema, mtoto huyo ambaye ni wa kiume aliokotwa akiwa hai baada ya kutupwa muda mchache baada ya kuzaliwa, alikutwa katika mfuko.

Hivyo, aliwataka wazazi ambao hawahitaji watoto pindi wanapojifungua ni vyema wakawapeleka serikalini kwa sababu serikali imetenga nyumba maalum ya kuwalea watoto hao.

"Haipendezi hata kidogo kuona watoto wanatupwa wakati watu wanawahitaji wanaenda hadi India na nchi zingine kuhangaika kupata kizazi, Leo Mungu amekubariki kupata mtoto lakini wewe unamtupa,"alisema.

Alivitaka vyombo vya sheria kuhakikisha wanamtafuta aliyefanya kitendo hicho na endapo akipatikana achukuliwe hatua za kisheria.

Waziri Riziki alisema, mtoto huyo kwa sasa anaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Mnazimmoja kwa ajili ya uangalizi maalum na hali yake inaendelea kuimarika.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mariyam Juma Sadala, alisema kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto namba 6 ya mwaka 2011 ni kosa la jinai kumtupa mtoto.

Alisema mtoto huyo alikuwa na uzito kwa kilo 1.8 na ni mtoto ambaye hajafikisha muda wa miezi tisa ya kukaa tumboni kwa mama yake.

Alisema kufuatia uongozi wa Shehia ya Muungano na maofisa wa ustawi wa jamii baada ya kichanga hicho kuokotwa alipelekwa polisi na kuwahishwa hospitali.

"Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto namba sita ya mwaka 2011 ni kosa la jinai kutupa vichanga na kifungu namba 3 cha sheria hiyo ni kosa la jinai na endapo mzazi atapatikana kuhusika na tukio hilo atafikishwa mahakamani na sheria kuchukua mkondo wake,"alisema.

Alisema, tangu mwaka 1964 Serikali ya Zanzibar inatoa huduma katika kuwahudumia watoto, kuhakikisha haki zao zinapatikana na kulelewa katika mazingira bora kwa sasabu mtoto ni taifa la baadae.

Alisema kuwa serikali imepokea maombi ya wazazi watano ambao wanaomba watoto kwa ajili ya kuwalea.

Alisema serikali inasimamia haki za watoto na inalea watoto 24 ambao wengine yatima na waliotupwa wakiwamo mapacha tisa ambao kila pacha watoto watatu, pia inasimamia malezi ya watoto 103 ambao wanaishi katika mazingira magumu.

Katibu Mkuu huyo alisema, tangu Juni hadi Septemba kuna kesi nyingi za watoto kukosa huduma kutoka kwa wazazi wao, kesi 103 za udhalilishaji na kesi 32 watoto wameingiliwa kinyume na maumbile.

Alisema ni jukumu la wazazi kuwalea watoto kwa pamoja ili kupata haki zao ikiwamo huduma, hifadhi na malezi bora.



Mwakilishi wa Jimbo la Mwera, Mihayo Juma Nhunga (kulia) na mwakilishi wa kuteuliwa na rais, Juma Ali Khatib, wakifuatilia kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yakanusha ofisa wake kuwa jasusi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imekanusha taarifa zilizoenea katika mitandao ya kijamii zinazomuhusisha Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi (ZIPA) kuwa ni jasusi.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi,Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema tuhuma hizo siyo za kweli na zimelenga kumchafua mtendaji huyo mwenye uzalendo.

Alisema tuhuma hizo zilizohusiana na mtendaji huyo kuwa na hati mbili za kusafirisha zinaonekana kuwapo kwa watendaji wasiokuwa waaminifu kuchezea mifumo ya nyaraka za serikali, hivyo uchunguzi unaendelea kufanyika ili kubaini aliyehusika kusambaza taarifa hizo.

Waziri Soraga, aliwaomba waandishi wa habari kuacha kuyatumia majukwaa ya habari kinyume na kazi yao, hivyo wazingatie miiko na maadili ya taaluma yao kwa kufanya uchunguzi wa jambo ili habari zao ziwe zimegusa pande zote mbili.

Mkurugenzi wa (ZIPA), Sharif Ali Sharif, aliitaka jamii na waandishi wa habari kufanya uchunguzi wa kina ili kujiridhisha na tuhuma hizo kabla ya kusambaza taarifa kwa lengo la kujua ukweli wa jambo hilo.

Alisema, wasambazaji wa taarifa hizo wameshindwa kufanya uchunguzi kwa sababu yeye hana hati mbili za kusafiria na hana uraia wa nchi nyingine zaidi ya Tanzania.

Alisema: "Mimi ninapacha mwezangu ambaye tumepishana dakika tano tu kuzaliwa na tumefanana sana yeye anaishi nchini Zcheek na ana urai wa nchi hiyo, hivyo wasambazaji wa taarifa hizo hawakufanya uchunguzi na kuzani kuwa ni yeye Mkurugenzi wa ZIPA".

## Sheria ya Uvuvi kufumuliwa itatue kero za wavuvi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010 itafanyiwa marekebisho kwa ajili ya kukabiliana na matatizo mbalimbali yanayowakabili wavuvi ikiwamo kuingia kwa sera ya uchumi wa buluu.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Suleiman Masoud Makame wakati akijibu hoja za Kamati ya Kilimo na Maliasili na Uvuvi ya Baraza la Wawakilishi ambao walichangia uchumi wa buluu.

Makame, alisema Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010 inahitaji marekebisho makubwa ili kwenda na mabadiliko yaliopo sasa ambayo yatawawezesha wavuvi kuingiza kipato kikubwa.

Alisema, kufuatia kuwapo kwa sera ya uchumi wa buluu mapitio ya Sheria ya Uvuvi inahitaji kupitiwa upya na kuzipatia kero zote zilizojitokeza ili kukabiliana na mabadiliko ya sera ya uvuvi.


Alisema, wizara ipo katika mchakato wa kutayarisha sera ya uchumi wa buluu ambayo itazingatia mahitaji muhimu ikiwamo kuweka muongozo wa kulinda mazingira ya baharini kwa ajili ya kupambana na uvuvi haramu.

"Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu ipo katika hatua za mwisho wa kupitia sera ya uchumi wa buluu ambayo miongoni mwa malengo yake ni kuona mazingira ya bahari yanalindwa na kupambana na mabadiliko ya tabia ya nchi katika maeneo ya baharini"alisema.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia hotuba hiyo waliitaka wizara kufanya mapitia ya Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010 kwa ajili ya kulinda mazingira ya baharini na kupambana na uvuvi haramu.

Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamad Omar alisema Sheria ya Uvuvi inahitaji marekebisho makubwa kuhakikisha rasilimali za baharini zinalindwa na kuweka aina ya uvuvi ambao utazingatia mazingira bora ikiwamo kulinda mazao ya baharini.

Alisema: "Matumbawe ya baharini ambayo ni mazalia ya samaki yapo katika tishio la kutoweka kutokana na uharibifu unaofanywa na wavuvi wanaofanya uvuvi haramu".





## J/Wazazi yapata mwenyekiti mpya

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

HAMISI Shikuba, ametangazwa mshindi nafasi ya mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Shinyanga Vijijini, baada ya kupata kura 425, dhidi ya mpinzani wake, Perepetua Masesa aliyepata kura 61.

Msimamizi wa uchaguzi huo, Bernard Shigela, alimtangaza Shikuba kuwa mshindi wa nafasi hiyo katika uchaguzi uliofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita.

Aidha, aliwatangaza Awadhi Aboud, kuwa mshindi wa nafasi ya mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Wazazi Taifa, Kashinje Komanya mjumbe Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya na Leticia Masalu mjumbe wa Mkutano Mkuu Wazazi Mkoa.

Shigela, aliwataja washindi wengine watatu kuwa wajumbe baraza la wazazi wilaya ambao ni Nyamizi Robert, Leonarld Waziri na Mathias Rugata huku aliyeshinda mjumbe wa mkutano mkuu CCM mkoa ni Mrisho Hamad huku Jilunguya Ngelya akishinda nafasi ya mjumbe wa UVCCM.

Mwenyekiti huyo mpya wa Jumuiya ya Wazazi, akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, aliomba ushirikiano na uhusiano mzuri katika kazi ili kuisukuma jumuiya hiyo mbele.

Katika uchaguzi huo, ushindani ulikuwa mkali na kusababisha kura za kumpata mwenyekiti kurudiwa mara ya pili.

Uchaguzi huo ulifanyika juzi kwenye Uwanja wa CCM Kambarage mjini Shinyanga, na kutokana na mshindi kutopata idadi ya kura zinazotakiwa ili kutangazwa mshindi ilibidi zirudiwe.

# Wanufaika wa TASAF wafundwa kuhusu ruzuku

**Na Restuta Damian,** MULEBA

BAADHI ya wanufaika mpango wa kunusuru kaya maskini unaoratibiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), awamu ya tatu katika kipindi cha pili Kata ya Gwanseli, Muleba mkoani Kagera, wameshauri wenzao kutumia ruzuku wanayopata kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Wakizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki iliyopita katika kijiji cha Katunguru, walisema ruzuku hiyo ikitumiwa vizuri itawasaidia walengwa kuondokana na umaskini.

Mmoja wa mnufaika hao, Majid Athuman alisema tangu mwaka 2015 alipoingia katika mradi huo, amepata manufaa ikiwamo kununua shamba na mifugo.

"Mimi nimeingia mwaka 2015 nilipata ajali ya pikipiki, lakini hadi sasa hivi kupitia hela ya TASAF nimepata shamba ekari moja, kuku 10 pamoja na mbuzi watano.

"Hata serikali ikisema ituache sisi na wengine wapate nipo tayari kabisa vitu ambavyo nimeanzisha vitanisaidia kuongeza vingine kidogo kidogo na wenzangu waige kujitegemea, hata mtoto ukimzaa si kwamba atakaa na wazazi milele," alisema Athuman.

Mnufaika mwingine, Raymond Titagekulwa, kutoka kijiji cha Bushozi, alisema ameboresha maisha yake kwa kupanua shamba lake kwa ajili ya kilimo.

Alisema, upanuzi wa makazi pamoja na shamba ilikuwa ndoto yake na kwamba kwa sasa imetimia kwa kuwa kilimo kitasaidia familia yake.

Titagekulwa alisema, mategemeo yake ni kuachia na wengine waingie katika mpango huo ili wajikwamue kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Mtendaji wa Kijiji cha Katunguru, Elizeus Simon, alisema tangu kuanza kutekelezwa kwa mpango huo mwaka 2015 hadi sasa, kaya 422 zenye watu 2,526 zimenufaika.

Alisema, katika idadi hiyo, wanawake ni 1,293 na wanaume 1,233 na kati ya hao wenye uwezo wa kufanya kazi za uzalishaji wanafikia 461.

Pia, alisema kuna mafanikio yaliyopatikana kutoka kwa walengwa ikiwamo ufugaji wa mbuzi na kuku ambazo zinawasaidia kujipatia kipato.

Katibu Tawala wa Mkoa Kagera, Toba Nguvilla, alisema lengo la serikali ni kupunguza umaskini kwa jamii ikiwamo kuzisaidia kaya maskini kupata chakula, huduma za afya na elimu.

Alisema, ziko kaya zinazosahau jukumu la ruzuku hiyo kama ni kuondoa umaskini, hivyo zinaamua kufanya matumizi yasiyotarajiwa na kusahau kujiendeleza kiuchumi.



Wachimbaji wadogo wakiwa kazini katika mgodi wa Nyamatagata Halmashauri ya Mji wa Geita. **PICHA: ALPHONCE KABILONDO**

# Halmashauri yapokea fedha umwagiliaji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Msalala, Kahama mkoani Shinyanga, imepokea Sh. bilioni 1.4 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha umwagiliaji katika kata ya Chela.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, aliyabainisha hayo jana katika hafla ya kukabidhi matrekta 21 kwa wakulima wa Kanda ya Ziwa kwa ufadhili wa Kampuni ya Uwezeshaji wa Zana za Kilimo (PASS Leasing), iliyofanyika katika eneo la maegesho la magari makubwa yaendayo Rwanda, Burundi, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Alisema, serikali kupitia Wizara ya Kilimo imekuwa ikitengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya wakulima ikiwamo kupunguza gharama za pembejeo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Mjema alisema, watabiri wa hali ya hewa wanadai kuwa katika msimu wa kilimo ujao kutakuwa na uhaba wa mvua na kuwataka wakulima kutunza chakula badala ya kuuza chote halafu wakapata njaa.

Aliwaagiza wakuu wa wilaya wote mkoani Shinyanga kusimamia agizo la kutouza chakula chote hususani mpunga ambao ni chakula kikuu kwa mkoani hapo.

Mwaka wa fedha 2022/23, alisema mkoa ulipokea Sh. bilioni 190 kwa ajili ya usambazaji wa maji, kilimo cha umwagiliaji na kutunza mazingira, hivyo sehemu zote hususani vijijini ambako kuna uhaba wa maji wananchi wake watanufaika.

"Maofisa ugani wetu hakikisheni mnawatembelea wakulima mara kwa mara na kutoa elimu ya kulima kisasa kulingana na hali ya maeneo yao ya kilimo, tunataka msimu ujao tuongeze uzalishaji nchi nzima kwa mazao yote kwa kutumia trekta na kituo cha kilimo Chela cha umwagiliaji," alisema Mjema.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, aliahidi kufanyia kazi agizo lililotolewa la kuzuia wananchi kutouza holela mazao yao.

Alisema, msimu wa kilimo uliopita wakulima wa pamba walizalisha kilo 800,000 tofauti na kipindi cha nyuma na msimu ujao makisio waliyoweka ni kuzalisha zaidi ya kilo milioni tano.

# Italia kuwa na waziri mkuu mwanamke

**MILAN,** ITALIA

MUUNGANO wa vyama vinavyoegemea mrengo wa kulia unaoongozwa na Chama cha Giorgia Meloni cha Brothers of Italy, unatarajiwa kushinda katika uchaguzi wa serikali mpya nchini Italia.

Kura za maoni zilionyesha kuwa muungano huo ulionekana kushinda na takribani asilimia 45 ya kura. Kura hizo zitatosha kuuwezesha muungano huo kuwa na wingi wa viti bungeni.

Matokeo yanayotarajiwa yanaashiria kupanda kwa kasi kwa chama cha mrengo wa kulia cha Meloni, ambacho kilipata asilimia 4 pekee ya kura katika uchaguzi uliopita. Chama cha Brothers of Italy sasa kinatarajiwa kushinda asilimia 22.5 hadi 26.5 ya kura.

Meloni anaweza kuwa waziri mkuu wa kwanza mwanamke wa Italia.

Idadi ya wapigakura ilikuwa inaelekea kuwa ya chini huku zaidi ya nusu ya watu wakipiga kura hadi saa nne kabla ya zoezi hilo kufungwa.

Uchaguzi huo mkuu wa ghafla ulichochewa na kujiuzulu mwezi Julai kwa waziri mkuu anayemaliza muda wake Mario Draghi. **DW**

# Ebola yazidi kusambaa Uganda

**KAMPALA** UGANDA

SERIKALI ya Uganda imesema kuwa watu 16 wameambukizwa virusi vya ugonjwa wa ebola, huku wengine 18 wakishukiwa kuwa na maambukizo ya virusi hivyo.

Kutokana na ongezeko hilo, imechochea hofu ya kuenea kwa mlipuko wa ugonjwa huo ambao chanjo yake bado haijapatikana.

Katika ujumbe kupitia mtandao wa twitter, Wizara ya Afya nchini humo, imethibitisha vifo vya watu wanne kutokana na ugonjwa huo huku wengine 17 walioshukiwa kuwa na ugonjwa huo pia wakifariki dunia.

Mlipuko huo sasa umeenea katika wilaya tatu zote zikiwa katikati mwa Uganda.

Ugonjwa wa ebola ulitangazwa wiki iliyopita kutokea katika wilaya ya Mubende nchini humo.

Maambukizi ya ugonjwa huo mara nyingi husababisha homa kali na kutokwa na damu ndani.
**DW**

# Zelensky awataka raia kutoroka maandamano yakizidi Russia

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amewahimiza raia wa Russia kutoroka zoezi la usajili wa wanajeshi wa akiba au kujisalimisha katika nchi yake kama chaguo lao la kwanza.

Akizungumza katika utaratibu wake wa kuzungumza na wananchi kila siku jioni, Zelensky alisema kama watu hawataki kuona ndugu zao wanauawa, basi ni muhimu kutoroka.

"Ninatangaza tena kuna njia ya kukabiliana na hili, usijisalimishe kwa usajili wa kihalifu. Toroka au jisalimishe kwa Ukraine mara ya kwanza," alisema Zelensky.

Aliongeza: "Warussia wengi wanajaribu kulinda maisha yao wenyewe, ndiyo vita hivi vya uhalifu vya Russia vitaisha".

Akijibu maandamano yaliyofanyika jana Dagestan, Zelensky alisema kuwa watu hao ambao wanapigania maisha yao na maisha ya watoto wao, na kuwataka wote kufanya hivyo.

"Kwa sababu ukija kumaliza maisha ya watoto wetu, hatutakuacha urejee ukiwa hai," alisisitiza kiongozi huyo.

Aidha, Zelensky aliahidi matibabu ya kibinadamu kwa wanajeshi wote wa Russia waliojisalimisha.

**MAANDAMANO YAONGEZEKA RUSSIA**

Watu katika eneo la Dagestan nchini Russia wamekabiliana na polisi katika maandamano ya kupinga hatua ya kusajili wanajeshi 300,000 wa akiba.

Zaidi ya watu 100 walikamatwa wakati wa maandamano katika mji mkuu wa mkoa wa Makhachkala, hayo ni kwa mujibu wa Taasisi ya OVD-Info, mfuatiliaji huru wa haki za binadamu nchini Russia.

Kundi hilo liliongeza kuwa lina wasiwasi na ripoti za kuzuiliwa kwa nguvu kwa watu kunakotokea katika eneo hilo.

Dagestan ni eneo lenye Waislamu wengi nchini Russia ambalo wakati mmoja lilijulikana kwa vurugu kali.

Uchambuzi wa hivi majuzi wa idhaa ya BBC ya Kirusi ulionyesha kuwa wanajeshi wasiopungua 301 kutoka Dagestan wamefariki, mara 10 zaidi ya Moscow.

Zaidi ya watu 2,000 wamekamatwa kwenye maandamano makubwa yaliyofanyika tangu Rais Vladimir Putin atangaze kuwakusanya wanajeshi wa akiba siku ya Jumatano.

Wakati maandamano makubwa yamefanyika katika miji mikubwa nchini Russia katika siku za hivi karibuni, zaidi ya watu 700 wakikamatwa kwa Jumamosi pekee.

Mamia ya video zilizochapishwa kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha waandamanaji wakikabiliana na polisi na maofisa wengine wa usalama huko Makhachkala, huku OVD-Info ikiripoti kuwa maofisa waliamua kutumia bunduki na virungu dhidi ya umati.

Katika video moja, mwanamume aliyezuiliwa na maofisa anampiga kichwa ofisa wa polisi, kabla ya kupigwa na wengine.

Video nyingine ilionyesha ofisa wa usalama akitoroka kutoka kundi kubwa la waandamanaji, ambao baadhi yao walijaribu kumkamata alipokuwa akikimbia.

**KENYA KUNUNUA MAFUTA RUSSIA**

Rais wa Kenya, William Ruto, ameiambia BBC kuwa yuko tayari kununua mafuta kutoka Russia.

Nchi kadhaa zimekataa kushirikiana na Russia tangu uvamizi wa Ukraine lakini Rais Ruto alisema anazingatia chaguzi zote zilizopo.

Kenya inakabiliwa na mzozo mkubwa wa kiuchumi, na kusababisha bei ya chakula na mafuta kupanda.

Licha ya kupanda kwa bei ya mafuta Ruto alitetea uamuzi wake wiki jana wa kufuta baadhi ya ruzuku za mafuta.

Alisema ruzuku hizo siyo endelevu na zinakabiliwa na unyanyasaji. **BBC**




Mgombea wa nafasi ya Waziri Mkuu wa Italia, Giorgia Meloni wa Chama cha Brothers of Italy akipiga kura. Meloni anaongoza katika matokeo ya jumla. **PICHA: AFP**

# Al Shabaab yalipua kambi Somalia

**Mogadishu,** SOMALIA

MWANAJESHI mmoja ameuawa na wengine sita kujeruhiwa wakati mshambuliaji wa kujitoa mhanga alipojilipua katika kambi ya jeshi Magharibi mwa mji mkuu wa Somalia wa Mogadishu.

Kulingana na Shirika la Habari la REUTERS, kundi la wanamgambo la al-Shabaab limedai kuhusika katika shambulizi hilo.

Aden Omar, ofisa wa jeshi katika kambi hiyo, aliliambia shirika hilo kwamba mlipuaji huyo alijifanya kama mwanajeshi wa kawaida na kujiunga na wengine walipokuwa wakiingia kwenye kambi hiyo ya kijeshi mapema juzi kabla ya kulipua kilipuzi alichokuwa nacho.

Kundi la al- Shabaab limedai kuwaua wanajeshi 32. Kituo cha redio cha Al Andalus kinachomilikiwa na kundi hilo la al-Shaabab, kimemnukuu msemaji wa operesheni za kijeshi wa kundi hilo Abu Musab akisema kuwa mlipuaji huo aliwauwa wanajeshi 32 na wengine zaidi ya 40 kujeruhiwa ndani ya kambi hiyo mjini Mogadishu. **DW**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE
NO. 128 OF 2022
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE
AUGUSTINO ABELI MAPUNDA of Ipagala within
Dodoma Region.
AND
IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR
LETTERS OF ADMINISTRATION BY
AVELINA VICTORIA MAPUNDA

**GENERAL CITATION**
(RULE 75 OF PROBATE RULES GN NO. 369 OF 163)

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 29 Day of 9,2022.
**Dated at Dodoma this 19TH day of August, 2022.**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JULIUS NDESANJO KESSY**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T. 875 ARM.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/368860/2022.**

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE
NO. 129 OF 2022
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE
MKAMA ANDREA NJARABI of VEYULA within
Dodoma Region.
AND
IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR
LETTERS OF ADMINISTRATION BY
DICKSON MKAMA ANDREA NJARABI

**GENERAL CITATION**
(RULE 75 OF PROBATE RULES GN NO. 369 OF 163)

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 29 Day of 9,2022.
**Dated at Dodoma this 20TH day of August, 2022.**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**EZEKIEL MUSA MSIKA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC.670 BRL.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/380898/2022.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MASHUGHULI SASINE MINJA**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T322CAT.**
Chasses Namba **RZH1254004437,** Engine Namba **2RZ3744**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
**Polisi Taafifa :**
**KIL/MOS/RB/376458/2022**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA SHINYANGA
RUFAA YA ARDHI NAMBA 95 YA 2021
(SHAURI LA MAOMBI ASILIA NAMBA 33 YA 2022
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA
YA SHINYANGA) JOHN STEPHAN
DHIDI YA
1. MAHONA NTIGA
2. MACHIYA NDANYA

**POPOTE ULIPO**
Wajibu rufaa katika shauri hili ndugu Mahona Ntiga na Machiya Ndanya mnajulishwa kwamba mnano tarehe 30/09/2022 saa 5;00 asubuhi shauri husika limepangwa kusikilizwa kwa rufaa dhidi yenu.
Hivyo mnaamriwa kuhudhuria siku hiyo nyinyi ama Wakili wenu bila ya kukosa na kama hamtahudhuria rufaa hiyo itasikilizwa na kutolewa uamuzi bila nyinyi kuwepo.
**Imetolewa kwa amri yangu na kupigwa chapa ya Mahakama hii leo Tarehe 21/09/2022**

NAIBU MSAJILI MAHAKAMA KUU SHINYANGA

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA SHINYANGA

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF
MOROGORO
FORM NO 58
DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO 99 OF 2022

In the Matter of the Estate of the Late:
REGINA ALOYCE KAJILA

BY 1. JAMES BAKINEGE MBALWE
**All persons** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above -named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 04 day of OCTOBER.........2022
**Dated at MOROGORO this 20 day of SEPTEMBER...2022**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA CHETI



**IRENE ALEX MTUI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne Chenye namba **CS 150134783** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kwa mtihani wa mwaka 2015 katika shule ya Sekondari ya Mazoezi Kleruu
Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.Taarifa ya polisi namba **IRI/IRI/RB/381490/2022**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

NGOMENI ENTERPRISES

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA NA NOTISI YA KULIPA DENI.

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na CRDB PLC makao makuu Dar es salaam, tunatoa notisi ya siku kumi na nne(14) tu ili uweze kulipa deni lote unalodaiwa Pamoja na gharama za Dalali. Kukaidi au kushindwa kulipa deni hilo tutauza dhamana uliyoweka kwa mnada wa hadhara kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini.

| S/N | JINA LA MTEJA | DHAMANA/MAHALI | TAREHE/MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | MARTIN DANIEL SELEMANI | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MWEMBEMSAFA KINGOLWIRA MANISPAA YA MOROGORO. | 11.10.2022, SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 2. | KENNEDY CHRISTOSIAN MATHEMU. | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO UKONGA MTAA WA MADAFU MANISPAA YA KINONDONI DAR ES SALAAM, | 25.10.2022, SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3. | ROBERT SHAO | PIKIPIKI REG NO. MC 817 CLA MC 308 CGJ, MC 427 CGJ | 20.10.2022. SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA.**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na 75% atalipia ndani ya siku 14.
3. Mnuniuzi atakayeshundwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu, hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki,kutwaa nyumba na gharama nyinginezo zitzkuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua dhamana hizo muda wowote isipokuwa usiku.

**MAWASILIANO:**
**CRDB BANK PLC HEAD QUARTER,**
**NGOMENI ENTERPRISES, DSM. SIMU**
**0719974916/0784252048**


OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuzi wa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# AKON, MICHAEL NA MPANGO WA VYUO AFRIKA



**NEW YORK, Marekani**

NYOTA wa muziki wa R&B, na Hip Hop wa nchini Marekani, Akon amesema yeye na Michael Jackson walikuwa wakijadili kuhusu mipango ya kufungua vyuo kadhaa vya muziki katika bara la Afrika.

Lakini, ndoto hizo zilisambaratika baada ya kifo cha Jackson aliyefariki mwaka 2009 ambaye alikuwa mfalme wa muziki wa Pop duniani.

Katika mahojiano yake na TMZ.com, Akon mwenye asili ya Senegal, ambaye jina lake halisi ni Aliaune Damala Badara Akon Thiam, amesema yeye na Michael walikuwa na wazo la kuanzisha vyuo hivyo ili kuvipaisha vipaji vya muziki kutoka Afrika.

Akon alisema, yeye na Michael walitaka kuwapa wanafunzi zana, miundombinu na ushauri wa tasnia hiyo ili kuboresha ujuzi.

"Mimi na MJ tulikuwa bado tunajadiliana na tulitaka kuvitambua vipaji vya Afrika. Kwani Afrika bado kuna vipaji vingi ambavyo havijagunduliwa.

"Cha kusikitisha ni kwamba, Michael alifariki mwaka 2009 kabla hatujaanzisha chuo chochote, lakini ni jambo ambalo bado nataka lifanyike katika siku zijazo," alisema Akon, ambaye ana uraia pacha wa Marekani alikozaliwa na Senegal ambako ni asili yake.

"Nina ufunuo wa kuvutia sana kuhusu Michael na watu hawapaswi kutilia shaka urithi wa MJ, nitahakikisha nakamilisha kile tulichopanga."

# KONDE MUSIC KUACHIA WASANII WAKE



MMILIKI wa lebo ya Konde Gang, Rajabu Abdul 'Harmonize', ametangaza kuwa kuna baadhi ya wasanii wake watahitimu katika lebo hiyo na hivyo watakuwa huru kwenda kujitafutia maisha sehemu nyingine.

Harmonize bila kuwataja majina wasanii hao, aliandika kupitia Insta Story yake kuwa kuna baadhi ya wasanii watahitimu na atawatangaza siku ambayo anasherehekea miaka minne ya lebo hiyo.

"Tarehe 10/10 KondeGang tunatimiza rasmi miaka minne. Sio rahisi asikuambie mtu, vipindi vya kucheka, kulia, kuteleza na kuamka yote tunamshukuru Mungu pamoja na wewe unayesoma umefanikisha kuifanya Kondegang kuwa lebo kubwa Afrika Mashariki asante sana.

"Lengo ni kujikwamua kama watoto wa kimasikini tunatarajia kufanya jambo kubwa, jambo kubwa katika siku hiyo kubwa kwetu ikiambatana na kuhitimu kwa baadhi ya memba kadhaa wa KondeMusic," aliandika Harmonize.



# ISHA MASHAUZI ATAFUTA MUME

**Na Mwandishi Wetu**

MKALI wa muziki wa taarabu na rhumba, Isha Mashauzi, amefunguka kuwa yupo tayari kuolewa tena kwa sasa.

Akizungumza na kituo kimoja cha redio, Isha alisema: "Ndoa ni rikizi na Mungu anapanga na hakuna mtu asiyetaka, hata mimi leo akitokea mume aje anioe," alisema huku akitaja namba zake kwa yule aliyekuwa tayari.

"Jimbo liko wazi, sijaolewa namkaribisha mwanaume yeyote" alisema Mashauzi.

"Nimewahi kuolewa mara mbili mume wangu wa kwanza nimezaa naye mtoto mmoja, na mume wangu wa pili hatukubahatika kupata naye mtoto.

"Waume zangu wote tulihitilafiana kila mmoja akaenda kutengeneza maisha yake. Sasa hivi niko mwenyewe natafuta mtu. Wanitafute, nahitaji nipate mtu atakayenienzi, atakayenipenda, sijali kuhusu muonekano wake, lakini tu awe na kipato cha kuweza kunisaidia na familia yangu. Nataka kweli sio kwamba natania, mimi ni mzuri wa kila kitu, wanitafute," alisisitiza Isha.

# AZAM FC KUITUMIA PRISONS KUWAWINDA WALIBYA CAF

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC umesema licha ya lengo lao kuu la kutafuta pointi katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Tanzania Prisons, lakini wataitumia vema mechi hiyo kama sehemu ya maandalizi ya michezo ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Akhdar ya Libya.

Azam FC watacheza dhidi ya Tanzania Prisons Septemba 30, mwaka huu, mchezo utakaopigwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya na baada ya hapo wataanza safari ya kuelekea jijini Benghazi, Libya kukabiliana na Al Akhdar ya nchini humo kati ya Oktoba 7-9 kabla ya marudiano Oktoba 15, mwaka huu katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Zakaria Thabiti 'Zaka Zakazi', alisema timu hiyo itasasafiri Alhamisi wiki hii kuelekea Mbeya, kukabiliana na Tanzania Prisons kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo huo.

Alisema wanatambua mechi hiyo ya ligi itakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kila timu imejiandaa vizuri na wao wanatumia mchezo huo pia kufanya maandalizi ya mechi ijayo ya kimataifa.

"Benchi la ufundi linaloongozwa na kocha wetu Denis (Lavagne), anaendelea kukinoa kikosi kuwa imara na tunaenda kutafuta pointi tatu za Tanzania Prisons na matokeo hayo yataongeza morali kuelekea mechi yetu ya kimataifa dhidi ya Al Akhdar," alisema Zaka Zakazi.

Al Akhdar inakutana na Azam FC baada ya kuitupa nje Al Ahli Khartoum ya Sudan kwa jumla ya mabao 3-0, wakishinda nyumbani 3-0 kabla ya kutoka suluhu ugenini.

Azam FC ni miongoni mwa timu 14 za Afrika zilizokwepa kuanzia raundi ya awali ya michuano hiyo kutokana na ubora, na ilipangwa kucheza na mshindi wa jumla wa mechi hiyo.




Meneja Masoko wa Kampuni ya 10Bet, George Abdulrahman (kulia) na mshindi wa Sh. milioni 49.8, Derick Mustafa aliyepatia mechi 14 kwenye ubashiri wa mechi, wakionyesha ishara ya ushindi baada ya hafla fupi ya makabidhiano ya hundi mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# *Shabiki Simba ashinda mil. 49/- za 10Bet*

**Na Mwandishi wetu**

SHABIKI wa klabu ya Simba na timu ya Manchester United, Derick Mustafa, ameshinda Sh. milioni 49.8 baada ya kubashiriki kwa usahihi mechi 14 za ligi mbalimbali za soka duniani kupitia 'mkeka' wa Kampuni ya 10Bet.

Mustafa ambaye ni mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam amesema haikuwa kazi rahisi kushinda kiasi kikubwa cha fedha kutokana na kupata ugumu katika baadhi ya mechi zilizokuwa zinachezwa.

Alisema mechi iliyompa wakati mgumu zaidi ilikuwa kati ya Manchester United na Sheriff Tiraspol zilizokuwa zinacheza mchezo wa Ligi ya Europa na Manchester United kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 ikiwa uwanja wa ugenini.

Kwa mujibu wa Mustafa, timu hizo zilikuwa na uwiano sawa na alikuwa na wasiwasi wa timu yake kutokana na matokeo ya nyuma ambayo hayakuwa mazuri.

"Nilitumia uzoefu wangu katika kutabiri mechi hiyo na baadaye kupatia ambapo Manchester United ilishinda mabao 2-0. Nilifurahi kwani mbali ya ushindi, nimeweza kupata fedha kwa kupitia 10Bet," alisema Mustafa.

Kuhusu matumizi ya fedha hizo, alisema atazitumia kuboresha biashara yake ndogo ya mtaji na kupanua mtandao wake wa masoko.

"Nitatumia fedha hizi kuanzisha na kuboresha miradi yangu mbalimbali ya ujasiriamali. Ni faraja kwangu kushinda kiasi hiki kikubwa cha fedha. Lazima nichanganue aina ya biashara ninayoenda kufanya, faida na changamoto zake kabla ya kuamua chochote," alisema.

Meneja Masoko wa 10Bet Tanzania, George Abdulrahman, alisema Mustafa anakuwa mshindi wa kwanza kujishindia mamilioni ya pesa kupitia kampuni yao.

Abdulrahman alisema 10BET ina bonasi kubwa zaidi barani Afrika yenye asilimia 1,000 ambayo inamwezesha mtu anayebashiri kushinda fedha nyingi zaidi kwenye ushindi wake.

"Mustafa alifanikiwa kuweka dau lake lililomwezesha kushinda Sh. milioni 49.8 kupitia 'bonus yetu ya 'multibet' ya asilimia 1,000, tunatoa rai kwa watu wenye umri kuanzia miaka 18, kubashiri na 10bet ili kuweza kushindia fedha nyingi kupitia mkeka mmoja na zaidi. Unachotakiwa kufanya ni kutembelea www.10bet.co.tz, au kupitia App yetu na USSD *149*00#, " alisema Abdulrahman.

# Simba Queens yaalikwa Ulaya

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Mabingwa wa Afrika Mashariki kwa Soka la Wanawake, Simba Queens, kimepata mwaliko kutoka nchi mbalimbali, Afrika na barani Ulaya kwa ajili ya kwenda kucheza mechi za kirafiki, ikiwa ni maandalizi ya kwenda kucheza fainali za Ligi ya Mabingwa nchini Morocco mwezi ujao, imeelezwa.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu, amesema wamealikwa nchi za Ghana, Ujerumani, Ureno na Hispania, hivyo ni lazima kati ya hizo waende nchi moja tu kwa ajili ya maandalizi ya fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa soka la wanawake.

"Tumeshaanza kujiandaa na Ligi ya Mabingwa Afrika, tumeshaanza mazoezi, kikosi kipo kambini, na hivi sasa ni lazima tupate mechi za kirafiki ili kujiweka sawa. Hivi ninavyosema tumeshapata mialiko hapa Afrika nchi ya Ghana na Ulaya nchi za Ujerumani, Ureno, na Hispania kwa ajili ya kwenda kucheza mechi za kirafiki za kimataifa kabla ya michuano hiyo, na kati ya sehemu zote hizo ni lazima twende sehemu moja tu.

"Tutakachofanya sasa ni kuangalia umbali wa sehemu na muda wa michuano, hali ya hewa na mazingira, hatuwezi kuipeleka timu sehemu yenye joto wakati tunakwenda kucheza michuano hiyo kwenye nchi yenye baridi, au kwenda kwenye baridi wakati ligi inachezwa sehemu ya joto. Vitu vyote hivi tutakaa na kuviangalia, tutakuja na tamko twenda nchi gani ambayo itakuwa na mazingira mazuri, ukaribu wa kurejea kwenda kwenye nchi ambako michuano inafanyika na inayofanana hali ya hewa kwa kipindi hicho," alisema Mangungu.

Alisema Simba itakuwa ndiyo timu ya kwanza Tanzania kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika kwa upande wa wanawake, michuano hiyo ikiwa ni ya pili tangu ianzishwe.

Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake inatarajiwa kucheza nchini Morocco kuanzia Oktoba 30, mwaka huu na Simba ambao ni Mabingwa wa Ukanda wa CECAFA, watakuwa Kundi A pamoja na timu za Asfar ya Morocco, Green Buffaloes ya Zambia na Determine Girls ya Liberia.

Kundi B linaundwa na timu za Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, Bayelsa Queens ya Nigeria, Wadi Degla ya Misri na TP Mazembe ya DR Congo.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

**LUKAKU HARUDI CHELSEA**
MCHEZAJI wa kimataifa wa Ubelgiji, Romelu Lukaku hana mpango wa kurejea Chelsea atakapokamilisha mkopo wake wa msimu mzima pale Inter Milan. Klabu hiyo ya Italia inatarajiwa kuongeza muda wa mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. (***La Gazzetta dello Sport, via Football Italia***)

**TROSSARD KUMFUATA POTTER**
MSHAMBULIAJI wa Brighton na Ubelgiji, Leandro Trossard mwenye umri wa miaka 27, amesema yuko tayari kumfuata kocha wake wa zamani, Graham Potter kule Chelsea, lakini angetaka kucheza na si kukaa benchi. (***Het Nieuwsblad, via Mail***)

**FODE SAFI MAN CITY**
MACHESTER City wamefikia makubaliano kimsingi juu ya mkataba mpya wa mshambuliaji wa England, Phil Foden, na mkataba huo unaaminika kuwa wa zaidi ya miaka sita na utamfanya alipwe pauni 250,000 kwa wiki. (***Football Insider***)

**VAN DIJK AMKUBALI TIMBER**
MLINZI wa Liverpool, Vigil van Dijk mwenye umri wa miaka 31, anaamini beki mwenzake, Mholanzi Jurrien Timber, ambaye alihusishwa na uhamisho wa kwenda Manchester United msimu wa majira ya joto, anaimarika zaidi katika uchezaji wake kuliko yeye wakati akiwa na umri kama huo wa miaka 21. (***Manchester Evening News***)

**MARTINEZ AFUNGUKA AJAX**
MLINZI wa Argentina, Lisandro Martinez mwenye umri wa miaka 24, amesema hakuzingatia kukosolewa kwake wakati wa maandalizi ya mwanzo wa msimu baada ya kuhamia Manchester United msimu wa majira ya joto kutoka Ajax. (TyC Sports, via Metro)

**GOSENS ATAKIWA LEICESTER**
KLABU ya Leicester City inaweza kuchukua hatua kujaribu kumsajili mchezaji wa kimataifa wa Ujerumani, Robin Gosens mwenye umri wa miaka 28, ambaye anaweza kucheza katika safu ya ulinzi au kiungo wa kushoto, kutoka Inter Milan, Januari. (***FC Inter News***)

**MATIC KUJIFUNGA ROMA**
KIUNGO wa kati wa Serbia, Nemanja Matic, ambaye alijiunga na AS Roma majira ya joto baada ya mkataba wake na Manchester United kumalizika, yuko mbioni kuongeza mpya katika klabu hiyo ya Serie A. (***La Gazzetta dello Sport, Football Italia***)

**KAMARA KUUZWA JANUARI**
KLABU ya Rangers iko tayari kumuuza kiungo wa kati wa Finland mwenye umri wa miaka 26, Glen Kamara katika dirisha la uhamisho la Januari. (***Football Insider***)

**PICKFORD KUMRITHI DE GEA**
MANCHESTER United inamuwania golikipa wa England na Everton, Jordan Pickford mwenye umri wa miaka 28, kama mrithi wa David de Gea mwenye umri wa miaka 31 raia wa Hispania. (***Metro***)

**JUVE NA OFA KWA GRIEZMNANN**
JUVENTUS inajiandaa kutoa ofa kwa fowadi Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 31, kama Atletico Madrid hawatamsajili moja kwa moja kutoka Barcelona. (***Gazzetta dello Sport, via Mail***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# DESCHAMPS AMTAKA KOCHA PSG KUMPUMZISHA MBAPPE

### ●●● Lengo ni kumpa nguvu kuelekea Kombe la Dunia, asema ili...

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps, amemwomba Kocha wa Paris Saint-Germain, Christophe Galtier, kumpumzisha Kylian Mbappe, kwa ajili ya Kombe la Dunia litakaloanza mwishoni mwa Novemba mwaka huu.

Msimu huu wa soka kwa ngazi ya klabu utasimama katika kipindi chote cha Novemba na Desemba ili kupisha Kombe la Dunia litakalofanyika nchini Qatar, lakini makocha wana wasiwasi kuhusu upatikanaji wa wachezaji waliofiti kutokana na ratiba za mechi za ligi.

Mbappe, tayari amefunga mabao 10 katika mechi tisa msimu huu na amekosa mechi moja pekee ya ligi hadi sasa.

Huku pia, akiichezea Ufaransa katika kila mechi mbili za mwisho za hatua ya makundi ya Ligi ya Mataifa ya Uefa.

**Akizungumza na Kituo cha Televisheni cha Telefoot cha nchini Ufaransa, Deschamps alionyesha wazi kuhusu wasiwasi wake kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23.**

"Najua (Galtier) bado anataka kumchezesha Kylian. Lakini si mara kwa mara, anatakiwa kupewa nafasi ya kupumua kidogo," alisema Deschamps.

PSG, wakiwa wameanza vizuri zaidi msimu wa ligi, Mbappe ameonyesha kiwango bora chini ya kocha mpya Galtier, pia ni vigumu kufikiria kwamba anaweza kupumzishwa.

Mfaransa huyo alicheza kwa dakika zote 90 katika mechi zote mbili za PSG za hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

PSG imekuwa na shinikizo kubwa kwenye mashindano hayo ya Ulaya, baada ya kushindwa kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu kupanda kwao kwa umaarufu wa soka katika kipindi cha muongo mmoja uliopita.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,034,9

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 27, 28 NA 29 SEPTEMBA 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 27/09/22 | 21:45 | Portugal vs Spain | 2.28 | 3.22 | 3.12 |
| 02. 27/09/22 | 21:45 | Ukraine vs Scotland | 2.47 | 3.28 | 2.77 |
| 03. 28/09/22 | 01:00 | CA Atlanta vs Chaco For Ever | 2.80 | 2.85 | 2.55 |
| 04. 28/09/22 | 01:05 | Raya2 Expansion vs M. Zacatecas | 2.43 | 3.14 | 2.70 |
| 05. 28/09/22 | 05:00 | Mexico vs Colombia | 2.70 | 3.21 | 2.65 |
| 06. 28/09/22 | 18:00 | Inter Turku vs Haka | 2.22 | 3.41 | 3.11 |
| 07. 29/09/22 | 01:00 | Coritiba vs Ceara CE | 2.40 | 3.00 | 2.85 |
| 08. 29/09/22 | 01:00 | Club Celaya vs F Atlante | 2.26 | 3.04 | 3.04 |
| 09. 29/09/22 | 03:00 | Cuiaba MT vs America Mineiro MG | 2.24 | 2.90 | 3.24 |
| 10. 29/09/22 | 03:45 | Goias vs Botafogo RJ | 2.46 | 3.10 | 2.70 |
| 11. 29/09/22 | 03:45 | Atletico Mineiro vs Palmeiras | 2.27 | 3.18 | 3.23 |
| 12. 29/09/22 | 18:00 | Honka vs HJK Helsinki | 2.72 | 3.05 | 2.47 |
| 13. 29/09/22 | 21:30 | Barracas Central vs Gimnasia y Esgrima | 2.85 | 3.15 | 2.42 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa airtel money ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MAN CITY YAMPA MKATABA MNONO FODEN




**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City na Phil Foden wamefikia makubaliano ya kimsingi juu ya kuongezwa mkataba mpya wa thamani ya pauni milioni 78, kwa mujibu wa Football Insider.

Foden, amekuwa na kiwango cha kuvutia tangu alipoingia kwenye kikosi cha kwanza cha Man City na mabingwa hao wa Ligi Kuu England wana nia ya kumzawadia mkataba mpya.

Kiungo huyo wa kati wa England, mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2024, lakini City wanataka kubaki na mchezaji huyo kwa muda mrefu zaidi.

Mkataba huo wa fedha nyingi utamfanya alipwe mshahara wa takriban pauni 250,000 kwa wiki kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, na hivyo kumsogeza karibu na Kevin De Bruyne na Erling Haaland ambao ndio wanalipwa mishahara mikubwa klabuni hapo.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mkataba huo mpya utakuwa ni wa muda wa miaka sita kwa nyota huyo mzaliwa wa Stockport, ambaye alipitia akademi ya Man City.

Kocha wa City, Pep Guardiola ni shabiki mkubwa wa mchezaji huyo na amekuwa na nia ya kutaka kufanya naye kazi kwa muda mrefu.

Ripoti hiyo imesema kwamba, wakati wowote Foden, atasaini mkataba huo mpya na kikosi hicho chenye maskani yake pale kwenye dimba la Etihad.

# Kane ataka wahukumiwe baada ya Kombe la Dunia

**LONDON, England**

HARRY Kane amesema anaelewa kufadhaika kwa mashabiki wa England kutokana na mwenendo mbaya wa timu, lakini amewataka watunze kwanza maneno yao hadi Kombe la Dunia litakapomalizika ili waweze kuwahukumu.

Kipigo cha 'Simba Watu' hao kutoka kwa Italia mwishoni mwa wiki kilithibitisha kuteremka daraja kutoka kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa A, na kuwaacha bila ushindi katika mechi tano kabla ya kwenda kwenye michuano ya Kombe la Dunia nchini Qatar.

England, imetajwa kuwa mojawapo ya timu inayopewa nafasi kubwa ya kutwaa taji hilo baada ya kufanya vizuri katika michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018 na Euro 2020, lakini



kushuka kwao kiwango hivi karibuni kumewashitua mashabiki.

"Naelewa kufadhaika kwa mashabiki," alisema Kane akinukuliwa na BBC Sport.

"Nilikuwa shabiki wa England na bado ni shabiki wa England hata kama ninacheza au la. Kwa hivyo ninaelewa. Lakini hatimaye tutahukumiwa kwa kile kitakachotokea Novemba.

"Ikiwa tutakuwa na michuano yenye mafanikio, sina uhakika kama watu watakuwa na wasiwasi kuhusu uchezaji ambao tumekuwa nao wakati wa majira ya joto - na hilo ndilo jambo la msingi. Tunahitaji kuimarika. Tunajua hilo.

"Kila mtu atafurahia Kombe la Dunia, bila kujali kitakachotokea. Tunatumaini tunaweza kuwalipa kwa matokeo mazuri."

Kane mwenyewe amekuwa na wakati mgumu kwenye mechi za kimataifa akifunga mara moja tu kwa penalti katika mechi zake sita zilizopita.

## HABARI MICHEZO

# 905,195/-


# TOYOTA IST MPYA KUTOLEWA SUPA JACKPOT JUMAMOSI

**Na Thobias Mwanakatwe, Mbulu**

KUELEKEA droo kubwa ya gari aina ya Toyota IST itakayochezeshwa Jumamosi wiki hii, Fundi Uashi mkazi wa Hydom Wilaya ya Mbulu Mkoa wa Manyara, John Maho Tsii (37), amejishindia Sh. milioni mbili na runinga ya nchi 32 baada ya kuibuka mshindi katika mchezo wa SUPA Jackpot unaochezeshwa na Radio One.

Akizungumza na gazeti hili jana mjini Hydom wakati akikabidhiwa zawadi zake, Tsii alisema, alitangazwa mshindi Septemba 17, mwaka huu kwa kupigiwa simu saa 5:00 usiku na Radio One.

Tsii alisema, hadi kuibuka mshindi ameshacheza mara 48 na kwamba kila siku alikuwa akicheza kwa Sh.1,000 bila kukata tamaa ingawa familia yake ilikuwa ikimlalamikia kwamba anapoteza pesa kwa kucheza mchezo huo.




Mshindi wa mchezo wa SUPA JACKPOT unaochezwa na Radio One, John Maho Tsii, mkazi wa Hydom wilayani Mbulu, Manyara, akikabidhiwa zawadi ya Smart TV aina ya Hisense na hati ya makabidhiano ya mchezo huo kutoka kwa mwakilishi wa ITV/Radio One, Elisante Mkumbo kwa niaba ya Radio One. Makabidhiano hayo yalifanyika jana wilayani humo. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

Alisema, fedha alizopata zitamsaidia kumalizia ujenzi wa nyumba yake iliyopo eneo la Uwanja wa Ndege Hydom na kuwataka wananchi wengine kucheza mchezo wa SUPA Jackpot kwani hauna upendeleo mtu yeyote anaweza kushinda.

"Natoa wito kwa watu wengine wacheze mchezo wa SUPA kwani hauna upendeleo fikiria mimi nipo kijijini na nimeweza kushinda kwa hiyo huu mchezo ni mzuri sana," alisema.

Mchezo huo ambao ulianza mwanzoni mwa mwezi huu, utafikia tamati Jumamosi wiki hii kwa kuchezeshwa droo kubwa na mshindi kuibuka na gari aina ya Toyota IST mpya.

Namna ya kushiriki ni kwa kutumia mitandao yote ya simu, unakwenda sehemu ya lipa bili kisha unaingiza namba ya kampuni ambayo ni 222223 baada ya hapo utaulizwa kumbukumbu namba, hivyo utaingiza 111 au neno SUPA, hapo utakuwa umeshiriki na kujiweka katika nafasi nzuri ya kujishindia ndinga mpya Jumamosi pamoja na zawadi nyingine.

## Mgunda: Naanza na Dodoma Jiji

INATOKA UK. 32

matokeo ya jumla itafuzu moja kwa moja hatua ya makundi ya michuano hiyo itakayopoteza itaangukia mechi za mchujo Kombe la Shirikisho Afrika ili kuwania kushiriki hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Msimu uliopita katika hatua kama hiyo, Simba ilianzia ugenini dhidi ya Jwaneng Galaxy FC ya Botswana na kushinda mabao 2-0, na katika mechi ya marudiano ikajikuta ikifanya makosa na kupigwa 3-1 nyumbani hivyo kutolewa kwa faida ya bao la ugenini na kuangukia Kombe la Shirikisho.

# Mayele, Fei Toto wampa jeuri Nabi

INATOKA UK. 32

pungufu ya kikosi cha timu hiyo.

Kocha huyo alisema kurejea kwa Fei Toto na nyota wengine akiwamo Mayele ambaye baada ya kutoka kuuguza majeraha, juzi alicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Air Force ya Ligi Daraja la Pili na kutupia mabao mawili katika ushindi wa 4-0 walioupata.

Nabi alisema mchezo huo wa kirafiki unamsaidia kufanya vizuri na kuona ubora na mapungufu yao kabla ya kukutana na Ruvu Shooting kwenye Ligi Kuu.

Yanga itakabiliana na Ruvu Shooting, Oktoba 3, mwaka huu katika mchezo wa raundi ya tano wa ligi hiyo na siku sita baadaye itaikaribisha Al Hilal katika mchezo wa kwanza wa raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga ilitinga katika raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu baada ya kuibuka na ushindi wa jumla wa mabao 9-0 dhidi ya Zalan FC ya Sudan Kusini, ambapo mechi ya kwanza ilishinda 4-0 na ya pili 5-0, zote zikipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kutokana na hali ya usalama nchini Sudan Kusini kutokuwa shwari.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/10/22 | 17:00 | Coventry vs Middlesbrough | 2.70 | 3.30 | 2.55 |
| 02. 01/10/22 | 17:00 | Fulham vs Newcastle | 3.04 | 3.39 | 2.27 |
| 03. 01/10/22 | 17:00 | Rotherham vs Wigan | 2.33 | 3.19 | 3.09 |
| 04. 01/10/22 | 17:15 | Getafe vs Valladolid | 2.44 | 3.03 | 3.08 |
| 05. 01/10/22 | 18:00 | Strasbourg vs Rennes | 2.92 | 3.36 | 2.32 |
| 06. 01/10/22 | 19:30 | Sevilla FC vs Atletico Madrid | 2.84 | 3.14 | 2.54 |
| 07. 01/10/22 | 19:30 | Werder Bremen vs Borussia Monchengladbach | 2.58 | 3.57 | 2.48 |
| 08. 02/10/22 | 14:00 | Lorient vs Lille | 2.92 | 3.42 | 2.30 |
| 09. 02/10/22 | 14:00 | Stoke City vs Watford | 2.38 | 3.18 | 3.03 |
| 10. 02/10/22 | 15:00 | Espanyol vs Valencia | 2.73 | 3.22 | 2.58 |
| 11. 02/10/22 | 16:00 | AJ Auxerre vs Brest | 2.67 | 3.36 | 2.52 |
| 12. 02/10/22 | 16:00 | Troyes vs Reims | 2.47 | 3.36 | 2.72 |
| 13. 02/10/22 | 16:00 | Sampdoria vs AC Monza Brianz | 2.31 | 3.29 | 3.04 |
| 14. 02/10/22 | 16:30 | Hertha BSC vs Hoffenheim | 2.97 | 3.56 | 2.21 |
| 15. 02/10/22 | 17:15 | Celta Vigo vs Betis | 2.45 | 3.29 | 2.84 |
| 16. 02/10/22 | 18:30 | Leeds vs Aston Villa | 2.59 | 3.43 | 2.59 |
| 17. 02/10/22 | 19:30 | Girona vs Real Sociedad | 3.19 | 3.14 | 2.31 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE- 27/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3219 | Dong Tam Long AN vs Phu Tho FC | 1.50 | 3.53 | 6.67 |
| 14:00 | 5168 | South Korea vs Cameroon | 1.56 | 4.08 | 5.72 |
| 14:30 | 2376 | CSC Dumbravita vs FC Politehnica Iasi | 2.85 | 3.19 | 2.30 |
| 15:00 | 1644 | Bristol City U23 vs Swansea U23 | 1.56 | 4.20 | 4.50 |
| 15:00 | 1703 | Estonia U19 vs Bosnia & Herzegovina U19 | 4.81 | 4.03 | 1.55 |
| 15:00 | 1769 | Denmark U19 vs England U19 | 2.95 | 3.34 | 2.17 |
| 15:00 | 2716 | Poland U19 vs Italy U19 | 3.39 | 3.49 | 1.93 |
| 15:00 | 3557 | Vietnam vs India | 1.45 | 4.60 | 6.54 |
| 16:00 | 1693 | Indonesia vs Curacao | 2.70 | 3.50 | 2.38 |
| 16:00 | 2975 | Ittihad AL Ramtha vs AL Tora | 2.05 | 3.14 | 3.39 |
| 16:00 | 5434 | Ripensia Timisoara vs U Craiova SA | 4.80 | 3.87 | 1.58 |
| 16:00 | 5489 | BFC Daugavpils vs Rigas Futbola Skola | 8.27 | 4.92 | 1.29 |
| 16:30 | 5867 | CS Soimii Lipova vs Gloria Buzau | 5.29 | 3.62 | 1.58 |
| 17:00 | 1112 | Luxembourg U19 vs Azerbaijan U19 | 1.60 | 3.93 | 4.52 |
| 17:00 | 1745 | Armenia U19 vs Belarus U19 | 5.49 | 4.21 | 1.47 |
| 17:00 | 2022 | Bulgaria U19 vs Turkey U19 | 2.70 | 3.34 | 2.32 |
| 17:00 | 2288 | Watford U23 vs Charlton U23 | 2.94 | 3.87 | 1.99 |
| 17:00 | 2709 | Belgium U19 vs Spain U19 | 2.45 | 3.34 | 2.55 |
| 17:00 | 3282 | DAR AL Dawa vs Al Ahli Amman | 4.13 | 3.39 | 1.78 |
| 18:00 | 1474 | Romania U19 vs Austria U19 | 2.75 | 3.35 | 2.28 |
| 18:00 | 2787 | Lithuania U19 vs Latvia U19 | 4.12 | 3.73 | 1.70 |
| 18:30 | 3368 | Ukraine U21 vs Slovakia U21 | 1.93 | 3.49 | 3.39 |
| 18:45 | 5929 | CSA Steaua Bucuresti vs Chindia Targoviste | 2.65 | 3.19 | 2.45 |
| 19:00 | 1457 | Czech Republic U21 vs Iceland U21 | 1.77 | 3.55 | 3.94 |
| 19:00 | 2563 | Denmark U21 vs Croatia U21 | 2.12 | 3.39 | 3.00 |
| 19:00 | 5250 | Canada vs Uruguay | 4.09 | 3.53 | 1.88 |
| 19:30 | 1047 | Greece U19 vs Czech Republic U19 | 2.60 | 3.34 | 2.40 |
| 20:00 | 3763 | Hungary U19 vs Ireland U19 | 2.44 | 3.53 | 2.45 |
| 20:00 | 3827 | Chile vs Qatar | 2.05 | 3.47 | 3.52 |
| 20:15 | 5248 | Israel U21 vs Ireland U21 | 2.13 | 3.25 | 3.10 |
| 21:00 | 4028 | Ivory Coast vs Guinea | 1.74 | 3.56 | 4.89 |
| 21:00 | 4885 | Saudi Arabia vs USA | 3.72 | 3.47 | 1.99 |
| 21:30 | 4528 | Brazil vs Tunisia | 1.19 | 6.54 | 14.30 |
| 21:45 | 1099 | Sweden vs Slovenia | 1.75 | 3.59 | 4.55 |
| 21:45 | 1453 | Greece vs Northern Ireland | 2.01 | 3.18 | 3.88 |
| 21:45 | 2273 | Norway vs Serbia | 2.25 | 3.33 | 3.08 |
| 21:45 | 2706 | Ukraine vs Scotland | 2.42 | 3.24 | 2.88 |
| 21:45 | 2718 | Grimsby vs Carlisle | 2.07 | 3.05 | 3.70 |
| 21:45 | 3318 | Braintree vs St.Albans | 2.31 | 3.38 | 2.69 |
| 21:45 | 3378 | Albania vs Iceland | 1.98 | 3.33 | 3.78 |
| 21:45 | 3434 | Plymouth Parkway vs Salisbury City | 3.04 | 3.34 | 2.12 |
| 21:45 | 3525 | Kosovo vs Cyprus | 1.60 | 3.74 | 5.66 |
| 21:45 | 4122 | Farsley Celtic vs Boston Utd | 2.61 | 3.30 | 2.42 |
| 21:45 | 4720 | Portugal vs Spain | 2.29 | 3.18 | 3.13 |
| 21:45 | 4934 | Oxford City vs Ebbsfleet | 4.20 | 3.75 | 1.73 |
| 21:45 | 5601 | Switzerland vs Czech Republic | 1.66 | 3.63 | 5.25 |
| 21:45 | 5751 | Ireland vs Armenia | 1.36 | 4.45 | 8.90 |
| 21:45 | 5990 | Gainsborough vs Guiseley | 2.05 | 3.40 | 3.15 |
| 23:00 | 1533 | Universitario Popayan vs FC Aguablanca | 2.72 | 2.96 | 2.53 |
| 23:00 | 2522 | AD Grecia vs CS Herediano | 3.09 | 3.24 | 2.14 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Septemba 27, 2022

Nipashe


UKURASA 30



## Man City yampa mkataba mnono Foden

# MAYELE, FEI TOTO WAMPA JEURI NABI

●●●Arejea na kutupia wakishinda 4-0 mechi ya kirafiki, kocha ataka tena moja kabla...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema kurejea kwa nyota wake waliokuwa majeruhi kutamsaidia katika upangaji wa kikosi chake kuelekea katika mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal ya Sudan.

Majeruhi waliorejea uwanjani ni kiungo wao tegemeo, Feisal Salum 'Fei Toto', aliyekuwa akisumbuliwa na nyama za paja baada ya kuumia kwenye mchezo wa marudiano wa raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zalan FC uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Septemba 17, mwaka huu na Yanga kuibuka na ushindi wa mabao 5-0.

Majeraha hayo yalimfanya mchezaji huyo kujiondoa katika kikosi cha timu ya Taifa 'Taifa Stars' kwa ajili ya mechi mbili za kirafiki huko Libya zilizopo kwenye Kalenda ya Fifa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema Fei Toto, amejiunga na kikosi kwa ajili ya kuendelea na programu za maandalizi ya mechi zinazofuata za timu hiyo dhidi ya Ruvu Shooting kwenye Ligi Kuu na kisha Al Hilal, Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema kikosi kinaendelea vema na mazoezi yake kambini Avic Town Kigamboni na wachezaji wote ambao walikuwa majeruhi wapo fiti na wameungana na timu kwa ajili ya maandalizi ya mechi hizo.

"Fiston Mayele na Khalid Aucho walipata majeraha madogo baada ya kupatiwa matibabu walishaungana na kikosi na mchezaji mwingine ambaye alikuwa majeruhi ni Feisal Salum, naye ataanza mazoezi ya pamoja na wenzake leo (jana), baada ya kupona majeraha yake ambayo yalimfanya ashindwe kusafiri na timu ya taifa," alisema Nabi.

Alisema kutokana na kundi kubwa la wachezaji kupata fursa ya kuitwa katika timu za taifa kwa ajili ya mechi za kimataifa za kirafiki, wamelazimika kujikita zaidi katika mazoezi ya kujenga stamina kwa wachezaji waliopo ingawa wanafanya pia yale ya mbinu.

"Tuna wachezaji kama 10 hivi wapo katika majukumu ya timu za taifa, tunalazimika kuendelea na mazoezi na hawa waliopo tukingoja waungane na wenzao japo muda uliopo hadi mechi zilizopo mbele yetu ni mfupi," alisema kocha huyo.

Kuhusu mechi za kirafiki, alisema wako kwenye mpango wa kucheza moja kabla ya kukabiliana na Ruvu Shooting, na hautakuwa wa wazi kwa sababu ya kufanyia kazi ma-

INAENDELEA UK. 31



Fei Toto

## Mgunda: Naanza na Dodoma Jiji FC

**Na Hadija Mngwai**

WAKATI akitarajia kukiongoza tena kikosi chake kucheza mechi ya kirafiki kesho dhidi ya Kipanga FC ya Zanzibar, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda amesema kwa sasa mtazamo wake ni kuhakikisha anafanya vizuri katika mechi yake dhidi ya Dodoma Jiji Jumapili kisha kuigeukia Primeiro de Agosto ya Angola.

Simba ipo visiwani Zanzibar kucheza michezo miwili ya kirafiki ambapo tayari imeshacheza na Malindi SC na kushinda bao 1-0 katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Amaan juzi huku ikitarajia kushuka tena dimbani hapo kesho dhidi ya Kipanga ambayo nayo inajiandaa na mechi ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Club Africain ya Tunisia.

Akizungumza na Nipashe jana, Mugunda alisema anafanya maandalizi kwa hatua na utaratibu wa hali ya juu ili aweze kufanikiwa kufanya vizuri kwenye mechi za Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Natumia mechi hii ya kirafiki kuangalia mapungufu na mazuri ndani ya kikosi ili niweze kufanyia maboresho mapungufu niliyoyaona na kuboresha yale mazuri ambayo wanayafanya wachezaji.

"Kwa sasa mtazamo wangu ni kuandaa timu katika mechi moja moja, naelekeza nguvu zangu kwanza katika mechi ya Ligi Kuu ya Jumapili dhidi ya Dodoma Jiji kisha ndio nitaangalia mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya De Agosto.

"Kila mechi inakuwa na maandalizi yake, naendelea kuangalia kikosi katika mechi ya Jumatano dhidi ya Kipanga, kuangalia wachezaji wameshika wapi na nini hawajashika ili niweze kufanyia kazi," alisema Mgunda.

Simba inajiandaa na mchezo wa raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Primeiro de Agosto ambapo itaanzia ugenini Oktoba 9, kabla ya kurudiana Uwanja wa Benjamin Mkapa Oktoba 16, mwaka huu.

Timu itakayopata

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >